# Nipashe

Jumatatu Novemba 7, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581122

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US









**Walimu** kikaangoni kisa video chafu za wanafunzi kwenye mahafali ya shule

UKURASA 3



NIPASHE JUMATATU NOVEMBA 7, 2022

Nipashe Spotika

WAAMUZI 10 BORA WA WAKATI WOTE DUNIANI UK.16

ISIKUPITE

KIKOSI cha Pep Guardiola, Manchester City msimu huu ndani ya Ligi Kuu England: Mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean sheets' - Ederson (5), kinara wa ufungaji - Erling Halaand (18), pasi nyingi za mwisho 'assists' -Kevin De Bruyne (9), timu yenye mabao mengi - Manchester City (39).

NDIO ZANGU HIZI...

Beki wa Simba, Shomari Kapombe, akicheza mpira kwa kichwa wakati wa mazoezi ya timu hiyo kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Singida Big Stars itakayochezwa keshokutwa Jumatano kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida. Kushoto ni Jonas Mkude, mazoezi hayo yalifanyika juzi katika Uwanja wa Mo Simba Arena ulioko Bunju, Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**

UKURASA 13

# MSHTUKO

**MVUVI NA USHUHUDA**


"Abiria waliokuwa katika ndege walifungua mlango wa dharura, lakini hakuna aliyeweza kusema chochote, wakati wakiokolewa wengi wao walionekana kuwa na hofu."



• **Ndege** ya Kampuni ya Precision Air yaanguka ziwani na kusababisha vifo vya watu 19, wavuvi waokoa abiria... *Endelea ukurasa 2*

**UTATA VIFO VYA WATU WAWILI**

Utata umeibuka miili ya watu wawili iliyoopolewa eneo la tukio wakiwa si abiria wala wafanyakazi wa ndege.





Ndege ya Precision Air namba PW 494 ikiwa imeanguka katika Ziwa Victoria karibu na Uwanja wa Ndege wa Bukoba mkoani Kagera jana. **PICHA: MTANDAO**

**ALIYEOKOLEWA ANENA**

"Tulikwenda hadi Bukoba, alijaribu kutua bila mafanikio na kuzunguka muda mrefu na tulijulishwa tutarudi tena kwenye uwanja kujaribu kutua lakini ilishindikana na tukajikuta tupo kwenye maji."





RIPOTI MAALUM

## Kutoka kuwa wazalishaji wa chakula hadi kulia njaa

UKURASA 4

MICHEZO NABI AIPA ULINZI, MBINU YANGA UK.32 KABWELA UK.7

# Mshtuko ndege ikianguka ziwani

**Na Waandishi Wetu**

NI mshtuko! Ndivyo unavyoweza kusema kutokana na watu 19 kufariki dunia na wengine 26 kuokolewa katika ajali ya ndege iliyoanguka Ziwa Victoria jana.

Ndege hiyo ya Kampuni ya Precision Air yenye namba za usajili PW 494 inayotumia usajili wa ndege ya ATR-48 (PWF) ilizama Ziwa Victoria mita 500 kutoka eneo la kutua katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba mkoani Kagera.

Akizungumza jana jioni na wananchi na viongozi waliokuwa wanaokoa watu eneo la tukio, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alisema hadi muda huo, walithibitishwa kufariki dunia ni 19.

Waziri Mkuu alisema uchunguzi ulikuwa unaendelea kufanyika ili kubaini ongezeko la watu wawili ambao hawakuwa miongoni mwa abiria wa ndege hiyo, akibainisha kuwa marubani wa ndege hiyo walifariki dunia papohapo.

Taarifa iliyotolewa na serikali jana asubuhi, Shirika la Precision Air na mamlaka nyingine, ilibainisha ndege hiyo ilikuwa na abiria watu wazima 38, mtoto mmoja, marubani wawili na watoa huduma wawili.

"Tunaendelea na uchunguzi wa miili miwili iliyokutwa kwenye waliokufa kwa kuwa baada ya kuokoa watu 26, tulitegemea watabaki 17 lakini baadaye tumekuta wako 19," Waziri Mkuu alibainisha.

Majaliwa pia alitangaza kufungwa kwa shughuli zote za kutua kwa ndege katika Uwanja wa Ndege Bukoba hadi serikali itakavyojiridhisha baada ya usafi kufanyika na ndege iliyozama kutolewa.

Majaliwa akielezea ajali hiyo, alisema ni tukio ambalo halijawahi kutokea miaka mingi na kwamba wakati wa ajali, ndege hiyo ilitanguliza kichwa, hali iliyosababisha rubani kupoteza maisha.

Waziri Mkuu alisema vifaa vya kisasa kwa ajili ya uokoaji vilichelewa na kuwashukuru wananchi waliojitolea kwa kutumia vifaa duni walivyokuwa navyo.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, miili ya marehemu itaanza kutambuliwa baadaye na serikali itatoa taarifa kamili.

**KUTOKA HOSPITALINI**

Taarifa ya awali iliyotolewa asubuhi na Mganga Mkuu Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera, Dk. Isesanda Kaniki, ilibainisha kuwa waliofariki dunia ni wanaume wawili na mwanamke mmoja, wakati huo uokoaji ulikuwa unaendelea.

"Hadi sasa (majira ya saa sita mchana) tumepokea wenzetu 26 wakiwa hai, wanaume 17 na wanawake tisa. Tumepokea ndugu zetu watatu wamefariki dunia, wanaume wawili na mwanamke mmoja. Uokoaji unaendelea, kwa walio hai huduma zinaendelea kutolewa na hali zao zinaendelea vizuri," alisema.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Ndege la Precision Air, Patrick Mwanri, akibubujikwa machozi wakati akitangaza ajali ya ndege ya shirika hilo iliyotokea Bukoba mkoani Kagera jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**SALAMU ZA RAIS**

Kupitia ukurasa wake wa Twiter, jana majira ya saa 5:09 asubuhi, Rais Samia Suluhu Hassan aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya ajali ya ndege ya Shirika la Precision katika Ziwa Victoria mkoani Kagera. Ninatuma salamu za pole kwa wote walioathirika na ajali hii. Tuendelee kuwa watulivu wakati huu zoezi la uokoaji likiendelea huku tukimwomba Mungu atusaidie."

**HALI ILIVYOKUWA**

Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Alberth Chalamila, alitangaza majira ya saa tatu asubuhi kuwa watu 26 waliokolewa huku Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, William Mwampaghale akibainisha kuwa ajali hiyo ilitokea majira ya saa 2:35 asubuhi ikiwa ni mita 100 kabla ya kutua katika Uwanja wa Ndege wa Bukoba.

Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Zimamoto na Uokozi, Zabron Muhuma, alisema jeshi hilo lilikuwa linaendelea na uokoaji ili kuhakikisha ndege hiyo inatolewa majini.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na kampuni ya utengenezaji wa meli na vivuko ya Songolo Marine, mapema jana walipeleka msaada wa vifaa vya kusaidia kunyanyua ndege pamoja na kamba kwa ajili ya kufanikisha shughuli za uokoaji.

Wavuvi na wananchi wengine walionekana wakitumia kamba kuvuta ndege hiyo bila mafanikio, huku kamba walizokuwa wanatumia zikikatika.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima, alisema vifaa vilivyosafirishwa pamoja na askari watano wa uzamiaji kupitia njia ya maji vilitarajiwa kufika mkoani Kagera ndani ya saa mbili.

Mmoja ya wavuvi, Ashimu Rashidi alisema alishiriki kujitolea kuokoa abiria na walifanikiwa kuwatoa watu saba katika eneo la ufukwe wa Nyamukazi.

Alisema tatizo kubwa lilikuwa na ukosefu wa vifaa na kwamba kamba walizotumia zilikatika na kwamba wengi hawakuwa na uelewa wa kutosha kutekeleza kazi hiyo huku maji yakiendelea kujaa kwenye ndege hiyo.

"Asubuhi nikiwa Nyamukazi kama ilivyo desturi ya wavuvi, nilishuhudia ndege ikibadili mwelekeo wa kutua uwanjani na ghafla mlio ulisikika ziwani, tuliwasha boti kuelekea eneo la tukio.

"Abiria waliokuwa katika ndege walifungua mlango wa dharura, lakini hakuna aliyeweza kusema chochote, wakati wakiokolewa wengi wao walionekana kuwa na hofu," alisema.

**KAULI YA TAA, TCAA**

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), Mussa Mbura, akizungumza na Nipashe jana, alisema timu ya uchunguzi imetumwa kuchunguza chanzo cha ajali hiyo, akieleza kuwa uchunguzi wa awali unaonyesha ilitokana na hali mbaya ya hewa.

Kiongozi huyo aliyekuwa njiani kuelekea Bukoba, alimweleza mwandishi wetu kuwa uokoaji ulikuwa unaendelea na kutoa matibabu kwa waliookolewa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, katika taarifa yake kwa umma jana, alisema ndege hiyo yenye namba za usajili 5W-PWF ilishindwa kutua.

"Ndege hiyo ilitua kwenye maji umbali wa takriban mita 500 kutoka eneo la kutua ilikopaswa kutua, shughuli za uokoaji zinaendelea na mamlaka itatoa taarifa kamili baada ya suala hilo kukamilika," alisema Johari.

**MKURUGENZI ALIA**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Precision, Patrick Mwanri, jana asubuhi alitokwa na machozi mbele ya waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya ajali hiyo iliyohusisha ndege yao.

"Hii ndege ilikuwa inatoka Dar es Salaam kuelekea Bukoba na baada ya hapo ilikuwa inakwenda Mwanza na kurudi Dar es Salaam," alisema mkurugenzi huku akibubujikwa na machozi.

Alisema ndege hiyo ilitoka Dar es Salaam majira ya saa 12 asubuhi na walitarajia ingetua Bukoba saa 2:30 asubuhi, matokeo yake ilipofika saa 2:53 kituo chao cha operesheni kilipata taarifa ya ndege kutokufika.

Alisema walianza kuwasiliana na mamlaka husika ili kupata taarifa ya ndege hiyo na kujulishwa wakati inataka kutua Bukoba ilidondoka ziwani.

Mwanri alisema wanashirikiana na mamlaka zote za uokoaji nchini kuhakikisha suala hilo linafanyika kwa haraka, ili kuwaokoa watu hao na tayari walikuwa wamefungua kituo kwa ajili ya kuwasaidia familia za waathirika kwa Bukoba na Dar es Salaam, ili kuwapata taarifa ya kile kinachoendelea.

Alipoulizwa na Nipashe ni lini ndege hiyo imekwenda kwenye matengenezo ya mara kwa mara, alisema uchunguzi unaendelea, akiahidi kutoa taarifa utakapokamilika.

**ALIYEOKOLEWA**

Richard Komba, mmoja wa abiria waliookolewa, alisema: "Tulichelewa kuondoka Dar na tulipofika Mwanza, wakati tukielekea Bukoba, rubani alitujulisha kuwa hali ya hewa ni mbaya na kulikuwa na mtikisiko mkubwa.

"Tulikwenda hadi Bukoba, alijaribu kutua bila mafanikio na kuzunguka muda mrefu na tulijulishwa tutarudi tena kwenye uwanja kujaribu kutua lakini ilishindikana na tukajikuta tupo kwenye maji.

"Nilijikuta nipo kwenye maji, wale waliokaa mbele walishafunikwa, mimi nilikuwa nimekaa nyuma kabisa, tulikuwa na mhudumu mmoja alikuwa anajaribu kufungua mlango, alifanikiwa na baadaye tulitoka, tulikaa muda mrefu ikaja bodi ya wavuvi, wakatuchukua ila tulikuwa tunaogopa tusije tukazama maana boti ilikuwa ndogo na sisi ni wengi."

**WALIOKWAMA MWANZA**

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mukajanga, aliyekuwa anasafiri kwenda Bukoba kupitia Mwanza kwa ndege ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), alisema walikuwa wamekwama kuendelea na safari yao.

"Mimi na wafanyakazi wenzangu tulikuwa tunakwenda Bukoba kikazi, tumekwama kwa saa kadhaa hapa, tumeambiwa Uwanja wa Ndege wa Bukoba umefungwa kwa muda, hiyo ni dakika 15 hadi 20 tangu tumefika," alilieleza Nipashe majira ya saa 5:56 asubuhi.

"Tuko salama lakini wengi tumepata mshtuko, tumewekwa pamoja wakati tunasubiri utaratibu kama tutaendelea na safari au la," alibainisha.

Hata hivyo, ilivyotimu saa 6:10 mchana, walitangaziwa kwamba safari imesitishwa hadi watakapojulishwa kisha wakapelekwa hotelini kwa gharama za ATCL kwa ahadi kuwa uwanja utakapofunguliwa wataendelea na safari.

**USULI NA HISTORIA**

Ripoti ya ajali za ndege nchini zinabainisha kuwa tangu mwaka 1920 hadi 2013 zimewahi kutokea ajali 52 zilizosababisha vifo vya watu 196 huku idadi kubwa ya ajali hizo zikitokea maeneo ya milimani kutokana na hali mbaya ya hewa na ukosefu wa vyombo vya kuangalia hali ya hewa.

Ripoti hiyo inataja ajali ya ndege ya kwanza kutokea katika Ziwa Viktoria ni ndege aina ya Cessna 402B ya Shirika la Safari la Air Nairobi. Ajali hiyo iliyotokea Agosti 12, 1976 katika ziwa hilo mkoani Mwanza, watu 10 walipoteza maisha.

Ajali ya pili kutokea katika Ziwa Victori ni ya ndege ya IL76-TD mali ya Shirika la Air Trans Inc, Moldova iliyotokea Machi 23, 2005 mkoani Mwanza na kuua watu wanne.

Ndege nyingine zilizopata ajali nchini ni pamoja na Cessna 404 ya Shirika la Northern Air iliyotokea Septemba 9, 1999 katika Mlima Meru, Arusha ikisababisha vifo vya watu 12.

Nyingine ni Ndege Cessna 402b ya Shirika la Safari la Air Nairobi iliyotokea Agosti 12, 1976. Pia zilitokea ajali za ndege za Shirika la Ndege la Afrika Mashariki ndege DC-3 iliyotokea katika eneo la Mlima Kilimanjaro na kuua watu 20, ndege Vickers Viking ya Shirika la Ndege la Afrika ya Kati iliyotokea Machi, 1953 eneo la Mkuyuni, Handeni Tanga, walipoteza maisha watu 13.

Ajali nyingine ya ndege aina ya Cessina 206 5H-SAL 206 kutoka kampuni ya Safari Air Link ilitokea mkoani Arusha Agosti 9, 2017, alifariki dunia rubani aliyejulikana kwa jina la David Mbale (25), mkazi wa jijini Dar es Saalam.

**HISTORIA YA NDEGE**

Kwa mujibu wa Mtandao wa Usalama wa Ndege (Aviation Safety Network), ndege hiyo ni aina ya ATR 42-500 ina umri wa miaka 12 na miezi mitatu, iliruka kwa mara ya kwanza Agosti 16, 2010.

■**Imeandikwa na Restuta Damian (BUKOBA), Vitus Audax (MWANZA) na Beatrice Shayo (DAR)**.

# Walimu kikaangoni kisa video chafu za wanafunzi

**Na Jenifer Gilla**



WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (pichani) amesema serikali inaendelea kufuatilia utovu wa nidhamu uliofanywa na baadhi ya wanafunzi wa shule za Wilaya ya Kisarawe wakati wa mahafali ya kidato cha nne.

Amesema hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote walioruhusu vitendo hivyo kufanywa na wanafunzi, akibainisha kuwa uchunguzi wao wa awali umebaini walimu wamewapa wanafunzi uhuru kufanya mambo yasiyokuwa na maadili katika sherehe za shule.

Prof. Mkenda aliyasema hayo jana katika mahafali ya shule za Kiislamu za Ilala yaliyofanyika katika Uwanja wa Garden jijini Dar es Salaam na kuongeza kuwa video hizo zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii ziliishtua serikali, viongozi wa dini na jamii, wakiwamo wazazi.

"Na ninalaani vikali sana wale walioruhusu ule mchezo wa shule hizo pale Kisarawe na picha zikapigwa, haiwezekani walimu hawakujua, hairuhusiwi na tunaahidi kwamba tutachukua hatua zaidi," alisema.

Waziri Mkenda alisema serikali haitoivumilia shule isiyozingatia maadili mema, akiwaagiza viongozi wa dini kwa kushirikiana na walimu na wamiliki wa shule kuhakikisha suala hilo linakuwa kipaumbele katika malezi ya watoto.

Alisema wazazi wamewapa shule jukumu la kuwalea watoto wao katika misingi mizuri ikiwamo kuwakuza kimaadili kwa kuwa wanakaa nao muda mrefu, hivyo walimu wahakikishe jambo hilo linatekelezeka na serikali itakuwa pamoja nao.

"Tunahitaji katika shule zetu kuona watoto wanapata malezi ambayo wazazi wanatarajia, wazazi walitukabidhi watoto wao, wanataka shule zetu ziendeleze malezi ambayo wao wangependa kuyaendeleza na serikali imeweka amri kwamba mwanao lazima aende shuleni," alisema Mkenda.

Alisema suala hilo pia linapaswa lizingatiwe katika kusimamia mitihani na kulaani tabia ya baadhi ya walimu kujihusisha kimapenzi na wanafunzi, akisisitiza serikali itahakikisha tabia hizo zinakomeshwa na wanaofanya wanadhibitiwa kulingana na sheria za nchi.

Waziri huyo pia alisema atalipa msukumo serikalini somo la Kiarabu ili lifundishwe kidato cha tano na cha sita kuzalisha wataalamu watakaokwenda kufanya kazi za tafsiri kimataifa.

Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhaj Musa Salim alisema katika Uislamu suala la elimu limepewa kipaumbele, kwamba tangu mtu anapozaliwa hadi anapofariki dunia anapaswa kuendelea kujifunza, hivyo kuwataka wanafunzi hao kuishika elimu.

"Tunawataka watoto wetu tunaowaaga leo na watakaoendelea, kushikamana na maadili, elimu haina maana yote mbele ya jamii iliyokosa maadili, ninyi ndiyo taifa la baadaye, nchi hii inawategemea katika suala la maadili, endapo taifa litakosa maadili ni sawa na kusema taifa hilo ni mfu," alionya.

Aliitaka jamii ya Kiislamu kujitafakari kwa kuwa ndiyo inayoongoza kwa mmomonyoko wa maadili, akitolea mfano kuwa kati ya 'panyaroad' 10, saba ni waislamu, jambo linaloitia aibu serikali na jamii kwa ujumla.

Akitoa taarifa ya maendeleo ya shule hizo, Mkuu wa Shule ya Al Haramain, Buhero Issa alisema mahafali hayo yanafanyika kwa mara ya 11 na kuhusisha shule 11 za Kiislamu kutoka Dar es Salaam. Shule hizo ni za sekondari Kunduchi na Ununio, Tekeme Islamic, Muzdarfa Islamic, Dar es Salaam Islamic, Al Haramain na Hijra Islamic, Nuru Islamic na Kinondoni Muslim.

Alisema shule hizo zimekuwa zikifanya vizuri kitaaluma na mwaka jana asilimia 98 ya wanafunzi katika shule hizo walifanikiwa kujiunga na kidato cha tano.

Alisema shule hizo zinakabiliwa na shida ya mmomonyoko wa maadili ya wanafunzi, somo la dini kutotahiniwa na Baraza la Mitihani (NECTA) na kutohesabiwa katika madaraja kidato cha nne.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wa kidato cha nne, mmoja wa wahitimu hao, Mwanaisha Khadir alisema wanategemea kupata matokeo mazuri na kuendelea na masomo ya juu kwa kuwa wameandaliwa vyema na walimu wao.

# Wawili mbaroni kwa kukutwa na ng'ombe 17 wanaodaiwa kuwaiba

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

POLISI mkoani Ruvuma inawashikilia watu wawili jamii ya wafugaji kwa tuhuma za wizi wa ng'ombe 17 wenye thamani ya Sh. milioni 14 mali ya Ajili Mgomile, mkazi wa Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi.

Akizungumza na Nipashe jana mjini hapo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Marko Chilya, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Ally Salebi (25), mkazi wa Kijiji cha Namatindi, Kata ya Kilimalondo wilayani Nachingwea na Omari Kitenge (22), mkazi wa kijiji cha Tinginya wilayani Tunduru.

Kamanda Chilya alisema tukio hilo lilitokea Novemba 4, majira ya saa nane mchana katika Kijiji cha Misufini, Tarafa ya Nakapanya, wilayani Tunduru ambako askari Polisi wakiwa katika operesheni ya kuwatafuta wahalifu waliwakamata watuhumiwa wakiwa na ng'ombe hao wa wizi.

Alisema siku ya tukio watuhumiwa walifika nyumbani kwa Ngomile majira ya saa za usiku kuvunja zizi kisha kuondoka nao kwa kupitia njia za porini hadi eneo la mlima Ndondocha.

Kamanda alisema Kijiji cha Tinginya wilayani Tunduru waliweka mpango wa kuwauza ng'ombe hao, lakini Polisi waliwahi kuwamata na wanatarajiwa kufikishwa mahakamani baada ya upelelezi wa tukio hilo kukamilika.

Aliwaonya wanaojihusisha na matukio ya wizi wa mifugo na kisha kukimbilia Mkoa wa Ruvuma kwa kufikiri ni sehemu ya maficho, waache mara moja.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA KAGERA LILILOPO BUKOBA

MAOMBI MADOGO NA. 156/2022

METHODIA JUSTINIAN
WILSON NYAKAYANGO ..........................WENYE TUZO

DHIDI YA

FELIX MLENGEKI .........................MSHINDWA HUKUMU

KWA: FELIX MLENGEKI (POPOTE PALE ULIPO)

Unaarifiwa kuwa Maombi Madogo Na. 156/2022 yamepangwa kutajwa terehe 18.11.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2:00 asubuhi. Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na huduma kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 03/11/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

KUPOTEA KWA VYETI



**HENERICO J. WAYA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0332/0203** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOROGORO Sekondari mwaka 2005. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0660/0514** cha MOROGORO TEACHERS COLLEGE mwaka 2006. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **WMB/RB/3000/2022.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO SOKOINE WILAYA YA MVOMERO MKOA WA MOROGORO

SHAURI LA NDOA Na 01/....2022

JINA LA MDAI: ESTER MOSHI

JINA LA MDAIWA: JUAKALI MNYEGELE

KUITWA SHAURINI MDAIWA

(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: JUAKALI MNYEGELE WA MSATA................MDAIWA

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba:Kuomba kuvunja ndoa na kupatiwa talaka na matunzo ya mtoto. Kwa hiyo unatakiwa Kuhuduria binafsi katika mahakama hii tarehe 14/11/2022 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO:Kama hautohudhulia siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitishwa kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 02/11/2022

Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo
Futa lisilotakiwa*
FAHAMU:

SUMMONS TO APPEAR (Order V,R (1) of CPC
(Substituted service)
IN THE HIGH COURT OF THE UNITED RWPUBLIC OF TANZANIA
(IN THE DISTRICT REGISTRY OF ARUSHA)

AT ARUSHA

APPLUCATION FOR EXCUTION NO.29 OF 2022.

CHARLES MARCO NAIBALA.....DECREE HOLDER

VERSUS

THOMAS MARCO NAIBALA..... JUDGEMENT HOLDER

NOTICE OF MENTION

TO: THOMAS MARCO NAIBALA

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for Mention in the High court at Arusha on 13th day of December,2022 at 09:00 am in the forenoon.
YOU may appear in person or by advocate or agent duly authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents which you intend to rely upon in support of your case.
**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time for mention,the court may proceed in your absence.
GIVEN under my hand and seal of the court this 1st day of November,2022.

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF ARUSHA

KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENARD MWAISULE SILA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 370 DFY – MASSEY FERGUSON.** Chassis namba **9B76230.** Engine namba **5AFE53247.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/431538/2022.**

KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY IKOME MURUKE** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo (Degree of Bachelor of Commerce (Finance) chenye Registration **No. 2013-04-04023** cha UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi: Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/90618/2022.**

JAMHURIYA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA
Katika Mahakama ya Mwanzo wilaya ya KIGOMA
**Kituo cha:** UJIJI
**Mkoa:** KIGOMA
Shauri la Madai/Ndoa la **NA. 146 MWAKA 2022**
**Jina la Mdai:** OMARY MUSSA
**Jina la Mdaiwa:** JUMA MASHAKA
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(Kanuni ya 18 ya Kanuni za Taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo )

**Kwa: JUMA MASHAKA**
Kwakuwa Mdai/Wadai amelete/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) FIKA MAHAKAMANI..........................Kwahiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 9 Mwezi 11 Mwaka 2022 saa 2:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakam hili leo tarehe 3 Mwezi wa 11, Mwaka 2022.

**HAKIMU**

KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**PENDO EDWARD MLIGO** anatangaza kupote kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba **MC885 CBJ**, ENGINE NAMBA:AK-4KJ4772680 na CHASSIS NAMBA: MD6M-14PA0J4K61183. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**MKB/1R/RB/189/2022**

# Kutoka kuwa wazalishaji wa chakula hadi kulia njaa

**Na Jenifer Gilla, aliyekuwa**
HANDENI



Mkulima Safia Mselemu akionesha hali ilivyo shambani kwake kutokana na ukame. **PICHA: JENIFER GILLA**

NI majira ya asubuhi, anaonekana Safia Mselemu (72), mkazi wa Kijiji cha Sindeni, Kata ya Sindeni, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, akiwa katikati shamba lake lenye ukubwa wa ekari nne anazotarajia kupanda mahindi, anatazama juu kuhakiki hali ya mawingu kama inaleta matumaini ya mvua kunyesha.

Mama huyo wa watoto wanane na wajukuu wanne, anabainisha mazoea yao mwezi Novemba kunakuwa na mvua za vuli na wakulima kupanda mazao, lakini mwaka huu hali ni tofauti.

Anairejea taarifa iliyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) Septemba 2, mwaka huu, kwamba maeneo ya nchi yanayopata misimu miwili ya mvua, yanatarajiwa kupata mvua chini ya wastani hadi wastani, lakini anajipa moyo pengine mambo yatakuwa tofauti kwao.

Taarifa hiyo ya TMA inafafanua kutakuwa na ongezeko la joto katika msimu wa vuli hususani katika maeneo ya kaskazini mwa mikoa ya Morogoro na maeneo ya mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar, Arusha, Manyara na Kilimanjaro.

Safia anabainisha kuwa kwa takribani miaka mitatu sasa, shughuli za kilimo zimezorota kwao kutokana na mvua kutonyesha kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa, hali inayomweka katika hatari ya kukumbwa na uhaba wa chakula.

Mama huyo anayetamba kuwa mbobezi katika kilimo cha mahindi, akiwa na miongo miwili kwenye sekta hiyo, anasema analima kwa ajili ya biashara lakini tangu mwaka 2019, mavuno yake yamekuwa kidogo na kwamba kiasi kilichopatikana, walikitumia kwa chakula nyumbani na wakati mwingine havuni kabisa.

"Zamani katika ekari nne nilikuwa ninavuna magunia 40 hadi 50 ya mahindi lakini mwaka 2020 nilipata magunia 10, mwaka 2021 nilipata magunia matatu na mwaka huu mavuno ya masika sikupata kitu kabisa kwa sababu mvua haikunyesha kwa wakati na iliponyesha ikawa kubwa kupitiliza," anasema.

Safia aliyerithi mashamba hayo kutoka kwa baba yake, anasema alikuwa akitoa huduma kwa familia yake ya watoto wanane kupitia kilimo ambapo gunia moja la mahindi alikuwa akiuza Sh. 70,000 hadi 100,000, jambo ambalo kwa sasa linaonekana kugeuka historia.

"Kuna wakati siamini kama ni mimi niliyekuwa ninahudumia familia yangu, sasa nimekuwa maskini, hata chakula cha nyumbani pia sina, utajiri niliotegemea kurithisha wajukuu zangu unaangamia taratibu," analalama.

Shida hiyo haipo kwa Safia peke yake, kwani udadisi wa Nipashe umebaini ni tatizo kwa wakazi takribani 6,675 wa kijiji hicho, ambao kwa mchanganuo, wanawake ni 3,369 na wanaume 3,306 (Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012).


Selemani Hamza, mkazi wa kijiji hicho, anasema alisimulia alikuwa anapata faida isiyopungua Sh. milioni tatu kwa kuuza magunia 30 aliyokuwa akivuna, fedha alizotumia kumsomesha mtoto wake shule ya binafsi, lakini tangu mwaka juzi amekuwa akiambulia gunia moja la mahindi katika shamba lake la ekari mbili.

"Nimeshindwa kumsomesha kijana wangu tangu mwaka jana, kwa sababu shule anayosoma ada yake ni Sh. 600,000 kwa mwaka, imebidi niombe msaada kwa kaka zangu, nina miaka miwili sasa sipati mazao yoyote. Kwa kweli nimekata tamaa," Hamza anasema.

Anabainisha kuwa hata upatikanaji wa chakula nyumbani kwake umekuwa wa shida na sasa analazimika kutumia Sh. 5,000 kila siku kununua chakula cha kulisha familia yake, hali iliyomfanya kuingia katika biashara ya kuuza mkaa licha ya kutambua hatari yake katika uharibifu wa misitu na kuchangia uhaba wa mvua.

Saida Salehe (35), mkazi mwingine wa kijiji hicho anasema ukame huo umesababisha kukosa chakula, hali iliyochangia walazimike kupunguza milo nyumbani, sasa wakiambulia miwili kwa siku ili wamudu gharama za maisha kwa kuwa walikuwa wanategemea kilimo kujikimu.

"Mwaka juzi nililima, wakati mahindi yanakaribia kukomaa ikanyesha mvua kubwa yakaoza yote. Mwaka huu haijanyesha kabisa, nimeona niuze maandazi ili nihudumie familia, lakini kwa siku ninapata faida ya Sh. 2,000 ambayo haitoshi kuhudumia wanafamilia ya watano nilionao. Kwa hiyo, tukishakunywa chai asubuhi, tunasubiri jioni ndipo tunakula tena," anafafanua.




### KILIO KWA SERIKALI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sindeni, Haji Mhina anakiri kuwapo uhaba wa chakula kijijini huko na kuiomba serikali iwapatie chakula cha bei nafuu ili wamudu gharama za maisha.

"Tatizo hilo limekuwa kubwa katika eneo hili kwa sababu ukame umekuwa mkali na hatujui utaisha lini kwa sababu mvua hakuna. Tumelizungumza hata kwenye vikao vya kata kwamba watupelekee taarifa huko juu (halmashauri) watuletee chakula, hatutaki cha bure, tunataka cha bei nafuu," anasema.

Mwenyekiti huyo alisema kuwa kwa hali ilivyo kijijini huko, wanakijiji wanahitaji chakula kitakachouzwa chini ya Sh. 1,000 kwa kilo moja kwa kuwa vyanzo vyao vya mapato vyote vimeathirika na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Sindeni, Ramla Haruna, anabainisha kuwa kinachoshuhudiwa huko kwa sasa, kimetokana na mabadiliko ya tabianchi anayoyataja kurudisha nyuma shughuli za kilimo katika kata hiyo na kuchangia uhaba wa chakula.

"Msimu uliopita wa masika mvua ilikuwa kidogo na watu hawakupata mazao, uzalishaji ukapungua na hizi za vuli zinazonyesha mwezi wa 10 (Oktoba) mpaka sasa hakuna kitu. Kwa hiyo, matarajio ya kupata chakula kwa mwaka huu pia hakuna.

"Kufuatia hali hii, tumepeleka muhtasari wa kuiomba halmashauri chakula cha bei nafuu lakini mpaka sasa hawajatupatia majibu yoyote huku vyakula vikiuzwa bei ya juu ambayo wanakijiji hawawezi kuimudu kwa kuwa wengi wanategemea kilimo na ufugaji kupata fedha," ofisa huyo anasema.

Mkulima Zuwena Abdi ana hoja nyingine kwamba eneo hilo sasa linakabiliwa na uhaba wa maji ambao unaongeza ugumu wa maisha kwa kuwa wanashindwa hata kulima mboga za majani katika makazi yao.

"Kwa sasa maji nayo yamekuwa ya shida, ukame umechachamaa, jua limekuwa kali mno. Hata kupanda mboga nje ya nyumba ninashindwa, kwa sababu hata ukipanda, baada ya siku mbili tu unaona zinanyauka kwa jua," anasimulia.

Mama huyo wa watoto watatu anasema hali hiyo inamwongezea gharama za maisha kwa sababu mbali na kununua unga wa mahindi kwa Sh. 1,800 kwa kilo, pia analazimika kununua fungu la mboga za majani kwa Sh. 300, jambo ambalo miaka iliyopita lilikuwa anasa kwake.

### HALI YA WILAYA

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Yibaria Kamele, anasema wamefanya tathmini na kubaini upatikanaji wa chakula kikuu ambacho ni mahindi katika wilaya hiyo umeshuka kutoka asilimia 90 mwaka 2020 hadi asilimia 37 mwaka huu, sawa na upungufu tani 78,000.

"Sindeni imeathirika zaidi kwa sababu ni kukame zaidi kulinganisha na kata zingine kama vile Michungwani. Sasa ukijumlisha na athari za mabadiliko ya tabianchi, kumesababisha upatikanaji wa mazao yaliyozoeleka kama vile mahindi kuwa chini ya wastani kwa kipindi cha miaka miwili, hali inayosababisha uhaba wa chakula," anafafanua.

Katika kukabiliana na shida hiyo, Kamele anasema halmashauri imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi kupanda mazao yanayostahimili ukame kama vile mihogo, kunde, choroko na mahindi yanayokua kwa muda mfupi.

"Kwa kweli tunashukuru kwa sasa tuna mihogo ya kutosha ambayo inasaidia kupunguza makali ya ukosefu wa chakula, tatizo lililoko ni kuwa wananchi wamezoea chakula chao kikuu ambacho ni mahindi. Kwa hiyo, mihogo wanaichukulia kama chakula cha asubuhi," anasema.

Ofisa huyo pia anasema wanashirikiana na Wizara ya Kilimo na mashirika binafsi, likiwamo la Save the Children na World Vision, kuisaidia jamii kupunguza makali.

Anasema ushirikiano wao huo unajumuisha kutoa chakula kwa shule takribani 24 zilizoko katika Tarafa ya Magamba katika halmashauri hiyo.

Kamele pia anasema wameshaandaa mpango mkakati wa dharura wa kusaidia kata zilizoathirika zaidi, ikiwamo Sindeni, kukabiliana na uhaba wa chakula kwa kutoa elimu na kuwapatia mbegu za mazao yanayohimili ukame, hasa mihogo.

■ITAENDELEA KESHO

## HABARI KITAIFA

# Waziri Gwajima: Wanaume washirikishwe kupinga ukatili

**Na Mwandishi Wetu,** INSTANBUL

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (pichani), ametoa wito kwa wadau wote duniani kuona umuhimu wa wanaume kushiriki vita dhidi ya ukatili wa kijinsia unaowaathiri zaidi wanawake na watoto.

Dk. Dorothy aliyasema hayo kwenye Mkutano wa Tano wa Kimataifa wa Wanawake na Haki uliofanyika jijini Instabul, Uturuki juzi, akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan.

Akitoa salamu za Rais Samia, Waziri Dorothy, aliishukuru Serikali ya Uturuki kwa mwaliko wa mkutano huo wenye Kaulimbiu ya Kanuni za Kimataduni na Wanawake, akisema maendeleo ya kijamii na vizazi siyo suala la wanawake tu, bali ya jamii yote.

Waziri huyo alieleza jitihada zinazofanywa na Serikali ya Tanzania katika kuwezesha maendeleo yanayozingatia usawa wa kijinsia na kutokomeza ukatili kwa wanawake unaochangiwa na mila na desturi potofu.

Alisema kuwa sambamba na kuendelea kutekeleza makubaliano ya kikanda na kimataifa kuhusu wanawake na maendeleo kuelekea usawa wa kijinsia, wanawake wanaendelea kuwezeshwa kwenye elimu, uongozi wa kisiasa, kitaaluma na kijamii.

Alibainisha uwiano wa uandikishaji wa watoto wa kiume na wa kike shule ya msingi kufikia 1:1 huku serikali ikitekeleza mpango wa elimu bila ada kuanzia shule ya msingi hadi sekondari.

Alisema Tanzania inatekeleza mpango wa kujenga shule moja maalum ya sekondari kwa wasichana katika mikoa yote 26 nchini kwa ajili ya kufundisha masomo



ya sayansi, teknolojia, injinia na hesabu (STEM), jambo ambalo litawainua watoto wa kike kielimu.

Kuhusu wanawake na uongozi, waziri huyo alieleza mkutano huo kuwa Tanzania ipo mstari wa mbele katika kuwainua wanawake.

Alisema Tanzania pia inafanya vizuri katika eneo hili ikiwa na wabunge wengi wanawake, huku mabalozi wanawake na majaji wanawake wakiongezeka na ongezeko hilo limeenda sekta zote na ngazi zote.

Waziri huyo aliwataka wadau wa mkutano huo na dunia kwa ujumla kuona umuhimu wa kuhakikisha ushiriki wa wanaume katika vita vya kupinga ukatili wa kijinsia unaoathiri zaidi wanawake na watoto huku akirejea uchache wa wanaume kwenye mkutano huo.

Rais wa Jamhuri ya Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, aliyekuwa mgeni rasmi katika mkutano huo, katika hotuba yake alikemea vikali vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake, akisisitiza ukatili ni usaliti.

Mkutano huo ulioandaliwa na Serikali ya Uturuki kupitia Wizara ya Familia na Huduma za Kijamii ikishirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya Wanawake na Demokrasia (KADEM), uliohudhuriwa na mawaziri toka nchi mbalimbali duniani.

Waziri Dorothy alitumia fursa hiyo kufanya mikutano ya pembeni na mawaziri wa nchi za Algeria na Libya na kujadili umuhimu wa kuimarisha ushirikiano katika kufanikisha maendeleo ya wanawake, jambo ambalo litaratibiwa na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa nchini.

# Makandarasi wanawake wapatiwa elimu ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imetoa elimu kuhusu masuala ya fedha kwa mamia ya makandarasi wanawake wa Kitanzania waliokutana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa makandarasi hao ulioandaliwa na Chama cha Makandarasi Wanawake Tanzania (TWCA).

Mkutano huo ulifadhiliwa na Benki ya NMB kwa Sh. milioni 10, ukifanyika chini ya kaulimbiu 'Elimu ya Fedha kwa Maendeleo Endelevu ya Biashara na Viwanda'.

Akizungumza wakati wa kongamano hilo, Ofisa Mkuu Huduma Shirikishi wa Benki ya NMB, Nenyuata Mejooli, alisema benki hiyo imedhamiria kufanikisha ushirikishwaji wa kifedha nchini na itaendelea kufanyia kazi azma hiyo kwa kusambaza huduma za kibenki kwa wafanyabiashara wasio na benki ikiwa ni pamoja na biashara zinazomilikiwa na wanawake, jamii na watu binafsi kote nchini kupitia mtandao wake mpana wa matawi zaidi ya 228, zaidi ya ATM 750 na mawakala wa benki 17,000.

"Mwaka 2020, benki yetu ilizindua jukwaa la wanawake yaani 'NMB Jasiri' lenye lengo la kuwapa wanawake suluhisho na huduma kama mikopo yenye vigezo nafuu, amana za uwekezaji na akiba kwa njia ya kidigitali, mafunzo, maonyesho na warsha kama hizi," alisema.

Mejooli alisema kwa mwaka huu kupitia jukwaa hilo hilo la NMB Jasiri, benki yake imepeleka neema kwa wanawake makandarasi kwa njia ya mikopo na kuongeza kuwa tayari benki imetoa mikopo 30 kwa wanawake makandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 1.8.

Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolata Ngimbwa wakati wa hafla hiyo, alipongeza ushirikiano wa NMB na chama cha wanawake na kuwataka makandarasi wanawake kuzingatia ufanisi wanapotekeleza majukumu yao.

"Fanyeni kazi kitaalamu mnapopata zabuni kwa kutumia watu wenye uwezo na wenye taaluma. Hi itasaidia kampuni zinazomilikiwa na wanawake kukua na kupiga hatua.

"Pia mnapaswa kuja na takwimu halisi katika zabuni zenu kwani kununukuu kiasi kidogo kunakuhakikishia zabuni tu lakini biashara yako haitakuwa uendelevu wa biashara," alisisitiza.

Rais wa TWCA, Judith Odunga wakati wa hafla hiyo, aliitaka NMB kutafuta njia za kutoa mikopo kwa makandarasi wanawake ili kuwawezesha kununua mitambo ya kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Tunaiomba benki kutoa mikopo kwa makandarasi wanawake ili kuwawezesha kukuza biashara zao na hii itawawezesha kushindana vyema.

"Kwa sasa, kampuni nyingi za wanawake makandarasi zipo kwenye daraja 6 na 7 na nia yetu ni kuona kampuni hizo zikipiga hatua. Inapowezekana, benki inapaswa kukubali mitambo yao kama dhamana," alisema.

Awali, mmoja wa mlezi wa chama hicho, Getrude Mongella aliwataka makandarasi wanawake kujituma zaidi na kubuni mbinu za kutafuta fursa za biashara zilizopo katika sekta ya ujenzi huku akisisitiza kuwa sekta hiyo ni miongoni mwa sekta zinazotengewa fedha kubwa katika bajeti ya serikali kila mwaka.

"Kuna fedha nyingi katika sekta ya ujenzi. Wanawake wanahitaji kuweka mikakati na kunyakua fursa katika sekta hiyo kikamilifu," Mongella alisema.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Aisha Amour, wakati wa hafla hiyo, alisema tayari serikali imeweka mazingira mazuri ya biashara na sera za kuwezesha wanawake kushiriki kikamilifu katika sekta ya ujenzi.

Aliwataka wanawake kuunda ushirikiano na ubia kwenye kampuni na kuongeza kuwa itasaidia kuboresha ufanisi wao na utoaji wa huduma.

"Kampuni za wanawake lazima ziunde ubia kama zinataka kushindana kikamilifu kupata zabuni kubwa. Nia ya serikali ni kuona kampuni ya ndani zinakua na sisi kama serikali tunaendela kuboresha sera zitakazoboresha mazingira ya biashara," alisisitiza.


The Guardian Limited

VACANCY

Freelancer Sales Executive

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales personnel to join our advertising sales team in **Dar es Salaam, Mwanza and Kilimanjaro.**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration or Sales & Marketing
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

Please send application via Email to
vacancy@guardian.co.tz
before 15th November, 2022.

617131002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga ikipambana Tunisia makundi CAF inawezekana

**KLABU** ya Yanga tayari imetua nchini Tunisia tangu Jumamosi wiki hii na kuweka kambi mji wa Sousse umbali wa takriban Km. 140 kufika Jiji la Tunis utakapochezwa mchezo wao wa mkondo wa pili wa mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain.

Keshokutwa, Jumatano Yanga itashuka katika Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi kuwavaa wenyeji wao, Club Africain, ikiwa na lengo moja tu kupata ushindi ama sare ya mabao ili kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika baada ya mechi ya mkondo wa kwanza katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kulazimishwa sare tasa.

Yanga inashuka dimbani huku mashabiki wake wengi nchini wakibaki wamekata tamaa ya timu yao kufanya vizuri katika mchezo huo na kufuzu kutokana na rekodi nzuri ya timu za Ukanda wa Kaskazini, maarufu timu za Kiarabu zikicheza viwanja vya nyumbani.

Pamoja na hofu hiyo kubwa kwa mashabiki, sisi tunaamini hakuna kinachoshindikana kwa Yanga kama wachezaji wakiingia uwanjani kwa ari kubwa na lengo la kupambana mwanzo mwisho kwa dakika 90 za mchezo.

Hiyo ni kutokana na mifano hai ambayo tunayo, mosi ikiwa ni mechi ya michuano hiyo ya CAF mwaka 2003 ambapo mechi ya kwanza Simba ikiwa nyumbani ilishinda 1-0 na kwenda ugenini nchini Misri wenyeji wakapata matokeo kama hayo, lakini Simba ikasonga baada ya kuitoa kwa penalti 3-2.

Mfano mwingine ni mwaka 1979, kwenye michuano hiyo ya CAF, Simba ilikubali kichapo cha mabao 4-0 nyumbani dhidi ya Mufulira Wanderers ya Zambia na wakati wengi wakiwa wamekata tamaa ilienda ugenini na kupindua matokeo kwa kusonga mbele kwa ushindi wa mabao 5-0, hivyo matokeo ya kikatili katika soka yapo na hilo linawezekana pia kwa Yanga.

Hii inatuonyesha kwamba wachezaji waliamini mechi haijaisha hadi dakika 90 za pili ugenini zitakapomalizika, hivyo kwenda kwa lengo moja tu la kupambania matokeo jambo ambalo linawezekana pia kwa Yanga ambayo inahitaji sare yoyote ya mabao ama ushindi ili kufuzu hatua ya makundi.

Na kama matokeo yatakuwa suluhu, timu hizo zitaingia katika changamoto ya mikwaju ya penalti ambayo siku zote haina mwenyewe, hivyo kinachotakiwa kwa Yanga ni wachezaji kuamini wanaweza huku wakijituma mwanzo mwisho wa dakika 90 za pili nchini Tunisia.


Tunaamini benchi la ufundi na wachezaji wa Yanga wameona ubora na udhaifu wa wapinzani wao hao, hivyo kwa muda wa wiki nzima waliyokuwa nayo, umetosha kufanyia kazi kasoro zao na uimara wa Club Africain ili kupata matokeo keshokutwa.

Lengo letu kama ambavyo tumekuwa tukieleza siku zote pindi klabu za Tanzania zinapoiwakilisha nchini, ni kuona zinasonga mbele na kuliletea taifa sifa lakini pia katika mchezo hii ni muhimu kwa Yanga kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho baada ya kushindwa kufanya hivyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika na kushuhudia watani zao, Simba wakisonga mbele.

Hilo likitokea kwa Yanga, maana yake nchi itakuwa na timu mbili kwenye michuano hiyo ya CAF, hivyo kuiongezea pointi nyingi na kuiweka Tanzania katika nafasi nzuri zaidi ya kuingiza timu nne tena kwenye michuano hiyo msimu ujao.

Tunataka kuona suala Tanzania kuingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF linakuwa la kawaida kila msimu kama ilivyo kwa Misri, Morocco, Tunisia na nchi nyinginezo, hivyo katika hili hakuna njia ya mkato zaidi ya klabu zetu kupambana zaidi na kufika angalau hatua ya robo fainali, nusu na ikiwezekana fainali kila msimu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kongole Simba Queens CAF, endeleeni kuiheshimisha nchi

Na Adam Fungamwango

**HISTORIA** imeandikwa, baada ya timu ya soka ya Wanawake ya Klabu ya Simba, Simba Queens, kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Ikiwa nchini Morocco ambapo michuano hiyo inachezwa, juzi timu hiyo iliibamiza Green Buffaloes ya Zambia mabao 2-0 yaliyowekwa wavuni na mastraika wake wawili, Asha Djaffar raia wa Burundi na nahodha wa timu hiyo Opa Clement.

Ilikuwa ni siku ya furaha si tu kwa Watanzania, bali Ukanda wote wa Afrika Mashariki na kati. Ikumbukwe kuwa michuano hii inachezwa kwa washindi wa kanda saba za Afrika, hivyo Simba Queens ilikuwa ni bingwa wa Ukanda wa CECAFA, hivyo ilikuwa ikiziwakilisha nchi zote za ukanda huo.

Na hii ni mara ya kwanza kwa timu kutoka ukanda huu kufika hatua hiyo kwenye michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF).

Cha kufurahisha ni kwamba wameifunga timu ambayo si tu Mabingwa wa Zambia, lakini ndiyo bingwa pia wa Ukanda wa COSAFA na mwakilishi wa kanda hiyo, kwani Mamelodi Sundowns Queens inashiriki kama bingwa mtetezi.

Si kazi rahisi na wala haikuwa kazi ndogo kufika hapo ilipofika kwani pamoja na viongozi wa klabu hiyo kabla ya michuano hiyo kubainisha kuwa lengo ni kufikia hatua hiyo, lakini haikufanikiwa.

Naandika hili ikikumbukwa kuwa kwenye mechi ya kwanza tu ya Kundi A ilichapwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji, Asfar ya Morocco na ikawa kama safari hiyo imewekewa kizingiti, hivyo kuhitaji ushindi kwenye mechi zote mbili zilizobaki.

Kwenye mechi iliyofuata iliifunga Determine ya Liberia mabao 2-0, matokeo ambayo bado yalikuwa hayaipi uhakika wa moja kwa moja kusonga mbele.

Kwa bahati mbaya sana kwenye mechi ya mwisho ilicheza na timu ngumu ya Green Buffaloes ambapo mbali na kuwa ina wachezaji wengi wenye uwezo mkubwa, na asilimia kubwa wakiwa wanaichezea timu ya Taifa ya Zambia ambao walikuwapo kwenye michuano ya AFCON iliyofanyika nchini Morocco Julai mwaka huu na wakatolewa hatua ya robo fainali na Afrika Kusini.

Niliwaona zaidi ya wachezaji watano wa timu hiyo waliokuwa AFCON, kwa maana hiyo walicheza na timu ngumu, ambayo pia nayo ilikuwa inawania kufuzu hatua hiyo kwa hali yoyote ile.

Ikawa ni kama mechi ya fainali kwa Simba Queens, tena haikutakiwa hata sare kwa sababu isingefuzu zaidi ya ushindi.

Kutokana na uwekezaji wa Mohamed 'Mo' Dewji, na safu yote ya uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi, benchi la ufundi yalifanyika maandalizi kabambe ambayo yamewezesha kufikia ndoto iliyokuwa inaotwa, tena kwa muda mfupi tu kwenye soka la kinadada.

Hongera nyingine ziende kwa wachezaji kwa sababu mbali na matatizo ya hapa na pale ya kiufundi, lakini walionekana kucheza kwa kujituma na ari kubwa ya upambanaji na ndiyo kwa kiasi kikubwa siri ya mafanikio.

Ukiangalia wachezaji wa Simba Queens wanaoshiriki fainali hizo za Ligi ya Mabingwa ni wale wale tu ambao walicheza hatua za awali ya ligi hiyo kwenye kanda na hakuna mchezaji aliyeongezeka.

Si kwa sababu haina wachezaji wengine wapya, bali walikataliwa na CAF kwa sababu ya kusajiliwa nje ya muda. Kwa mujibu wa Meneja wa Klabu ya Simba Queens, Selemani Makanga, wachezaji hao ni straika Jentrix Shikangwa na kiungo Ruth Ingotsi wote raia wa Kenya ambao waliongezwa kwa ajili ya kukipa nguvu kikosi, lakini ikashindikana.

"Hawa tuna mkataba nao, lakini kwa bahati mbaya tuliwasajili wakati dirisha limefungwa, tumejaribu kupambana sana lakini imeshindikana. Unajua walimaliza mikataba yao wakati dirisha likiwa wazi na walikuwa hawajapata timu, wakaja kupata wakati dirisha limefungwa.

FIFA inasema kama dirisha lingekuwa limefungwa kabla mikataba yao kumalizika,

# Polisi yashtuka raia kuwaua watuhumiwa

**Na Neema Hussein,** KATAVI

SIKU chache baada ya kutokea tukio la mtoto kuuawa wakati akichunga ng'ombe, Jeshi la Polisi mkoani Katavi limewataka wananchi kutojichukulia sheria mkononi.

Kauli hiyo imekuja baada ya wananchi kuchukua uamuzi wa kuwapiga watuhumiwa wawili wa tukio hilo na kusababisha kifo chao.

Akitoa taarifa ya matukio mbalimbali kwa waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, alisema kuwa baada ya tukio hilo wananchi walifanikiwa kuwakamata watuhumiwa wawili kati ya watatu waliohusika na tukio hilo.

Kamanda Makame aliwataja watuhumiwa waliokamatwa kuwa ni Amos Mashauri (22), mkazi wa Kijiji cha Kasekese, Malimi Selemani (24), mkazi wa Kijiji cha Kawanzige na mwingine ambaye hakupatikana aliyetambulika kwa jina la Moses.

Alisema baada ya watuhumiwa wawili hao kukamatwa, wananchi walijichukulia sheria mkononi na kuanza kuwashambulia.

Jeshi la Polisi baada ya kufika eneo la tukio, lilikuta tayari mtuhumiwa mmoja ambaye ni Malimi Selemani ameshafariki dunia na mtuhumiwa wa pili ambaye ni Amos Mashauri akiwa katika hali mbaya ambapo alikimbizwa hospitali lakini baadaye alifariki dunia akiwa anapatiwa matibabu.

Alisema Jeshi la Polisi linaendela kumtafuta mtuhumiwa wa tatu kwa kuwa baada ya tukio hilo alitoroka na kwenda kusikojulikana.

**DIWANI ASAKWA**

Mbali na hilo, jeshi hilo pia linaendelea kumsaka Diwani wa Itenka, Joseph Laurent kwa tuhuma za kujaribu kumuua mkewe, Restuta Januari kwa kumkata kwa kitu chenye ncha kali shingoni.

Alisema chanzo cha tukio hilo ni wivu wa mapenzi na mtuhumiwa baada ya kutenda kosa hilo alikimbia kusikojulikana, hivyo Jeshi la Polisi linamtaka kujisalimisha.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Suzanne Ndomba (wa pili kulia), alipowasili kwenye Waajiri Health Bonanza, lililoandaliwa na chama hicho viwanja vya Leaders Club Kinondoni, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Shirika la Kazi kwa Afrika Mashariki, Wellingtone Chibebe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Dk. Mwinyi atoa ufafanuzi zabuni iliyozua malalamiko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amelitolea ufafanuzi sakata la kampuni ya DNATA kupewa zabuni ya kufanya kazi katika Uwanja wa Ndege wa Abeid wa Kimataifa wa Amani Karume katika jengo la tatu la abiria.

Dk. Mwinyi alitoa ufafanuzi huo juzi Ikulu, Zanzibar katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya kuulizwa swali na mwandishi wa Nipashe kuhusu suala hilo lililozua malalamiko kutoka kwa baadhi ya wadau.

Alisema kuna propaganda zinazotolewa katika vyombo vya habari kuhusu kampuni hiyo ambayo imepewa kazi ya kushughulikia mizigo katika jengo hilo, akisisitiza kuwa taarifa hizo si za kweli. Rais Dk. Mwinyi alisema kampuni hiyo ina ujuzi na uzoefu mkubwa katika kutoa huduma na imeshatoa huduma katika viwanja vya ndege mbalimbali duniani ikiwamo Dubai na kwa Zanzibar, kampuni hiyo imeajiri wafanyakazi zaidi ya 600.

"Ndege zote ambapo zinataka kuendelea na kampuni ya kusafirisha mizigo ya Zati au Trasword waendelee katika jengo la pili la abiria. Hizi tuhuma za kupoteza ajira za wafanyakazi 600 ni propaganda tu na hakuna sababu ya kupoteza ajira," alisema.

Dk. Mwinyi alisema kinacholalamikiwa na baadhi ya wadau wa uwanja huo ni propaganda za watu wasiotaka ushindani na waliozoea kukaa katika viwanja vya ndege miaka yote bila ya kuwa na huduma bora.

Alisema lazima katika viwanja hivyo kuwe na kampuni zenye huduma bora ili kuendelea kupata wageni wengi katika viwanja hivyo na lazima huduma zake ziwe za kisasa.

Rais Dk. Mwinyi alisema Zanzibar ni nchi ya utalii na inategemea uchumi wake kutoka viwanja vya ndege na bandari, hivyo lazima taasisi hizo kuwa na kampuni kubwa ili kubadilisha utendaji.


"Leo bandarini, meli ya mzigo ikija inakaa mpaka wiki tatu kushusha mzigo wakati wenzetu meli mmoja inashusha kwa saa 12 halafu tukileta kampuni ya nje kuja kufanya kazi utasikia kelele tu," Dk. Mwinyi alitamka kwa ukali, akionesha kukasirishwa na propaganda hizo.

Alisema kuzipa kampuni kubwa kufanya kazi katika mamlaka hizo ni kwa nia njema ya kukuza uchumi na kuwa na utendaji bora.

Alisema jengo la tatu la abiria lazima liendane na hadhi ya kuwa na huduma bora badala ya kuendelea kuwa na huduma za kizamani.

Hivi karibuni Chama cha Waendeshaji Ndege Tanzania (TAOA) kilitoa siku saba kwa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) kusitisha uamuzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) kuiteua Kampuni ya DNATA toka Dubai kuwa mtoa huduma pekee katika jengo la tatu (Terminal III) la Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume.

**KABWELA** **Fadhili Mohamed**



# Waachiwa huru kesi ya SGR

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewaachia huru mfanyabiashara Kanji Mwinyijuma na aliyekuwa Mwanasheria wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Emanuel Massawe katika kesi ya jinai iliyokuwa inahusisha mradi wa reli ya kisasa (SGR) wenye thamani ya Sh. trilioni 15.

Uamuzi huo ulitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ngimilanga, baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuwasilisha ushahidi unaotengeneza kesi kuwataka kutoa utetezi dhidi ya mashtaka yaliyokuwa yakiwakabili.

Hakimu Ngimilanga alisema ni takwa la kisheria upande wa mashtaka kuthibitisha kesi yao, hivyo kwa kushindwa kufanya hivyo, anawaachia huru Kanji na Massawe kwa kuwa hawana kesi ya kujibu. Alisema kuwa baada ya kupitia ushahidi uliotolewa na mashahidi tisa ili kuthibitisha mashtaka, mahakama imeona kuwa upande wa mashtaka haujathibitisha kesi ya awali dhidi ya washtakiwa hao wawili.

Hata hivyo, upande wa mashtaka ulioongozwa na Wakili kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Magera Ndimbo na Wakili wa Serikali, Iman Nitume, ulifanikiwa kutengeneza kesi dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Rahco, Benhadard Tito ambayo ushahidi wake unamtaka ajitetee.

Hakimu huyo alisema kesi ya awali inathibitishwa kwa upande wa shtaka la pili hadi la saba linalomkabili Tito. Mshtakiwa wa kwanza ana kesi ya kujibu na anatakiwa kujitetea.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao walikuwa wanakabiliwa na mashtaka manane yakiwamo ya uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, kula njama na kuisababishia RAHCO hasara ya dola za Marekani 527,540.

Upande wa mashtaka ulidai kuwa Februari 27, 2015, katika ofisi za RAHCO Wilaya ya Ilala, wakati akitekeleza majukumu yake, akiwa Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Tito alitumia vibaya nafasi yake kwa makusudi kwa kununua kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Limited.

Ilidaiwa kuwa kampuni hiyo ilinunuliwa kama mshauri wa shughuli za mradi wa kuboresha ukanda wa reli ya kati nchini kwa njia moja bila kupata kibali cha awali cha Bodi ya Zabuni ya RAHCO, kitendo ambacho kilikuwa ni ukiukaji wa Sheria ya Ununuzi.

Kati ya Machi 12 na Mei 20, 2015, katika ofisi za Rahco, Tito na Massawe walidaiwa kutumia nafasi zao vibaya kwa kusaini barua ya kuteua kampuni hiyo ya Afrika Kusini na kushindwa kuwasilisha mkataba wa huduma za ushauri kati ya kampuni hiyo na RAHCO kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.

Washtakiwa hao wawili kati ya Mei 20 na Juni 20, 2015 wakiwa katika ofisi za Rahco, walidaiwa kutumia vibaya nafasi zao kwa kutia saini mkataba wa ushauri na kushindwa kuwasilisha nakala kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Mkaguzi Mkuu wa Ndani na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).




Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) Temeke, Rajabu Kivande, akiwasilisha mada kuhusu shughuli za mfuko kwa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Klabu ya Waandishi wa Habari wa jijini Dar es Salaam (DCPC) uliofanyika jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mamilioni yatengwa ujenzi wa madarasa

**Na Steven William,** MUHEZA

SERIKALI imetenga Sh. milioni 180 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa tisa katika baadhi ya shule za sekondari wilayani Muheza mkoani Tanga.

Fedha hizo zilizotolewa katika Wilaya ya Muheza zikiwa sehemu ya fungu lililotengwa na serikali kwa ajili ya kuhakikisha wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza mwakani wanapata mahali pa kusomea.

Ofisa Tarafa wa Tarafa ya Muheza mkoani Tanga, Japheti Hayule alisema juzi katika mkutano na wananchi kuwa serikali imeleta fedha Sh. milioni 180 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa tisa katika baadhi ya shule za sekondari.

Hayule alisema Tarafa ya Muheza imepata madarasa matano ambapo katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Magila yatajengwa mawili na ofisi moja, Shule ya Sekondari ya Kata ya Mtindiro imepata madarasa mawili na ofisi na Shule ya Kata ya Kwabada imepata darasa moja wanaendelea na msalagambo.

Wananchi wa Kata ya Magila kutoka katika vijiji vya Mikwamba, Magila, Kwedunda na Misongeni walijitokeza kwa wingi katika msalagambo Shule ya Sekondari Kata ya Magila.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Magila, Sheikhe Semtawa, alisema anaishukuru serikali kwa kuamua kujenga madarasa hayo mawili ya sekondari na ofisi moja.

Diwani wa Magila, David Kilua, alisema hivi sasa wananchi wameelekeza nguvu zao katika ujenzi wa madarasa hayo mawili na ofisi moja ili watoto waingie kwa wakati mwakani kuanza kidato cha kwanza.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Halima Bulembo, aliagiza ifikapo Desemba 30 mwaka huu, ujenzi wa madarasa ya sekondari uwe umekamilika ili mwakani wanafunzi wa kidato cha kwanza waingie darasani.

# Aliyegombea ubunge kupitia CHADEMA atimkia CCM

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

ALIYEKUWA mgombea ubunge wa Masasi Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mwaka 2020, Mustapha Swalehe amejiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa madai kuwa amefurahishwa na kasi ya maendeleo inayofanywa na serikali chini ya Rais Samia Suluhu.

Swalehe alitangaza uamuzi huo kwenye mkutano wa hadhara ulioandaliwa na Mbunge wa Jimbo hilo, Geofrey Mwambe kwa kushirikiana na Mwenyekiti CCM Wilaya ya Masasi, Mariam Kasembe na Katibu wa chama hicho, Didas Zimbihile.

Alisema alikuwa ndani ya CHADEMA kwa zaidi ya miaka 20 lakini kwa sasa anaridhishwa na kazi nzuri inayofanywa na serikali ya Samia.

"Leo nimeamua kujiunga na CCM na sasa mimi ni mwanachama mpya, kazi iliyofanywa na mbunge wetu kuleta maendeleo inastahili kuungwa mkono," alisema.

Kwa mujibu wa Swalehe, kuwa mpinzani siyo kupinga kila kitu bali pale unapoona maendeleo yanayofanywa kuna kila sababu ya kuunga mkono maendeleo hayo na siyo kuendeleo kupinga.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Masasi, Mariam Kasembe, alisema wanampokea mwanachama huyo na wanaamini kuwa watashirikiana pamoja katika mambo mbalimbali ya kimaendeleo.

HABARI KITAIFA

# Utafiti: Wastaafu huyatumia mafao kuingia ndoa za uzeeni

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

WATAFITI kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) Kampasi ya Dar es Salaam, wamebaini wastaafu wengi kutoka taasisi za serikali na zisizo za kiserikali wanatumia sehemu ya fedha za kiinua mgongo kujiingiza katika ndoa za uzeeni.

Hali hiyo imekifanya chuo hicho kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo maalumu watumishi wa serikali wanaokaribia kustaafu kuwapa mbinu za kufanya shughuli za uwekezaji na ujasiriamali kwenye biashara na kilimo.

Akizungumza katika mafunzo hayo, yaliyoshirikisha watumishi 26 wa serikali wanaokaribia kustaafu, mwezeshaji mkuu wa mafunzo hayo kutoka TPSC, Anselm Namala, alisema pamoja na kupewa mbinu za kufanya ujasiriamali, wanawaandaa kisaikolojia kuishi maisha ya kujipanga mshahara unapokoma.

Alisema katika utafiti waliofanya pia wamebaini wastaafu wengi hawajiandai mapema maisha ya kustaafu kwa kuwekeza katika shughuli mbalimbali za kujiingizia kipato na wanapopata fedha hizo hujikuta wakizifanyia starehe na baada ya kuisha baadhi yao wanapoteza maisha kutokana na kuugua magonjwa yasiyoambukizwa kama shinikizo za damu kutokana na ugumu wa maisha.

Alisema kuwa hali hiyo inatokana na kukata tamaa na maisha huku wakiwa na mtazamo hasi kuwa kustaafu ni kikomo cha maisha bila kujua kuwa bado maisha yanaweza kuendelea kwa kutumia ubunifu wa miradi mbalimbali.

Namala alisema ili kupata mafanikio kuna umuhimu kwa wajiri kuwapeleka katika kozi hizo wafanyakazi wao mapema badala ya kusubiri muda mchache kabla ya kustaafu.

Naye mtaalam wa uchumi, kilimo na biashara kutoka Taasisi ya Malembo Farm inayojishughulisha na ushauri na uwekezaji katika kilimo biashara, Lucas Elias, alisema wanawapa maarifa na taarifa wastaafu hao tarajiwa jinsi ya kutumia mafao yao kuwekeza katika kilimo, ufugaji na uvuvi ili kujipatia kipato.

Alisema lengo lao ni kuhakikisha wastaafu hao wanakuwa sehemu ya waajiri kwa kutumia mafao yao hatua ambayo itawezesha kuendesha maisha yao kwa kujingizia kipato baada ya ukomo wa ajira zao za serikali.

Mmoja wa wastaafu watarajiwa, Edna Shimbe, kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), alisema mafunzo hayo yamewapa uelewa mpana wa kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kwa kuanza kufanya uwekezaji na ujasiriamali mapema badala ya kusubiri fedha za kustaafu.



Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza (wa pili kushoto) na viongozi wengine wa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali, wakibadilishana mawazo baada ya mkutano wa kujadili mikakati ya kupambana na ukatili wa kijinsia katika jamii jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

## AGGCI yaishukuru serikali kuipa usajili

**Na Grace Gurisha**

ASKOFU Mkuu wa Assemblies of God Gospel Church International (AGGCI), Dk. Asumwisye Mwasabila, amesema hawezi kuihasi serikali kutokana na neema aliyoipata ya kupata katiba ya kanisa lake.

Dk. Mwasabila alisema hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu kutoka mkoani Mbeya, baada ya serikali kukubali kulisajili kanisa hilo bila usumbufu.

Alisema anaishukuru serikali kwa kuendelea kuisimamia amani ya nchi na kutoa uhuru wa kuabudu kwa Watanzania bila ubaguzi wa aina yoyote tofauti na baadhi ya nchi kuabudu kwao ni shida.

"Namshukuru sana rais hakunibagua kwa chochote wakati wa matatizo yangu na kanisa, mimi nasema sitaihasi serikali yangu kwa neema hii niliyoipata," alisema Askofu Dk. Mwaisabila.

Alisema kanisa limefikia hatua ya kupata katiba hiyo kwa sababu serikali imemuheshimu na anakwenda kuwatangazia wakristo, wachungaji, wainjilisti na watu wote kwamba wamepata katiba ya kanisa hilo.

"Nawaomba wachungaji mliopewa kibali hiki na katiba hii, asiwapo mtu mwingine akainuka tofauti na wenzake na wasihi fanyeni kazi ya Mungu kama serikali ilivyotuheshimu. Nataka kuliona kanisa limesimama vizuri," alisema.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa AGGCI, Askofu Dk. Robert Ngai, alitoa wito kwa wachungaji wa kanisa hilo kuwa kwa sasa wanaendelea na maandalizi ya mkutano mkuu utakaofanyika Kahama mkoani Shinyanga Novemba 9 na 10, 2022.

Naye Mweka Hazina Mkuu wa kanisa hilo, Askofu Jacobo Chacha, alisema mkutano huo utatoa taswira halisi ya watakavyoendesha kanisa lao na mipaka waliyopewa na serikali.

# Mwendokasi ulivyoua wawili, kujeruhi watatu

**Na Samson Chacha,** TARIME

WATU wawili wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria kutoka Tarime mjini kwenda Sirari kupinduka.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Tarime-Rorya, ACP Gofrey Sarakikya, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, ambayo alisema watu hao walikuwa wanatoka kwenye starehe.

Alisema ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia Ijumaa eneo la Sirari na watu wawili, Rusui Keryoba, mkazi wa Isebania aliyekuwa dereva wa gari lenye namba za usajili KDB 958 B, aina ya Pick-Up Toyota Hilux na mwenzake Ezekel Jomo, walifariki na wengine watatu kujeruhiwa.

Kamanda Sarakikya alisema, "ajali hiyo ilisababishwa na mwendo kasi na gari hilo kukosa mwelekeo na kuingia pembezoni mwa barabara na kupinduka.

Alisema polisi walifika eneo la tukio kuwachukua majeruhi watatu na kuwakimbiza hospitali kwa matibabu.

Aliwaasa madereva wanapokuwa barabarani kuzingatia sheria za usalama barabarani na kutotumia kilevi cha aina yoyote wakati wa kuendesha chombo vya moto.

Wakazi wa miji ya Isebania na Sirari mpakani waliojitambulisha Samwel Wambura, Peter Marwa na Bhoke Nyamhanga ambao ni ndugu za majeruhi, waliwataja vijana wengine waliojeruhiwa katika ajali hiyo kuwa ni Nestori Kasuku mkazi wa Sirari, Emanuel Ngera na mwendesha bodaboda aliyetajwa kwa jina la Ibrahim, mkazi wa Sirari.

# Wanafunzi waandaliwa kuijenga Tz bila magonjwa yasiyoambukiza

**Na Mwandishi Wetu,**
MWANZA

WIKI ya Magonjwa Yasioambukiza (NCD) imeanza jijini hapa kwa wanafunzi 100 kutoka shule tano za sekondari wilayani Nyamagana kupatiwa elimu ya magonjwa hayo.

Lengo la mafunzo hayo ni hatua za kuanza kujenga kizazi kijacho kisicho na NCD na chenye uelewa wa magonjwa hayo ili kuwa na uwezo wa kuchukua hatua muafaka za kuyadhibiti.

"Mafunzo haya ni katika kutekeleza kaulimbiu ya mwaka huu ambayo ni 'Badili mtindo wa maisha, boresha afya.' Tunaamini tunaweza kubadili mtindo wa maisha kwa kuongeza nguvu kupitia wanafunzi," alisema Meneja Mipango wa Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), Happy Nchimbi.

Alisema wanafunzi 20 na walimu wawili kutoka shule tano za sekondari Wilaya ya Nyamagana walialikwa kwenye mafunzo hayo ili waandaliwe kwa elimu itakayowawezesha pia kwenda kuwafundisha wenzao wanakotoka.

Kaimu Ofisa Elimu ya Sekondari Jiji la Mwanza, Nyandaro Musagara, alizitaja shule zilizoshiriki kuwa ni Nsumba, Mwanza, Buhangwa, Musabe na Pamba.

Mmoja wa wakufunzi, Mwenyekiti wa TANCDA, Profesa Andrew Swai, aliyataja miongoni mwa magonjwa yasiyoambukiza kuwa ni ya moyo na mishipa ya damu, saratani, kisukari, kuoza meno, matatizo ya akili na selimundu.

Aliwaambia wanafunzi hao kuwa takwimu za magonjwa hayo zinaonesha kila mwaka idadi ya wanaougua inaongezeka kwa kasi jambo ambalo tayari taifa limeyatangaza kuwa ni janga.

Profesa Swai alitaja sababu kuu za mtu kupata NCD kuwa ni ulaji usiofaa, unywaji wa pombe kupita kiasi, matumizi ya tumbaku, dawa za kulevya, utawala duni wa msongo wa mawazo, kutopata usingizi wa kutosha na tabia bwete ya kutoshughulisha mwili.

Kuhusu ulaji usiofaa, Profesa Swai alisema; "ni kutokula kutoka kwenye makundi matano ya vyakula, kula chakula kupita mahitaji ya mwili, kutumia kwa wingi sukari, mafuta na chumvi, ulaji wa nafaka zilizokobolewa na kunywa juisi badala ya matunda yenyewe.

Aliwataka wanafunzi hao kuwaelimisha wenzao na pia kuanza kuwa waangalifu ili kujiepusha kupata magonjwa hayo.

Mtaalamu wa mazoezi, Waziri Ndonde, aliwawaasa wanafunzi kuepuka tabia bwete ya kutoshughulisha mwili.

Aliwachunguza aina ya mazoezi wanayofanya na kuwaelimisha kanuni sahihi zitakazowezesha kujenga afya zao.

Wiki ya NCD itahitimishwa kwa kongamano la kisayansi la siku mbili litakaloanza Alhamisi na utafiti wa magonjwa hayo kutolewa.

Hivi karibuni, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alinukuliwa akisema magonjwa yasiyoambukiza yana uelemea Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na kutishia kuufilisi.

Alisema hali hiyo inasababishwa na ongezeko la wagonjwa wa NCD pamoja na gharama kubwa za vipimo, huduma na dawa.

Miongoni mwa huduma ghali ni pamoja na upasuaji wa moyo, kuzibua mishipa, kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo na tiba za saratani.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kulia), akitoa maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Justice Kijazi, alipotembelea jana ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari za Ikungi na Unyahati. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# RC aagiza ujenzi madarasa uanze kwa kumwagwa zege

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MANYONI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amepiga marufuku wahandisi katika halmashauri Mkoa wa Singida kuacha kujenga vyumba vya madarasa kwa kupandisha ukuta kabla ya kumwaga zege (jamvi), ambako kunasababisha majengo kupata nyufa na kuhatarisha maisha ya wanafunzi.

Alisema hayo baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari za Manyoni na Mwese, wilayani Manyoni na kukuta ukuta wa madarasa umepandishwa bila kumwagwa jamvi.

"Mhandisi sitaki ujenzi wa aina hii nataka mnamaliza chini kwa kumwaga jamvi ndipo mnapandisha ukuta, nimepita Manispaa ya Singida na Halmashauri ya Wilaya Ikungi wanajenga kwa kuanza kumwaga zege ndipo wanapandisha ukuta wewe mhandisi ujenzi huu umeutoa wapi," alihoji.

Serukamba alisema inasikitisha kuona Wilaya ya Manyoni imepewa fedha nyingi kuliko wilaya nyingine za mkoa huo kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, lakini ndio wilaya ambayo ujenzi wa madarasa hauendi vizuri.

"Naombeni tuwe na uzalendo serikali hii imetuheshimu sana kutuletea fedha zote hizi sasa tafadhari mhandisi usikae ofisini hakikisha unatembelea kuona maendeleo ya kazi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kila siku," alisema.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ni jukumu la viongozi kuanzia Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi na Mhandisi kuhakikisha wanasimamia ujenzi ukamilike mapema na kwa ubora unaokubalika.

Serukamba alisema Wilaya ya Ikungi ni mfano mzuri wa kuigwa kwa kuwa licha ya kupewa fedha za ujenzi wa madarasa, kujenga na ofisi za walimu katika fedha hizo hizo.

Aidha, Mkuu wa Mkoa alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Rahabu Mwagisa, kumpa taarifa za maendeleo ya ujenzi kila baada ya wiki mbili.

Naye Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya Manyoni, Ahmed Seleman, alisema upatikanaji wa mawe umekuwa tatizo na mafundi wanalazimika kuanza ujenzi kwa kupandisha ukuta kabla ya kutandika zege.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Fadhili Chimsala, alisema halmashauri hiyo imepewa Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 85 vya madarasa.

# Diwani akerwa wanafunzi kuchezeshwa miondoko isiyo maadili katika mahafali

**Na Julieth Mkireri,**
RUVU

DIWANI wa Vigwaza Halmashauri ya Chalinze, Mussa Gama, amewashauri wazazi kukemea vitendo vya watoto kucheza hadharani kwa miondoko isiyo na maadili.

Gama alitoa rai hiyo juzi aliposhiriki katika mahafali ya darasa la saba Shule ya Msingi Ruvu na kushuhudia burudani zilizokuwa zinatolewa na wanafunzi kuonesha kucheza tofauti na maadili.

"Tumeona watoto wetu wamecheza na sisi wazazi tunashangilia na kuwatunza hii sio tabia nzuri kwa watoto wadogo kama hawa kukata nyonga namna hii nawaomba tuwasimamie kwenye maadili mema tusiunge mkono haya yanayofanyika."

"Tukiwashangilia sana tutambue baadaye wataharibikiwa tuwasimamie katika maadili yanayotakiwa na kwenye masomo wapende elimu ili watumie vyumba vya madarasa vinavyojengwa, tusipokuwa makini hawatasoma watajikita kwenye miziki," alisema Gama.

Aliwataka wazazi kutoacha jukumu la elimu kwa walimu pekee badala yake waungane nao ili kukuza ufaulu na kuwa na wanafunzi na kuwalea kwenye maadili mazuri.

Mwenyekiti wa kamati ya wazazi, Salum Makatuka, aliwataka wazazi kwenda kuwasimamia watoto wao ikiwa ni pamoja na kuwaandaa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2023.

Katika risala yao wanafunzi waliohitimu darasa la saba waliomba kupatiwa mashine ya kudurufu (photocopy) kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi wa walimu kuandaa mitihani ya kujipima shuleni hapo.



# Madiwani waikumbusha h'shauri kukarabati shule chakavu

**Na Allan Isack,** ARUMERU

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Arusha, limeikumbusha serikali kutupia macho shule kongwe za msingi ambazo zinatishiwa na uchakavu wa miundombinu na kuhatarisha usalama wa wanafunzi na walimu.

Shule nyingi za msingi za Wilaya ya Arumeru, zimechoka na zinahatarisha usalama kutokana na kujengwa kabla ya uhuru.

Kabla ya kupitishwa azimio la kuikumbusha serikali wajibu huo, hoja hiyo iliibuliwa na Diwani wa Bangata, Ezra Tomito, kwa baadhi ya vyumba vya madarasa vimebomoka, sakafu imegeuka kuwa udongo, milango imeisha kwa kulikuwa na mchwa, madirisha na mapaa.

Tomito alikuwa akizungumzia hali hiyo mwishoni mwa wiki, katika kikao cha kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za maendeleo za kata zao, kwa robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023.

Diwani Eliakimu Marivey alisema, "Baadhi ya shule zetu za msingi zina ubovu wa miundombinu ambayo inahitaji ukarabati wa haraka kwa mfano, Shule ya Msingi Seliani yenye miaka zaidi ya 100 ni moja ya shule inayohitaji ukarabati wa miundombinu yake karibu yote."

Diwani wa Sokon II, Obed Mollel, aliiomba serikali kuanza kutenga fungu la fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu hiyo kama inavyofanyika kwa shule za sekondari, ili wanafunzi waweze kusoma kwenye mazingira salama.

Akitoa majibu, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema serikali imejipanga vyema kwa ajili ya kutatua matatizo ya uchakavu wa miundombinu hiyo kwa kuwa hivi karibuni wataanza kufanya ukarabati, pamoja na ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa kwa shule zenye uhitaji ili wanafunzi wanaosoma katika shule hizo wasome kwa amani.

"Serikali inafahamu tatizo lililoko katika miundombinu ya shule za msingi hasa zile kongwe, kuna Mradi wa BOOST unaendelea kufanya tathmini ya uchakavu wa miundombinu kwa shule hizo, baada ya kukamilika kwake, kazi itaanza mara moja shule zenye uchakavu na uhaba wa vyumba vya madarasa," alisema.

Vilevile, mkurugenzi huyo, alisema kwa mwaka huu wa fedha, serikali imejipanga kutekeleza miradi mbalimbali kisekta ikiwamo ya afya katika Hospitali ya Wilaya ya Oltrumet, kwa kujenga uzio na mahitaji mengine ya maabara, jengo la mionzi na la kuhifadhia maiti.



Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara, Mbaraka Batenga (wa nne kushoto) akiwa na viongozi wengine pamoja wanafunzi wa shule za msingi waliokaa kwenye madawati katika uzinduzi wa uchangiaji madawati ili kumaliza upungufu wa madawati 9,000 juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Kijazi aagiza taasisi za umma zinazodaiwa kodi kulipa

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, ameagiza vituo vyote vya makusanyo ya kodi na masurufu ya serikali, kuzibana taasisi za umma zinazodaiwa kodi, kwa kuwa tozo hizo ni za kisheria na sio hiari.

Dk. Kijazi aliyasema hayo jana jijini hapo, wakati akifungua kikao kazi cha kujadili utekelezaji wa mkakati wa makusanyo ya kodi ya pango la ardhi unaotekelezwa na serikali na Benki ya CRDB.

Alisema kuwa ni muhimu kwa wamiliki wa ardhi kulipa kodi hizo kwa wakati ili kuruhusu utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya serikali iweze kufikiwa.

Aliongeza kuwa kwa sasa vituo vya makusanyo ya kodi vinatakiwa kuhakikisha kuwa hakuna mtu yeyote yule ambaye anaachwa hasa kwenye ukusanywaji wa kodi na ikitokea hawajalipa ni muhimu hatua kali na za kisheria zichukuliwe.

"Kodi ni suala la kisheria na sio hiari taasisi yoyote ambayo haijalipa kodi chukueni hatua kwa kuwa kutolipa kodi ya pango ni sawa na ukiukwaji wa sheria," alisema.

Kamishna wa Ardhi nchini, Mathew Nhongwe, alisema Wizara ya Ardhi, kwa mwaka huu wa fedha 2022/23, imejipanga kukusanya Sh. bilioni 250, tofauti na mwaka jana Sh. bilioni 130.

# Kata Mtindiro yakombolewa kuchimbiwa visima

**Na Steven William,** MUHEZA

VISIMA virefu 10 vimechimbwa na wafadhili mbalimbali ikiwamo Taasisi ya Islamic Help ili kutoa usaidizi kwa wanawake na watoto wa Kata ya Mtindiro, wilayani hapo kupata huduma ya majisafi na salama.

Diwani wa Kata ya Mtindiro, Mustafa Hatibu, alisema miradi hiyo ni mkombozi kwa jamii na hususani wanawake wanaokabiliwa kutembea umbali mrefu kutafuta maji.

Alisema kutokana na tatizo la maji, Kijiji cha Kibaoni na vijiji vingine vya kata hiyo, miradi hiyo imeleta nuru na kuwapunguzia gharama kwa kuwa wanachota bure na diwani analipia bili za umeme na matengenezo ya pampu za maji.

Diwani huyo alisema amepeleka maji katika shule ya sekondari ya kata na sasa anajiandaa kuchimba kisima kingine kirefu kwa ajili ya shule ya msingi Kijiji cha Kibaoni.

Pia familia ya Khamisi Selemani Mkelo, imejenga msikiti wa Masjid Khamisi kwa gharama ya Sh. milioni 50 unaochukua waumini 300 huku gharama za umeme akizilipia diwani huyo.

Wakishukuru kupata huduma ya majisafi na salama wakazi, Nuru Selemani na Maulid Hatibu, kwa nyakati tofauti walisema hapo mwanzo wanawake walikuwa wanalala visimani kusaka maji katika majabali na wengine kusababisha ndoa zao kuvunjika.

Asha Hassani, mwanafunzi wa darasa la nne Shule ya Msingi Kibaoni, alisema wanamshukuru diwani wao kwa kuleta wafadhili wa kuchimba visima na kuwaondolea adha ya kutafuta huduma hiyo.

Mbunge wa Jimbo la Muheza (CCM), Hamisi Mwinjuma, alisema ametatua changamoto ya miaka mingi ya kukosa majisafi na salama kwa wananchi wa jimbo hilo na sasa wakazi wake wananufaika na huduma hiyo baada ya visima 100 kuchimbwa vijiji mbalimbali na mfadhili wake wa kampuni ya Moo Maji.

# SACCOS KKKT yafunguliwa njia uwekezaji sukari

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SERIKALI imekifungulia njia ya kuwekeza katika sekta ya uzalishaji wa sukari nchini, Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha ELCT ND Saccos kinachomilikiwa na Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), chenye mtaji wa wanahisa 12,879.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema uamuzi wa wizara hiyo kukifuata na kukialika rasmi kuingia katika uwekezaji wa sukari, unatokana na azma yake ya kutaka kuachana na uagizaji wa sukari nje, ifikapo mwaka 2025.

Mvunde, alikuwa akizungumza na menejimenti ya chama hicho, viongozi wa serikali na wanahisa, wakati wa Mkutano Mkuu wa 27 wa ELCT ND Saccos uliofanyika Moshi Mjini.

"Pamoja na mambo mengine, nimekuja kuzindua mradi wa kwanza wa kimkakati nchini, unaohusisha ubunifu wa kisayansi wa matumizi ya mashine ya kutolea fedha (ATM) pamoja na mfumo maalum wa simu wa Saccos kiganjani (Mobile Saccos), unaolenga kupunguza kero za wanachama wa vyama vya ushirika.

"Lakini nimeshamshawishi Mwenyekiti wenu (Mchungaji Macha) tupeleke nguvu sasa ya kuwekeza kwenye sukari. Tumesema kama serikali, kwamba kwenye sukari ikifika mwaka 2025, nchi hii itaacha kuagiza nje ya nchi. Hivi sasa upungufu wa sukari tulionalo ni tani 50,000. Tumetoka kwenye upungufu wa tani 300,000 hadi 50,000. "Ukienda Kilombero, kuna upanuzi pale unafanyika, wanapanua kiwanda chao kutoka uzalishaji wa tani 126,000 na wakikamilisha mradi wao watakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 271,000 ifikapo mwaka 2025." Aidha, alisema Kiwanda cha Sukari cha Kagera, hivi sasa kinazalisha tani 95,000 na ifikapo mwaka 2024, kinatarajia kuzalisha tani 170,000, wakati Kiwanda cha Bakharesa kilichoko Pwani kitaanza kuzalisha tani 50,000.

"Tuna kiwanda kinamilikiwa na NSSF (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) kiko Morogoro watakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000. Kuna kiwanda kiko Rufiji, watakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 50,000, kuna Kampuni ya RYHNO itakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 100,000. Nchi yetu itaandika historia itaacha kuagiza sukari nje." "Tunataka vyama vya ushirika vya akiba na kukopa, hasa ELCT ND Saccos, kuendelea kubuni miradi ya kusaidia kuongeza kipato katika chama ili mwisho wa siku tuweze kupunguza makali ya umaskini wa kipato.

"Ningependa kuiona Saccos hii ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Dayosisi ya Kaskazini, ikisaidia kukuza sekta ya kilimo, hasa kwenye kufikia malengo tuliyojiwekea ya kuikuza sekta ya kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mavunde, Wizara ya Kilimo, inataka kulisaidia taifa kuchana na mzigo wa kuagiza sukari, mafuta ya kula na ngano.

Awali, Mwenyekiti wa ELCT ND Saccos, Mchungaji Michael Macha, alimweleza Mavunde kwamba takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya wanachama imeongezeka kutoka 10,898 kufikia Septemba mwaka 2021 hadi kufikia 12,879, Septemba mwaka huu.



Wakazi wa Songe, wilayani Kilindi, Mkoa wa Tanga, wakifurahia kukamilika kwa daraja linalounganisha mji huo na huduma za afya ambapo nyakati za mvua mto hujaa maji na kukatisha huduma mbalimbali. (Wa nne kulia) ni Diwani wa Kata ya Songe, Mohamed Makengwa na Diwani Viti Maalumu, Hamida Kidunda (kulia). **PICHA: DEGE MASOLI**

# Mil. 700/- kupunguza upungufu madawati

**Na Cynthia Mwilolezi,** KITETO

ZAIDI ya Sh. milioni 700 zinahitajika kumaliza upungufu wa madawati zaidi ya 9,000 kwa shule za msingi wilayani Kiteto mkoani Manyara ili kuwanusuru wanafunzi wasio na madawati kwa sasa.

Akizungumza mwishoni mwa wiki, wakati wa uzinduzi wa mpango mkakati wa uchangiaji wa madawati wa Wilaya ya Kiteto, Mwenyekiti wa Kamati, Papakinyi Kaai, alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi kukosa madawati.

Kaai, alisema ongezeko hilo limetokea wilayani huko, kutoka wanafunzi 40,000 mwaka 2016 hadi zaidi ya 60,000 mwaka 2022. Alisema uzinduzi wa mpango mkakati wa uchangiaji wa madawati wilayani humo, umelenga kuwaweka katika madawati watoto zaidi ya 27,000 ambao kwa sasa wanakaa chini. "Tunawashukuru wadau mbalimbali wa elimu wa wilaya ya Kiteto kwani wameunga mkono shughuli hii ya uchangiaji wa madawati ili kukuza elimu," alisema Kaai.

Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Batenga, alisema serikali imesikia kilio cha wanafunzi na watoto wa Kiteto na kwamba hakuna atakayekaa chini darasani. Aidha, Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, John Nchimbi, alisema bei ya dawati moja ni Sh. 80,000, mahitaji ya kwenye Shule za Msingi Kiteto ni 21,069 yaliyoko ni 12,046.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Kiteto, Denis Mwita, aliitaka jamii na viongozi wajitoe kwa hali na mali ili kuondoa upungufu huo ili wanafunzi wasome kwa kujinafasi.

# CUF yamsihi Rais Samia matakwa ya demokrasia

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, amemsihi Rais Samia Suluhu Hassan, kutekeleza kwa vitendo matakwa ya demokrasia, kama ana nia thabiti ya kuyaishi maridhiano aliyoyafanya na vyama vya upinzani nchini ili kujenga nchi yenye demokrasia.

Prof. Lipumba alieleza hayo jana, alipokuwa jijini Tanga kukagua maandalizi ya uchaguzi ndani ya chama hicho yanayoendelea.

"Rais Samia, wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Vyama vya Siasa nchini, Desemba 2021 jijini Dodoma, alitamka hakuna mtu mwenye hatimiliki ya Tanzania, wala chama, huku akiomba kuwapo na maridhiano ya kufanya siasa za kistaarabu.

"Katika mkutano huo, wajumbe walijadili hali ya demokrasia na kufikia maadhimio kwamba mchakato wa katiba mpya unaotokana na maoni ya wananchi, ukamilishwe na Tume Huru ya Uchaguzi iundwe ambayo itasimamia chaguzi zote za Rais, Wabunge, Madiwani na Serikali za Mitaa."

Aidha, suala la utaratibu wa kupata tume huru namna ya kuipata na namna itakavyofanya kazi tayari ilishaandikwa vizuri kwenye rasimu ya Katiba ya Tume ya Jaji Warioba na sura inayoelekeza.

Alisema watendaji wa kata na wa vijiji wasiwe wasimamizi wa uchaguzii bali tume iteue wasimamizi wengine ili watu waweze kusimamia na watu waombe kama ilivyokuwa ajira na Rais apewa orodha ya watu wenye sifa.

Katika hatua nyingine, Prof. Lipumba, alisema uchaguzi 2020 ulikuwa mbovu kuwahi kutokea nchini na kuandika historia ya ubakwaji wa demokrasia.

Alisema wakati wanaelekea kwenye uchaguzi huo hali ya kisiasa ilikuwa ngumu kutokana na vyama kutokutakiwa kufanya mikutano ya hadhara licha ya katiba kutoa ruhusa kwamba vyama kufanya hivyo kwa wanachama na wananchi wake.

Alisema yeye alikuwa mgombea wa urais alifanya kampeni nchi nzima alikwenda Kisesa jimbo la uchaguzi Wilaya ya Maetu na kufanya kampeni, lakini wakati anakwenda kusikiliza matokeo akasikia amepata kura sifuri, jambo lililomshangaza kuwa hata mwenyekiti wake wa Jimbo la Meatu hakumpigia kura.

Alisema anashangaa wananchi wa jimbo zima la Meatu wapo tayari kuingia gharama ya kumchinjia mbuzi, lakini kumpigia kura hawataki.

Lipumba, alisema tangu walipomaliza uchaguzi 2015 mwaka uliofuata 2016 mikutano ya hadhara ilipigwa marufuku na kuwaruhsu wabunge na madiwani akiwamo Rais, lakini vyama kuzuiwa kufanya mikutano ya siasa licha ya katiba na sheria ya vyama vya siasa kuruhsu.

Alisema wameingia kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa wagombea wote wa vyama vya upinzani walizuiwa hata waliokuwa wenyeviti waliokuwa wanatetea nafasi zao wakiwaambia hawajui kusoma na kuandika.

Nipashe
# Spotika



WAAMUZI 10 BORA WA WAKATI WOTE DUNIANI UK.16



## ISIKUPITE

KIKOSI cha Pep Guardiola, Manchester City msimu huu ndani ya Ligi Kuu England: Mechi nyingi bila kuruhusu bao 'clean sheets' - Ederson (5), kinara wa ufungaji - Erling Halaand (18), pasi nyingi za mwisho 'assists' -Kevin De Bruyne (9), timu yenye mabao mengi - Manchester City (39).

## NDIO ZANGU HIZI...

Beki wa Simba, Shomari Kapombe, akicheza mpira kwa kichwa wakati wa mazoezi ya timu hiyo kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Singida Big Stars itakayochezwa keshokutwa Jumatano kwenye Uwanja wa Liti mkoani Singida. Kushoto ni Jonas Mkude, mazoezi hayo yalifanyika juzi katika Uwanja wa Mo Simba Arena ulioko Bunju, Dar es Salaam. **NA MPIGAPICHA WETU**




# REKODI 3 ZA RONALDO ZILIZOVUNJWA NA MESSI HADI SASA MSIMU HUU

**PARIS,** Ufaransa

CRISTIANO Ronaldo na Lionel Messi ndio wachezaji wawili wenye mafanikio zaidi katika soka kwa sasa. Wachezaji wote wawili kwa ujumla wameshinda Ballon d'Or 12 kwa pamoja na wametawala mchezo kwa zaidi ya muongo mmoja.

**Hoja ya nani bora kati ya wachezaji hawa wawili itadumu miongoni mwa mashabiki kwa miaka mingi ijayo. Kutokana na idadi ya mabao yaliyofungwa, mataji na rekodi zao binafsi, Ronaldo na Messi wanapambana kila mara.**

Ronaldo hajawa katika kiwango cha juu msimu huu. Nyota huyo wa Manchester United ameanza taratibu akiwa na mabao matatu pekee na asisti moja katika mechi 14 alizocheza.

Kwa upande mwingine, Messi anaonekana hatimaye amerudi kwenye ubora wake katika maisha ya Ufaransa na Paris Saint-Germain. Nyota huyo wa zamani wa Barcelona amekuwa kwenye kiwango bora msimu huu, akifunga mabao 11 na asisti 12 katika mashindano yote hadi sasa.

Kukosekana kwa Ronaldo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kuanza kwake polepole msimu huu, kumemwezesha Messi kuzifikia baadhi ya rekodi za nyota huyo wa Ureno na pia kuzipita nyingine.

Bila kuchelewa, makala haya yanaangalia rekodi tatu za Ronaldo ambazo zimevunjwa na Messi hadi sasa msimu huu...

**#1. AMEZIFUNGA TIMU NYINGI ZAIDI KWENYE LIGI YA MABINGWA ULAYA (40)**

Lionel Messi kwa sasa anashikilia rekodi ya kufunga dhidi ya timu nyingi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, amefunga dhidi ya timu 40 kati ya 44 alizokutana nazo kwenye michuano hiyo barani Ulaya tangu alipoanza kucheza kwa mara ya kwanza mwaka 2004.

Mwanzoni mwa msimu wa sasa, Messi na Ronaldo walikuwa wamefungana kwa idadi ya timu walizofunga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya (38). Hata hivyo, fowadi huyo wa PSG alimpita mpinzani wake alipofunga katika ushindi wa 3-1 wa klabu yake dhidi ya Maccabi Haifa, Septemba 14, mwaka huu.

Kisha akaendeleza rekodi hii alipofunga bao pekee la PSG katika sare ya 1-1 na Benfica.

**#2. MABAO MENGI YASIYO YA PENALTI (681)**

Ronaldo na Messi ni wachezaji wawili waliofunga mabao mengi zaidi katika historia ya soka. Gwiji huyo wa Manchester United ndiye mfungaji bora wa muda wote katika soka la wanaume akiwa na jumla ya mabao 818, huku nyota huyo wa PSG akiwa na mabao 785 katika maisha yake ya soka.

Hata hivyo, ni nahodha huyo wa zamani wa Barcelona ambaye amefunga mabao mengi zaidi yasiyo ya penalti. Wachezaji hao wote walikuwa wamefungana kwa idadi ya mabao yasiyo ya penalti (671) mwanzoni mwa msimu wa 2022-23, lakini Muargentina huyo alimpita Ronaldo alipofunga bao la ushindi la PSG dhidi ya Olympique Lyon, Septemba 18, mwaka huu.

Kwa bao lake dhidi ya Lyon, Messi aliwapita Pele na Cristiano Ronaldo kwa mabao mengi yasiyo ya penalti katika historia ya soka.

Kwa sasa ana mabao 681 yasiyo ya penalti, nane zaidi ya Ronaldo, ambaye ana 673.

Wachezaji wote wawili wamekuwa na uwezo mkubwa wa kupiga penalti, jambo ambalo limeongeza idadi yao ya mabao. Mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid kwa sasa ana mabao 145 ya penalti huku Muargentina huyo akiwa na mabao 104 aliyofunga kutokana na penalti.

**#3. MABAO MENGI NJE YA ENEO LA HATARI UEFA (23)**

Kukosekana kwa Ronaldo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kumetoa mwanya kwa Messi kuziba pengo hilo na kumpita kwenye baadhi ya rekodi za mashindano hayo.

Mshindi huyo mara saba wa Ballon d'Or, hivi majuzi alimpita mpinzani wake kwa mabao ya nje ya eneo la hatari kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya (23). Yuko mbele ya Ronaldo kwa bao moja, ambaye ametikisa nyavu mara 22 kutoka nje ya eneo la hatari.

Tangu mechi yake ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2004-05, Messi amefunga mabao mengi kutoka nje ya eneo la hatari kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye mashindano hayo (23, moja zaidi ya Cristiano Ronaldo).

Alipata mafanikio hayo alipofunga bao la nne la PSG katika ushindi wa 7-2 dhidi ya Maccabi Haifa.

## MICHEZO



# SIMBA QUEENS KATIKA HISTORIA NYINGINE CAF

**Na Somoe Ng'itu,** MARRAKECH

HISTORIA nyingine katika soka la wanawake imeandikwa juzi na Simba Queens kutoka Dar es Salaam, Tanzania kwa kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayoendelea nchini Morocco.

**Hii inakuja baada ya mapema mwaka huu Timu ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), kufanikiwa kukata tiketi ya kucheza robo fainali ya Kombe la Dunia mwezi uliopita huko nchini India.**

Katika fainali hizi za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Simba Queens inapeperusha bendera ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), baada ya kutwaa taji hilo katika michuano ya ukanda huo iliyofanyika Dar es Salaam, Agosti mwaka huu.

Simba Queens ilianza fainali hizo kwa kuchapwa bao 1-0 na wenyeji ASFAR FC ya Morocco lakini ikaamka katika mechi ya pili kwa kuifunga Determine Girls kutoka Liberia mabao 2-0 na juzi usiku ilikuwa na kibarua kizito cha kuikabili Green Buffalo kutoka Zambia ambayo yenyewe ilihitaji matokeo ya sare ya aina yoyote ili isonge mbele katika michuano hiyo lakini ikajikuta nayo ikichapwa 2-0.

Mechi za hatua ya nusu fainali sasa zitachezwa keshokutwa, Jumatano na Simba Queens itakutana na timu iliyoshika nafasi ya kwanza katika Kundi B ambao ni Mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Mamelodi Sundowns Queens kutoka Afrika Kusini huku ASFAR FC ikikutana na mshindi wa pili wa kundi hilo.

Katika fainali za kwanza za michuano hii zilizofanyika mwaka jana huko Misri, CECAFA iliwakilishwa na Mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Kenya, Vihiga Queens ambao walishia hatua ya makundi.

**KOCHA ABADILI KIKOSI**

Katika kuhakikisha timu yake inafanya vizuri na hatimaye inasonga mbele, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, aliamua kupangua kikosi chake wakati anaivaa Green Buffalo ambayo ni mabingwa wa Ukanda wa COSAFA.

Lukula aliamua kuwaweka benchi Vivian Corazone Odhiambo, kiungo Mkenya ambaye hakuonekana kuwa na mchezo mzuri katika mechi mbili zilizotangulia dhidi ya ASFAR FC na Determine Girls, lakini nyota huyo aliingia kuwakabili Wazambia akitokea benchi na kufufua makali kwenye kikosi hicho cha Malkia wa Wekundu wa Msimbazi.

Kocha huyo pia aliamua kumweka nje mshambuliaji raia wa Burundi, Asha Djafari, kama mwenzake, alipoingia alicheza mpira wa kasi, akipoteza nafasi ya kufunga ya kwanza aliyoipata, akajiuliza na kuendelea kulisakama lango la wapinzani na kufanikiwa kufunga bao la kwanza na kuwainua mashabiki wa timu yake waliokuwa wakiwafuatilia wawakilishi hao.

Mshambuliaji mwenye nguvu na mwili mkubwa kutoka Ghana, Philomena Abaka alianza kwa mara ya kwanza juzi, lakini alishindwa kuonyesha makeke yake baada ya kuumia na hivyo nafasi yake kuchukuliwa na Asha.

Haikuwa siku nzuri sana kwa winga, Pambani Kuzoya ambaye alishindwa kuonyesha cheche kama alivyofanya katika michezo miwili iliyopita sawa na Olaiya Barakat ambaye alianzishwa kwa mara ya kwanza, aliisaidia timu lakini si kwa kiwango alichocheza wakati Simba Queens inawafunga Determine Girls.

Nahodha, Oppa Clement na mabeki, Fatma Issa 'Fetty Densa', Daniella Ngoyi pamoja na golikipa chaguo la kwanza la timu hiyo, Gelwa Yonna, waliendelea kuzitendea vema nafasi zao na wametoa mchango mkubwa kuifikisha timu katika hatua ya nusu fainali.

Kiungo Joelle Bukuru, si tu amejua kuiongoza vema timu yake, lakini ndiye kiungo anaongoza kwa kucheza pasi nyingi kwenye mechi za hatua ya makundi ya fainali hizi.

Akizungumza na gazeti hili, Lukula, alisema anawaamini wachezaji wake wote na bado moyo wake unamwambia watacheza fainali za michuano hii.

Lukula alisema mechi zote ni ngumu kwa sababu wanakutana na ingwa kutoka nchi mbalimbali, hivyo hakuna mchezo atakaoudharau katika fainali hizi zinazotarajiwa kukamilika ifikapo Novemba 13, mwaka huu.

"Mimi nimekuja kushiriki mashindano, sitaki kurudi nyumbani mapema, tuko hapa Morocco mpaka siku ya mwisho," hayo ni maneno ambayo kocha huyo wa zamani wa She Corporate ya Uganda alikuwa akiyarudia mara kwa mara anapozungumza na wachezaji.

Kocha huyo aliongeza kuwa anatamani kuona malengo yake ya kubeba ubingwa wa Afrika yanatimia ikiwa ni mara yake ya kwanza anashiriki katika fainali hizi.

"Tumekuja kushindana, tumekuja kusaka heshima ya Simba, Tanzania, CECAFA, na sisi wenyewe kama wachezaji na mimi kocha wenu, tunataka kumaliza safari tuliyoianza Dar es Salaam, tunaweza, uwezo tunao," Lukula alisema.

Aliongeza anafahamu kufanya vizuri katika mashindano haya kutapandisha heshima na thamani ya klabu yao ambayo kwenye michuano ya kimataifa kwa upande wa wanaume inaogopwa.

Naye nahodha wa Simba Queens, Oppa alisema kujituma kwa kila mmoja wao ndio siri ya mafanikio na wanaahidi wataendelea na kasi hiyo kwenye mechi itakayofuata.

"Hatujamaliza kazi, tumekuja kupambana na hatujaja Morocco kusindikiza, tunazidi kumshukuru Mungu kwa hatua tuliyofikia, kazi ilikuwa kubwa na ngumu," alisema mshambuliaji huyo.

Bingwa wa michuano hii inayoandaliwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), atapata Dola za Marekani 400,000 wakati mshindi wa pili ataondoka na kitita cha Dola za Marekani 250,000. Timu zilizoingia nusu fainali yaani itakayomaliza nafasi ya tatu na nne kila moja itaambulia Dola za Marekani 200,000.

Timu nyingine zilizomaliza katika nafasi ya tatu kwenye hatua ya makundi kila moja itapata Dola za Marekani 150,000 na kifuta jasho cha Dola za Marekani 100,000 kitakwenda kwa walioburuza mkia kwenye hatua hiyo.

**NJE YA UWANJA**

SIMBA Queens imekuwa timu ya kwanza kutoka Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake na kwa kufika hatua hiyo hadi sasa inauhakika wa kuondoka na Sh. milioni 465.4 na kama ikitinga fainali itaongezewa Sh. milioni 581.8, ikitwaa ubingwa itazawadiwa Sh. milioni 930.9.



# WAAMUZI 10 BORA WA WAKATI WOTE DUNIANI


COLLINA

**DOHA,** Qatar

BILA waamuzi bora, soka linaweza kuwa mchezo ambao hauwezi kuthaminiwa. Mwamuzi ana wajibu wa kuzingatia kanuni wakati wa mchezo wa soka.

**Kila shirikisho la soka huwasilisha maofisa wake wakuu kwa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), ili kujumuishwa kwenye orodha ya waamuzi wa kimataifa. Na waamuzi hupokea mafunzo yao katika kambi za kitaifa zinazohusiana na FIFA.**

Ofisa pekee uwanjani mwenye uwezo wa kuanza na kusimamisha mchezo pamoja na kuwaadhibu wachezaji wakati wa mchezo wowote wa soka ni mwamuzi.

Waamuzi hutoa maamuzi kuhusu mambo yote yanayohusiana na mchezo. Ili kuhakikisha kwamba michezo inakwenda kulingana na mpango, mwamuzi hushirikiana na waamuzi wasaidizi na hata ofisa wa nne.

Ni kazi ngumu na isiyothaminiwa kuwa mwamuzi. Wanaweka juhudi kubwa kufanya mechi za soka kuwa za haki. Unyanyasaji kutoka kwa wachezaji, mashabiki, na uchunguzi wa vyombo vya habari kwa kawaida ndio wanaopata kama malipo.

Kwa miaka mingi, kumekuwa na waamuzi mashuhuri kwenye mchezo huo. Makala haya inawaangalia waamuzi 10 bora zaidi katika historia ya mchezo huo.

### #10. PETER MIKKELSEN (DENMARK)

Baba wa waamuzi wa Denmark, ndivyo ambavyo wakati mwingine huitwa mwamuzi huyu, Peter Mikkelsen. Alifanya kazi kama mwamuzi rasmi wa FIFA katika kipindi chake chote.

Mikkelsen alitunukiwa tuzo ya mwamuzi bora duniani mwaka 1991 na 1993 na Shirikisho la Kimataifa la Historia ya Soka na Takwimu (IFFHS).

Alitangaza kustaafu kazi yake baada ya michezo ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la FIFA la 1998.

### #9. PEDRO PROENCA (URENO)

Pedro Proenca wa Ureno anachukuliwa kuwa mmoja wa waamuzi bora wa wakati wote. Alichezesha fainali zote mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa mwaka 2012, na kumfanya kuwa mwamuzi pekee kufanya hivyo ndani ya mwaka mmoja.

Mwaka 2007 na 2011, Pedro alipokea tuzo ya Mwamuzi Bora wa Mwaka wa Shirikisho la Soka la Ureno. IFFHS ilimtunuku mwamuzi bora zaidi duniani mwaka 2012.

### #8. KIM MILTON NIELSEN (DENMARK)

Kim Milton Neilsen anajulikana kwa umbo lake la urefu wa futi sita na inchi sita, alikuwa mrefu kuliko wachezaji wengi.

Aliongoza michezo 53 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na michezo 154 ya kimataifa katika maisha yake ya soka. Aliteuliwa na FIFA akiwa na umri wa miaka 28.

Mnamo Mei 16, 2009, alistaafu baada ya kufikia umri wa juu unaoruhusiwa na UEFA wa miaka 45.

Aliongoza michezo kadhaa muhimu, ikijumuisha Fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya za mwaka 2004 na 2005 pamoja na robo fainali ya mashindano hayo.

### #7. FRANK DE BLEECKERE (UBELGIJI)

Mwaka 1984 ndio ilikuwa mara ya kwanza kwa Frank De Bleeckere kuwa ofisa wa mechi. Kuanzia mwaka 1998 hadi 2012, alikuwa mwamuzi rasmi wa FIFA.

Bleeckere, mmoja wa waamuzi bora duniani, alipokea tuzo saba zilizoweka rekodi za kuwa mwamuzi bora wa mwaka wa Ubelgiji.

Wakati wa mechi ya kufuzu kwa Kombe la Dunia la FIFA 2002, alisimamia mechi kati ya Cyprus na Ireland.

Frank de Bleeckere aliongoza mashindano mbalimbali ya FIFA, yakiwamo Kombe la Dunia, Mashindano ya Vijana, Kombe la Dunia la Vijana chini ya umri wa miaka 17 na mengine.

Ndiye mwamuzi pekee wa Ubelgiji aliyechezesha mechi saba za Kombe la Dunia.

### #6. OSCAR RUIZ (COLOMBIA)

Oscar Ruiz ni mmoja wa maofisa bora kutoka Colombia. Kuanzia mwaka 1995 hadi 2011, alikuwa mwamuzi wa FIFA.

Amekuwa sehemu ya timu ya waamuzi wa FIFA inayofundisha tangu kustaafu kwake.

Mwaka 1995, Oscar alifanya kwa mara ya kwanza kazi nje ya nchini yake. Aliwahi kuwa mwamuzi wa Kombe la Dunia mara tatu mfululizo (2002, 2006, na 2010).

Pia, alishiriki katika programu ya wasaidizi wa waamuzi inayoendeshwa na Shirikisho la Soka la Amerika Kusini (CONMEBOL).

### #5. MARKUS MERK (UJERUMANI)

Akiwa na umri wa miaka 25, Markus Merk, alikua mwamuzi mwenye umri mdogo zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, mwaka 1988.

Alikuwa mwamuzi bora wa mwaka wa Ujerumani mara sita pamoja na tuzo ya mwamuzi bora wa mwaka wa IFFHS mara tatu.

Kwa sasa anafanya kazi kama daktari wa meno na anahudumu kama mchambuzi kwenye televisheni katika Ligi Kuu Uturuki.

### #4. CÜNEYT ÇAKIR (UTURUKI)

Cakir, mwanachama wa muda mrefu wa orodha ya waamuzi wa FIFA na UEFA, amefanya maendeleo makubwa katika ulimwengu wa soka.

Mturuki huyo, ambaye anachukuliwa kuwa mmoja wa waamuzi bora duniani, amekuwa akichezesha mechi za nyumbani katika nchi yake tangu 2001.

Amesimamia michezo muhimu ya Uturuki ya Super Lig pamoja na mechi muhimu za kimataifa.

Uchezeshaji wake bora ulikuja katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kati ya Barcelona na Juventus mwaka 2015 na nusu fainali ya michuano hiyo kati ya Barcelona na Chelsea mwaka 2012.

Zaidi ya hayo, Cakir aliongoza mechi sita za Kombe la Dunia katika miaka kumi iliyopita.

### #3. BJORN KUIPERS (UHOLANZI)

Mholanzi huyo amesimamia fainali 10 za kimataifa tangu alipopokea beji yake ya FIFA mwaka 2006. Pia Kuipers ameongoza fainali nane za nyumbani.

Mwaka 2002, mwamuzi huyo ambaye sasa amestaafu alianza taaluma yake katika Ligi Daraja la Pili ya Uholanzi na mwaka 2005 tayari alipanda Ligi Kuu, Eredivisie.

Alipokea beji yake ya FIFA mwaka mmoja baadaye, na ndani ya kipindi kifupi, alifanikiwa kusimamia Fainali za Duniani chini ya umri wa miaka 21 mwaka 2006 na 2009.

Katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Kuipers amehudumu kama mwamuzi katika michuano ya Klabu Bingwa Dunia ya FIFA, UEFA Super, Euro, Fainali za Ligi ya Europa, na Fainali za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

### #2. HOWARD WEBB (ENGLAND)

Howard Webb anachukuliwa kuwa mmoja wa waamuzi bora wa Ligi Kuu England na jamii ya Waingereza.

Kama kila mtu mwingine, Webb alikabiliwa na ukosoaji katika kazi yake, lakini alidumisha kiwango cha juu sana hadi kustaafu kwake mwaka 2014.

Webb aliteuliwa kwenye Ligi Kuu mwaka 2005 na akaongoza fainali ya Kombe la Ligi mwaka 2007.

Alikubaliwa kwenye orodha ya FIFA mwaka 2005, na tangu wakati huo amekuwa akisimamia mechi nyingi za hadhi ya juu, pamoja na Kombe la Dunia la 2010 na 2014. Aliongoza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2010 na fainali ya Kombe la Dunia la 2010.

Webb pia aliongoza michezo kadhaa mashuhuri nchini England, ikijumuisha fainali ya Kombe la FA, Ngao ya Jamii na fainali ya Kombe la Ligi. Webb alionekana kwenye BT Sport kama mchambuzi baada ya kustaafu na aliwahi kuwa mkurugenzi wa waamuzi wa Saudi Arabia.

### #1. PIERLUIGI COLLINA (ITALIA)

Pierluigi Collina ndiye mwamuzi aliyeheshimiwa zaidi na wachezaji wote uwanjani. Hakusimamia ujinga na wachezaji mara chache walienda kinyume na mamlaka yake au walimfokea na kumtukana.

Waliofanya hivyo walishughulikiwa ipasavyo. Zaidi ya hayo, hakuleta tofauti yoyote ikiwa ungekuwa mchezaji wa kawaida wa soka au mchezaji bora, Collina hakuonyesha kujali.

Fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1999 kati ya Bayern Munich na Manchester United na fainali ya Olimpiki ya Wanaume ya mwaka 1996 kati ya Nigeria na Argentina ni mashindano yake mawili muhimu zaidi. Pia aliongoza fainali ya Kombe la Dunia la 2022 kati ya Brazil na Ujerumani.

Mafanikio yake makubwa yalikuwa kushinda tuzo ya Mwamuzi Bora wa Mwaka wa IFFHS kwa kuvunja rekodi kwa miaka sita mfululizo.

Baada ya kuchezesha fainali ya Euro 2004, alitangaza kustaafu mwaka 2005.

Ni mmoja wa waamuzi wa soka wanaojulikana sana duniani na kwa sasa ni mshauri wa Kamati ya Waamuzi ya UEFA.

## Nukuu

"Mimi nimekuja kushiriki mashindano, sitaki kurudi nyumbani mapema, tuko hapa Morocco mpaka siku ya mwisho. Tumekuja kushindana, tumekuja kusaka heshima ya Simba, Tanzania, CECAFA, na sisi wenyewe kama wachezaji na mimi kocha wenu, tunataka kumaliza safari tuliyoianza Dar es Salaam, tunaweza, uwezo tunao," **Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula baada ya timu yake juzi kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake.**



"Tangu nilipoondoka Ufaransa, kila kitu kinakwenda chini. Ufaransa inanihitaji. Siihitaji Ufaransa. Hata ukiwa na Mbappe [Kylian], Neymar na Messi [Lionel], haikusaidii. Kwa nini? Kwa sababu huna Mungu (Mimi)," **mshambuliaji wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic**




"Kitu pekee ambacho ni hakika ni kwamba sitamchukua mchezaji ambaye hataweza kucheza mwanzoni mwa mashindano. Sijawahi kupeleka mchezaji aliyejeruhiwa kwenye mashindano makubwa. Kwenda kwenye mashindano makubwa na wachezaji ambao hawafai... ni jambo gumu," **Kocha wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Didier Deschamps, kuhusu hatima ya Paul Pogba na N'Golo Kante kwenda Kombe la Dunia.**






Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' mmoja wa wachezaji wanaonekana katika kasi ya ufungaji. **PICHA: MAKTABA**

# REKODI, TAKWIMU LIGI BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara imeingia raundi ya 10, ikiwa kwenye mzunguko wa kwanza, timu zikiendelea kuchuana vikali kusaka bingwa wa msimu huu.

**Mbali na ubingwa, pia zinawania nafasi ya pili ambayo kama vile bingwa, itakwenda kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa endapo tu Tanzania itafanikiwa kuingiza timu nne kwenye michuano ijayo ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.**

Ligi ya Tanzania imekuwa ngumu mno, kwa sababu hata mshindi wa tatu na wa nne anakuwa na matarajio ya kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, endapo zikitokea nafasi hizo nne huku bingwa wa Ligi Kuu akiwa ndiye mshindi wa Kombe la FA.

Hii imesababisha timu kuonekana kukomaa mno mbali na udhamini wa pesa zilizomwagwa, hivyo kusababisha timu kutofautiana sana pointi.

Katika makala haya, tumekukusanyia takwimu na rekodi za timu pamoja na wachezaji, zikiwekwa kwa mtindo wa namba...

**17.** Ni pointi za Simba na Azam FC kila moja ikimiliki pointi hizo, lakini Wekundu wa Msimbazi wakiwa juu kwenye nafasi ya tatu, huku 'Wanalambalamba' hao wakiwa nyuma yao. Namba hii pia inawakilisha idadi ya mabao ambayo Simba imefunga mpaka sasa na kuifanya kuwa juu ya Azam.

**16.** Hii ni idadi ya mabao ambayo Mtibwa Sugar imeruhusu kwenye wavu wake kugushwa mpaka sasa. Timu hiyo inashika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**15.** Ni pointi ambazo zinamilikiwa na timu tatu kwenye Ligi Kuu ambazo ni Mtibwa Sugar, Mbeya City na Namungo. Pamoja na timu zote hizo kila moja kuwa na idadi hiyo ya pointi, lakini Mbeya City inakaa juu yao kwa idadi kubwa ya mabao ya kufunga. Iko kwenye nafasi ya nne, Namungo ikiwa nafasi ya tano na Mtibwa Sugar inakamata nafasi ya sita.

**14.** Mabingwa watetezi, Yanga ambao pia ndiyo vinara wa Ligi Kuu, wamefunga idadi hii ya mabao mpaka sasa. Si peke yao, bali idadi hii pia imefungwa na Mbeya City inayokamata nafasi ya nne.

**13.** Timu za Prisons, KMC na Geita Gold zina idadi hii ya pointi kila moja kwenye ligi mpaka sasa. Wakati zote zina idadi hiyo sawa, Prisons inaziongoza ikiwa kwenye nafasi ya nane kutokana na tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa. KMC iko kwenye nafasi ya tisa, huku ya 10 ikishikiliwa na Geita Gold.

**12.** Mtibwa Sugar imefunga idadi hii ya mabao mpaka sasa, lakini pia namba hii inasimama kuwakilisha idadi pia ya mabao ya kufungwa ya timu za Kagera Sugar na Dodoma Jiji.

**11.** Ni idadi ya pointi ilizonazo Kagera Sugar mpaka sasa, lakini ikiwakilisha nafasi timu hiyo inayoshika kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**10.** Namba hii inasimama kama idadi ya mechi ilizocheza timu ya KMC, mabao yake ya kufunga na ya kufungwa pia. Timu hiyo inakamata nafasi ya tisa kwenye msimamo.

**9.** Ni idadi ya mabao ya kufunga ya timu za Geita Gold na Kagera Sugar, pia Namungo imeruhusu idadi kama hii kuguswa kwenye wavu wake.

**8.** Coastal Union ina idadi hii ya pointi kibindoni, lakini namba hii inasimama kuwa ni idadi ya kufunga ya timu za Prisons na Ruvu Shooting.

**7.** Ni idadi ya mechi ambazo Coastal Union imecheza, ikiwa ndiyo timu iliyocheza mechi chache zaidi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

**6.** Ni idadi ya mabao ambayo amefunga kinara wa kupachika mabao kwenye Ligi Kuu mpaka sasa, Reliants Lusajo wa Namungo.

**5.** Moses Phiri wa Simba na Sixtus Sabilo wa Mbeya City wamefunga idadi hii ya mabao kila mmoja mpaka sasa wakiwa nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji mabao Ligi Kuu.

**4.** Ni idadi ya mabao ya Feisal Salum wa Yanga na Matheo Antony wa KMC ambayo kila mmoja ameifungia timu yake, nao wakiwa kwenye nafasi ya tatu ya orodha ya wafungaji bora msimu huu.

**3.** Namba hii inasimama kama mabao ambayo yamefungwa na wachezaji kadhaa kila mmoja akiifungia timu yake wakiongozwa na Fiston Mayele wa Yanga. Wengine ni Nickson Kibabage na Charles Ilamfya wa Mtibwa Sugar, Anuary Jabir (Kagera Sugar), Augusatine Okrah (Simba), Hassan Maulid (Mbeya City) na Abdulkassim Suleiman wa Ruvu Shooting.

**2.** Mshindi wa Kiatu cha Dhahabu cha Ligi Kuu msimu uliopita, George Mpole, amefunga idadi hii ya mabao mpaka sasa msimu huu.

**1.** Namba hii inasimama kuwa idadi ya ushindi ambao timu za Polisi Tanzania, Ihefu na Dodoma jijini zimeupata mpaka sasa kwenye ligi.

**0.** Ni hii inawatambulisha vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao hawajapoteza mechi hata moja mpaka sasa.

**NDANI YA 18**



MSHAMBULIAJI wa zamani wa Arsenal, Thierry Henry, hadi sasa anashikilia rekodi ya kutoa pasi nyingi za mwisho 'assists' (20) kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu England, akifanya hivyo msimu wa 2002/03 sawa na Kevin De Bruyne (Man City) aliyejibu mapigo hayo msimu wa 2019/20, wakifuatiwa na Mesut Ozil (Arsenal) - 19, msimu wa 2015/16 na Frank Lampard (Chelsea) - 18 msimu wa 2004/05.

# SOKA



**MKALI WA WIKI**

**JINA KAMILI:** Kieran Tierney
**KUZALIWA:** Juni 5, 1997 (miaka 25)
**ALIPOZALIWA:** Douglas, Isle of Man
**KIMO:** 5 ft 10 in (1.78 m)
**NAFASI:** Beki
**KLABU:** Arsenal
**JEZI:** 3

Akilalamika baada ya kuchaniwa jezi na beki wa Zurich FC, Nikola Boranijasevic, kwenye mechi ya Europa League aliyoifungia Arsenal bao pekee ikishinda 1-0 wiki iliyopita katika Uwanja wa Emirates.

BILA waamuzi bora, soka linaweza kuwa mchezo ambao hauwezi kuthaminiwa. Mwamuzi ana wajibu wa kuzingatia kanuni wakati wa mchezo wa soka.

Uk. 16-17



VICTOR OSIMHEN

# WAAFRIKA WA5 WENYE KIWANGO BORA ULAYA

**LONDON,** England

BARA la Afrika limekuwa nyumbani kwa baadhi ya wanasoka bora duniani kama Didier Droga, George Weah, Yaya Toure na Jay-Jay Okocha.

**Afrika pia imekuwa ikijulikana sana kwa kutengeneza wachezaji mahiri na wenye bidii kwa miaka mingi.**

Msimu wa 2022-23, umekuwa tofauti kwani tumeshuhudia maonyesho mengi mazuri ya wachezaji kadhaa wa Kiafrika kote Ulaya.

Kwa hiyo, makala haya yanaangalia wachezaji watano wa Kiafrika walio katika kiwango bora zaidi barani Ulaya msimu huu, twende sasa...

**#5. ALEX IWOBI - EVERTON**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Nigeria, Iwobi amekuwa imara katika safu ya kiungo ya Everton, huku uwepo wake ukiwa na matunda kwa wachezaji wenzake wa 'Toffees' hao.

Iwobi amefunga bao moja na kusajili pasi za mwisho tano katika mechi 13 za Ligi Kuu England msimu huu. Zaidi ya hayo, amesajili pasi 432 zenye mafanikio, nyingi zaidi kwa mchezaji wa Everton kwa msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, ndiye anayeshika nafasi ya pili katika orodha ya watoa pasi za mabao kwenye Ligi Kuu msimu huu. Iwobi amekuwa ni mchezaji muhimu katika safu ya kiungo kwa kikosi hicho cha kocha Frank Lampard.

**#4. MOHAMED SALAH - LIVERPOOL**

Licha ya Liverpool kuwa kwenye wakati mgumu haswa katika Ligi Kuu, fowadi huyo wa Misri bado ni mmoja wa wachezaji wa Kiafrika wanaofanya vizuri zaidi msimu huu.

Mohamed Salah amesajili mabao manne na asisti tatu katika mechi 12 za Ligi Kuu England katika msimu unaoendelea. Pia amefunga mabao sita na kutoa asisti moja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hakuna mchezaji ambaye ana mabao mengi zaidi ya Salah kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu na anabaki kuwa kivutio muhimu katika kikosi cha kocha Jurgen Klopp.

**#3. TEREM MOFFI - LORIENT**

Mshambuliaji huyu wa Nigeria amekuwa na uwezo mkubwa wa kushambulia na utulivu wake mbele ya lango umekuwa muhimu kwa Lorient.

Terem Moffi amefikisha mabao nane katika mechi 11 za ligi na kwa sasa ni mfungaji bora wa nne kwenye Ligue 1 msimu huu.

**#2. SADIO MANE - BAYERN MUNICH**

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Senegal, alijiunga na Bayern Munich kutoka Liverpool kwa dili la thamani ya pauni milioni 35 wakati wa usajili wa majira ya joto.

Sadio Mane amefunga mabao sita na kusajili pasi mbili za mabao katika mechi 12 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, hadi sasa. Zaidi ya hayo, amefunga mabao matatu na kusaidia moja katika mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mabao 11, idadi kubwa zaidi ya mabao yaliyofungwa na mchezaji wa Bayern Munich katika msimu wa huu wa 2022-23 hadi sasa.

Mane ni mchezaji muhimu katika safu ya ushambuliaji kwa kocha Julian Nagelsmann na itafurahisha kuona kama anaweza kuendeleza ufungaji wake wa mabao.

**#1. VICTOR OSIMHEN - NAPOLI**

Nyota huyo wa Super Eagles, bila shaka ni mmoja wa washambuliaji bora zaidi barani Afrika na utulivu na mbinu yake ya umaliziaji imekuwa muhimu kwa Napoli msimu huu.

Victor Osimhen amefunga mabao saba na kusajili asisti moja katika mechi nane za Serie A akiwa na Napoli hadi sasa. Zaidi ya hayo, amefunga bao moja katika mechi mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ndiye mfungaji bora zaidi wa sasa wa Serie A licha ya kukosa mechi chache kutokana na majeraha.

Osimhen alifunga hat-trick yake ya kwanza ya klabu ya wakubwa katika ushindi wa 4-0 wa Napoli dhidi ya Sassuolo Oktoba 29, mwaka huu.

Anabaki kuwa mchezaji muhimu katika safu ya ushambuliaji kwa upande wa kocha Luciano Spalletti na litakuwa jambo la kuvutia kuona kama ataibuka mfungaji bora wa Serie A mwishoni mwa msimu.

**JE, WAJUA?**



Lionel Messi (227), ndiye mchezaji aliyetwaa Tuzo ya Mchezaji Bora wa Mechi mara nyingi zaidi kwenye historia ya LaLiga, akifuatiwa na Cristiano Ronaldo (93), Karim Benzema (53), Iago Aspas (49) na Antoine Griezmann (49).



# Zaidi mifuko 400 mbolea yakamatwa ikitoroshwa Malawi

**Na Grace Mwakalinga,**
SONGWE

SHEHENA ya mbolea iliyokuwa kwenye mifuko 403, imekamatwa katika Kijiji cha Chitete, wilayani Ileje mkoani Songwe wakati ikijaribu kuvushwa kwenda Malawi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, mwishoni mwa wiki walikamata mbolea hiyo baada ya wananchi kutilia shaka magari matatu aina ya Fuso yakipita kwenye njia ambayo haijazoeleka na wananchi hao.

Gidarya alisema baada ya kuona hali hiyo wananchi waliingia wasiwasi na kutoa taarifa kwa uongozi wa kata ambao waliripoti kwa polisi.

Alisema kamati ya ulinzi na usalama ilifika eneo la tukio na kuyakamata magari mawili aina ya Fuso yakiwa yamebeba mbolea hiyo na pikipiki iliyotumika kwa ajili ya ulinzi kusaidia magari hayo kupita.


"Gari namba T.463 CNN ilikuwa imebeba mifuko 201 na gari namba T.202 DGU ilibeba mifuko 202 na pikipiki MC 885 DFC ilitumika kwa ajili ya kufanya doria kufanikisha kupitisha mbolea hiyo, tumefanikiwa kuwakamata watu wanne mpaka sasa," alisema Gidarya.

"Mbolea hii imekamatwa ikisafirishwa kwenda nchi jirani ya Malawi huko wenzetu wanauza mfuko mmoja Sh. 110,000 wameona bei ni nzuri ndio maana wanatumia njia za panya sasa tutahakikisha tunawakamata wanaovusha mbolea," alisema Gidarya. Akizungumzia tukio hilo, mwakilishi kutoka Mamlaka ya kudhibiti Mbolea Tanzania, Kanda ya Nyanda za Juu kusini, Stephano Mfugale, alisema mbolea hiyo haikuwa na kibali cha kusafirishwa nje ya nchi.

Alisema, wanaendelea na msako kumbaini mfanyabiashara mwenye mzigo huo ambaye alikuwa akiusafirisha kwenda nje ya nchi bila kufuata taratibu za mamlaka zinazohusika na utoaji wa vibaji vya mbolea.

Antony Mwashitete, alisema waliingiwa na hofu kuona magari makubwa yakipita maeneo ambayo hayajazoeleka hali iliyowalazimu kufanya mawasiliano na viongozi wa wilaya kueleza taharuki hiyo.

Alisema kwa umoja wao walikusanyika na kuanza jitihada za kuyazonga magari hayo wakati wakisubiri vyombo vya dola kufanya uchunguzi.




Mwakilishi wa Kampuni ya Gradian Health System nchini, Ibrahim Bakari (kulia), akikabidhi mashine mbili za Oxygen zenye thamani ya Sh. milioni 70 kwa ajili ya wagonjwa mahututi wanaopata matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi wa Hospitali hiyo, Dk. France Rutwashoba, **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mgawo wawalazimu kutumia maji ya mifereji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

BAADHI ya wananchi jijini Mbeya wamesema wanalazimika kutumia maji ya mito na mifereji kutokana na mgawo huku mamlaka husika ikieleza tatizo ni mabadiliko ya hali ya tabianchi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti katika kata za Forest ya zamani, Majengo, Simike na Iganzo, walisema kutokana na matumizi ya maji yasiyo salama wana hofu ya kuibuka magonjwa ya milipuko.

Hadija Ally, mkazi wa Forest ya zamani alisema kuwa ufike wakati mamlaka husika inapotokea mgawo wananchi wapewe taarifa ili wachukue tahadhari ya kutunza maji.

"Tuna zaidi ya wiki moja sasa hakuna majisafi ya bomba na kulazimika kutumia maji ya mito na visima kwa matumizi ya nyumbani na kununua maji ya bomba ya kunywa kwa ndoo moja ya lita 20 kwa bei ya Sh. 700," alisema Hadija.

Mjasiriamali wa kufua nguo (dobi) Ally Joshua, mkazi wa Majengo, alisema kutokana na mgawo huo wanaomba mamlaka husika isambaza maji kwa magari ili kuwaondolea tatizo hilo.

Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (Mbeya -Uwwas), Neema Stanton, alisema mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba taifa yamesababisha kupungua kwa maji kwa kiasi kikubwa na kusababisha mgawo wa maji kwa maeneo mengi ya mkoa huo.

"Tunaendelea kufanya kila jitihada kuona jamii inapata maji na ndio maana huwa tunatoa tahadhari ya matangazo kwa kuwataka kuwa na matumizi mazuri ya maji ya utunzaji wa vyanzo ili kuepukana na ukame," alisema Neema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Maji, Edna Mwaigomole, alisema wananchi wa mkoa huo wataondokana na adha baada ya kuanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji kutoka mto Kiwira Wilaya ya Rungwe ambao utazalisha lita milioni 125 kwa siku.

## Jumuiya ya Maridhiano yakusanya chupa 180 za damu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya Chupa 180 za damu katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, zimekusanywa na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kwa ajili ya kuokoa maisha ya wananchi.

Kwa mujibu wa Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa Mkoa wa Mbeya, Ibrahim Bombo, lengo la kuhamasisha uchangiaji damu ni kuokoa maisha ya wanaojifungua, wanaofanyiwa operesheni na majeruhi.

Alisema ukusanyaji umesaidia kuokoa maisha ya wananchi wengine na hadi sasa wamevuka lengo la asilimia 100 la ukusanyaji damu kila mwezi kwa Jiji la Mbeya na wataendelea kuhamasisha shule nyingine ili kukusanya damu zaidi.

"Mbali na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kufanya shughuli za usuluhishi na utatuzi wa migogoro mbalimbali ikiwamo ya kisiasa, kidini na kiutamaduni tumeamua kujikita pia katika kuhamasisha uchangiaji damu kwa wananchi ili kuokoa maisha ya wagonjwa wa hospitalini," alisema Bombo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema yeye ni miongoni mwa wadau wakubwa wa kuchangia damu mara kwa mara.

Alisema uamuzi wa jumuiya hiyo kuhamisisha uchangiaji damu ni upendo wa hali ya juu na serikali itaendelea kuhamasisha wananchi ili kuokoa maisha ya wahitaji.

"Niliwahi kuokoa maisha ya mjamzito ambaye alikuwa anahitaji damu B+ ili kufanyiwa operesheni na mimi ndiye mtu pekee niliyekuwa na kundi hilo, nilijitolea na kuokoa maisha yake na sasa tumekuwa ndugu, nawahamasisha wenzangu tuchangie damu ili tuwasaidie wenzetu huko hospitali," alisema Dk. Chuachua.

Miongoni mwa wanafunzi waliochangia damu kutoka Sekondari ya Sangu, Kelvin Alex, alisema alihamasika kuchangia damu baada ya kuona hali za wagonjwa hospitali.

Aliipongeza Jumuiya ya Maridhiano kuhamasisha wanafunzi wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea ili kuchangia damu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Sangu, Ismail Mungure, alisema ataendelea kuhamasisha wananchi wake kuchangia damu na kwamba zoezi hilo kwake litakuwa endelevu.



# Wasambazaji mbolea ya ruzuku waiangukia serikali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

UMOJA wa Wakala wa Wasambazaji Mbolea ya Ruzuku umeiomba serikali kuwalipa madai yao ya muda mrefu ili kunusuru mitaji yao na kuwawezesha kuendelea kufanya kazi hiyo.

Ombi hilo lilitolewa jijini hapo na Mwenyekiti wao, Gerord Mlenge mbele ya Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Myasebwa Chimau aliyefika katika mkutano huo kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

“Tunaomba serikali isikilize kilio chetu, msitupuuze, mtusamehe hata kama katika utendaji kazi wetu kulikuwa na viashiria vya ubadhirifu, lakini tulikuwa na nia njema ya kuwahudumia Watanzania,” alisema.

Mlenge aliiomba serikali ifanyie kazi madai yao ili kulipwa kwa kuwa ni ya muda mrefu.

Wakala Albert Silvester alisema viongozi wao wamehangaika kwa muda mrefu kushinikiza serikali ihakikishe wanalipwa madai yao.

Akijibu hoja zao, Chimau alisema ameyachukua mawazo yote ya wadau na atayapeleka kwa Waziri Bashe ili kufanyiwa kazi.

Hata hivyo, alisema tayari serikali imeshaanza kuyafanyia kazi malalamiko ya mawakala hao na taarifa ya uhakiki wa madai yao kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imeshakamilika ili kulipwa.

Pia alizungumzia mikataba baina ya mawakala na kampuni za mbolea, akisema inaonekana mawakala wengi hawakuingia mikataba na kampuni kabla ya kuanza kazi ya kusambaza mbolea.

Aliwataka mawakala hao kuwa na desturi ya kutoa taarifa inapoonekana mahali kuna kikwazo cha upatikanaji wa mbolea ili serikali ifanyie kazi suala hilo kwa haraka zaidi.

“Tunajua tatizo lililoko lisipopatiwa ufumbuzi maana yake kilimo kimekwama, na sisi hatutakubali hili jambo litushinde, lazima litafanyiwa kazi kwa lengo la kuboresha namna ya usambazaji wa mbolea nchini,” alisisitiza Chimau.

## DC awapa angalizo wananchi sumukuvu

**Na Renatha Msungu**, KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remedius Mwema, amewataka wananchi kuacha kuanika mazao chini ili kuepukana na sumukuvu.

Mwema alitoa angalizo hilo juzi alipozungumza na wananchi wilayani humo kuhusu mradi ulioanzishwa wa Udhibiti wa Sumukuvu Tanzania (TANIPAC) unaotekelezwa katika wilaya hiyo ukilenga kukabiliana na sumukuvu.

Alisema Sh. bilioni 19 zimewekezwa katika mradi huo, hivyo ni vyema wananchi wakafuata elimu wanayopewa ili kuepuka sumukuvu ambayo ni hatari katika mazao.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema wananchi wakiendelea kuanika mazao chini, ni wazi watapata madhara, hivyo wanapaswa kuacha ili kujilinda na afya zao na kuongeza nguvukazi katika jamii na kuwa mfano wa kungwa katika nchi zingine.

“Sh. bilioni 19 zimewekwa katika mradi huu ili uweze kukamilika ambapo hadi sasa umewasaidia wananchi kupata ajira 210 zisizo za kudumu ambazo zimesaidia mradi huu kufikia hatua hii na kuleta maendeleo kwa wana Kongwa na wananchi wengine,” alisema.

Mkuu wa Wilaya huyo alisema wakiendelea kuanika mazao chini, watapata madhara kama vile saratani ya koo na kupunguza nguvukazi kwa taifa.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli, alisema upimaji wa sumu kwa kituo hicho umeleta fursa mbalimbali katika jamii hususan vijana.

Alisema wamejenga vituo 14 vya maabara vinavyojihusisha na upimaji wa sumu, kutoa elimu kwa wananchi, kufanya utafiti wa kutengeneza mbegu bora na kupata mazao ambayo hayajaathirika na sumu.

“Upimaji wa sumu kwa kituo hiki umeleta fursa kwa wananchi kupata fursa na huduma bora, ninawashukuru Canada na Benki ya Dunia kwa kuonyesha ushirikiano katika mradi huu wa Udhibiti wa Sumukuvu Tanzania (TANIPAC).

“Tumejenga vituo 14 vya maabara vinavyojihusisha na upimaji sumu kwa mazao na kutoa elimu kwa wananchi ili kuhakikisha kila mwananchi anajua madhara yapatikanayo na sumu na kufanya utafiti wa kutengeneza mbegu zilizo bora,” alisema.




Viongozi wa Chama cha Wakulima Tanzania (TASO) wakiwa pamoja baada ya kuchaguliwa kwenye mkutano mkuu jijini Dodoma jana. (Kutoka kulia) Makamu Mwenyekiti, Joyce Mwanga, Mwenyekiti Taifa, Isidori Mwalongo, Katibu Mkuu, Herry Beji na Naibu Katibu Mkuu, Idd Mbonde. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## TASO yabadili uongozi wao ikitaka mapinduzi ya kilimo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha Wakulima Tanzania (TASO) kimechagua viongozi wapya ili kuleta mapinduzi ya sekta ya kilimo nchini kwa miaka mitano.

Mwenyekiti wa chama hicho, Isdori Mwalongo akizungumza baada ya kuchaguliwa, aliahidi kufanya kazi kuhakikisha sekta ya kilimo inaendelea kutoa mchango mkubwa katika kukuza pato la taifa na kuboresha kipato cha wakulima.

Mwalongo alisema watahakikisha chama kinafanya kazi zake kwa ubunifu mkubwa na weledi ili kukifanya kuwa na thamani kimataifa pamoja na kujenga uhusiano mzuri zaidi na serikali.

“Kwa niaba ya viongozi wezangu, ninapenda kuwahakikishia wakulima kuwaboreshea kilimo chao huku ili kiwe na tija, huku ikiwaondolea kero ambazo leo hii zinakwamisha wakulima wengi kupitia mazao wanayoyalima,” alisema.

Hata hivyo, alisema moja ya vikwazo vinavyowakabili wakulima ni ukosefu wa masoko kutokana na Tanzania kuwa wazalishaji wakubwa wa mazao.

Msimamizi wa Uchaguzi huo kutoka Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA), Julius Msengezi, aliwataka viongozi waliochaguliwa kusimamia mabadiliko ya katiba ili iwanufaishe wakulima.

Alisema vyama vingi vimekuwa vikishindwa kusimamia katiba, hivyo kujikuta vikishindwa kutatua migogoro kwa wanachama wake.

Mwanasheria huyo alikitaka chama hicho kutumia mifumo ya TEHAMA ili iwasaidie katika kuweka kumbukumbu sahihi, hata kwenye utendaji wao wa kazi.



# CHADEMA yapendekeza SMZ kuangalia upya vikosi vyake

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu, amesema ipo haja kwa Serikali ya Zanzibar kuviangalia upya vikosi vyake ambavyo dhima na lengo la uwapo wake haviendani na wajibu wao hasa nyakati za uchaguzi mkuu.

Aliyasema hayo jana katika kongamano la CHADEMA digitali lililoandaliwa na Baraza la Wanawake (Bawacha) mjini hapo.

Alisema vikosi hivyo vinatakiwa kufanyiwa marejeo, uanzishwaji wake na muundo wake ili viwe vya kiadilifu na vinavyoheshimu utu na ubinadamu pamoja na sheria na katiba ya nchi.

"Unamkuta askari wa vikosi vya SMZ anapomshughulikia Mzanzibari mwenzake utafikiri kesho na keshokutwa hawatokutana sokoni wakipigania bei ya dagaa na tungule angalau watoto wao kupata mlo wa mara moja kwa siku," alisema Naibu Katibu mkuu huyo.

Mwalimu alisema CHADEMA imeamua kusamehe yale yote yaliotokea katika uchaguzi wa mwaka 2020 lakini imani yao kwamba safari ya kuelekea 2025 dhamiri inayoeneshwa na watawala akiwamo Rais Dk. Mwinyi atailinda, ataiheshimu na kuisimamia hadi siku ya mwisho ya uchaguzi mkuu.

Alisema imani yao hiyo ni kwamba Rais Dk. Mwinyi atakua tayari ama kuachia kwa atakayeshinda katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025 ama achiwe yeye iwapo atashinda, lakini ushindi huo uwe wa haki.

Alisema juhudi zinazoendelea hivi sasa zitafanya kuwa na uchaguzi huru, haki na wenye kuaminika mbele ya ulimwengu ili Wazanzibari waachiwe haki yao ya kuongozwa na watu wanaomtaka.

Alisema juhudi hizo hazitakuwa na tija kama itafika mwaka 2025 halafu Zanzibar ikarudi katika siasa za chuki, uhasama na ubaguzi unaotokana na Wazanzibari kudhulumiwa haki zao za kiuchaguzi.

"Ni pale tu ambapo tutafanikiwa kufanya chaguzi zenye haki dhamira hii na mema tunayooneshana hivi sasa ambapo Chadema tupo tayari kwa wenzetu kuijenga Zanzibar moja yenye mshikamano uhuru na haki ya watu kujiamulia na kupata pato sahihi bila ya mizengo yoyote," alisema.

Naibu Katibu Mkuu huyo, alisema CHADEMA ipo tayati kufanyakazi pamoja na Rais Mwinyi na Rais Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea maendeleo Watanzania na Wazanzibar na kupongeza hatua iliyofikiwa ya maridhiano ya kisiasa na imefanya kongamano hilo bila ya kubuguziwa.

Aidha, aliwataka wanachama wa chama hicho kushirikiana, kuwa wamoja, kushikamana na kusaidiana ili kufikia malengo ya chama hicho.

Alisema lazima kila mmoja kushirikiana bila ya kuoneana wivu na kuwa na utamaduni wa kuheshimu mchango wa kila mmoja.

Naye Makamu Mwenyekiti wa BAWACHA, Sharif Suleiman, alisema, lazima uwapo ushirikiano na kulijenga Baraza la Wanawake wa chama hicho kwa sababu hakuna mwenye hatimiliki nalo.

Sharifa ambaye ni Kaimu Makamu wa BAWACHA, alisema Baraza hilo limepiga hatua kubwa na katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 wanawake wa chama hicho walisimama kugombea nafasi ya uongozi majimboni kwa nafasi mbalimbali.

Alisema katika chama hicho kuna rasilimali kubwa ya wanawake wenye uwezo lakini bado hawajafikia asilimia inayohitajika kujisajili kidigitali kutokana na kutowafikia wanawake hao majimboni hivyo aliwaagiza watendaji kuwafikia wanawake hao kujisajili kidigitali kulipia ada ya uwanachama.

Kwa upande wake Naibu Katibu Mkuu wa BAWACHA, Caterin Ruge, alisema wanawake wa chama hicho wana fursa ya kufanya siasa na ni wajibu kuangalia historia ya wanamapinduzi wanawake ambao walijitolea kubadilisha mifumo kandamizi kwa wanawake.



Mafundi wakiendelea na ukarabati wa ujenzi wa soko kuu la Darajani lililojengwa miaka 118 iliyopita. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yaanza ukarabati soko kuu la Darajani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Mjini Magharib Unguja, Rashid Msaraka, amesema serikali imeamua kulifanyia ukarabati soko kuu la Darajani ambalo limejengwa tangu mwaka 1904 na ukarabati huo unaendana na hadhi ya Mji Mkongwe wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana visiwani humo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujenzi wa ukarabati wa soko hilo unaoendelea.

Alisema ukarabati huo unatokana na agizo la utelekezaji wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, katika kuimarisha maslahi, vitendea kazi na miundombinu ya wajasiriamali wadogo ili kujenga mazingira mazuri kwa wafanyabiashara hao.

Alisema rais ametoa maelekezo kuona manispaa zinatumia fedha kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi hivyo ukarabati huo upo chini ya maelekezo yake hayo.

Alisema soko hilo linatarajiwa kumalizika Desemba mwaka huu na mwanzoni mwa mwezi wa Januari, mwakani litazinduliwa ambalo ukarabati wake umegharimu Sh. milioni 400.

"Fedha hizi ni za serikali zilizotokana na makusanyo ya manispaa ya mjini kama rais alivyotuagiza kutumia pesa za makusanyo kwa ajili ya miradi ya maendeleo," alisema.

Alisema kabla ya ujenzi kuanza walikaa na wafanyabiashara na kukubaliana kuwa wawepo kando ya soko hilo kuendelea na biashara zao ili litakapomaliza kufanyiwa ukarabati kurejea ndani ya soko hilo kufanya biashara.

Alisema soko hilo litakuwa na kiwango, miundombinu yake yote itawekwa mipya ili soko hilo liendelee kuwa ni moyo wa biashara katika eneo la Darajani na baada ya kumalizika litachukuwa wafanyabiashara 1,500.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Mjini Ali Khamis Muhammed, alisema kabla ya kufanyiwa ukarabati walikaa na Mamlaka ya Mji Mkongwe na kupewa mwongozo wa kufuata vigezo vya ukarabati.

Wafanyabiashara wa soko hilo, walipongeza hatua hiyo ya ukarabati kutokana na kuwa katika hali mbaya ya uchakavu kutokana na soko hilo ni la muda mrefu.

Suleiman Khamis, mfanyabiashara wa soko hilo, alisema ukarabati huo ni hatua ya maendeleo hasa ikizingatiwa kuwa soko hilo ni sura ya utalii wa Zanzibar.

"Matumaini yetu baada ya kumaliza soko hili watalii watamiminika sokoni hapa ambapo wengi wao hufika kwa ajili ya ununuzi wa spice (viungo)," alisema mfanyabiashara huyo.

Mfanyabiashara mwingine Kombo Hamad Ali, alisema walipewa taarifa mapema ya ukarabati wa soko hilo na kuipongeza serikali kwa kuwaruhusu kuendelea kufanya biashara zao kwa lengo la kujipatia kipato.

"Tunaiomba serikali kuhakikisha kwamba baada ya kumalizika soko hili waturejeshe sisi wafanyabiashara tuliokuwapo awali ili kuendelea kufanya biashara zetu maana mimi nipo hapa zaidi ya miaka 30 nafanya biashara," alisema Kombo.

# Wakulima muhogo wakumbushwa kuzingatia mbinu bora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa zao la muhogo visiwani hapo wametakiwa kuzingatia mbinu bora za uzalishaji wa zao hilo.

Kaimu Mkurugenzi Idara ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar, Salma Omar Mohammed, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na wakulima katika uhamasishaji wa mbegu za muhogo zinatokana na mbarika kutoka katika kitalu na kuzipanda shambani.

Alisema lengo la kuzipanda mbegu hizo kuchunguza ustahamilivu wake wa maradhi ya virusi pamoja na kuzizoesha katika mazingira magumu kabla hazijagaiwa wakulima.

Alisema mbegu hizo zikishapandwa zitafanyiwa uchunguzi kwa muda wa miaka mitatu ili kuangalia ustahimilivu wa maradhi, wadudu na uzazi.

"Wizara yetu kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na kwa kushirikiana na Taasisi ya Mazao ya nchi za joto (IITA) itazitafiti mbegu hizi kwa ajili ya kutatua changamoto zinazowakabili wakulima katika zao la muhogo," alisema Salma.

Alisema uzalishaji wa zao la muhogo unaweza kufikia tani 24 hadi 30 kwa hekta moja iwapo wakulima watatumia mbegu bora zenye kustahamili maradhi na wadudu zinazopatikana katika taasisi hiyo iliyoko kizimbani ambazo ni Mahonda na Machui.

Alisema ZARI imeanza kusambaza mbegu hizo kwa wakulima tokea mwaka 2010 kuwasaidia wakulima waepukane na mbegu zinazopata mashambulizi ya virusi na kupunguza uzalishaji wa zao hilo.

Alisema zao hilo hushambuliwa zaidi na maradhi ya michirizi na ukoma yanayopunguza mavuno ambayo pia hatari iwapo mmea wa muhogo utashambuliwa ukiwa na umri wa chini ya miezi sita mkulima hataweza kuvuna chochote.

"Dalili za maradhi ni kuonekana michirizi ya kahawia kwenye kigogo, majani kuwa manjano na muhogo wenyewe kuwa vifundo vifundo na hatimaye kupata na utumbaku ndani yake," alifahamisha Kaimu Mkurugenzi huyo.

Alisema kwa upande wa maradhi ya ukoma dalili zake ni kuonekana majani kuwa manjano na kujikunja ambapo maradhi hayo huathiri sana ikiwa mmea utaweza kushambuliwa chini ya miezi sita na hupunguza mavuno ya muhogo.

Naye Mtafiti wa mazao ya mizizi katika taasisi hiyo, Ali Hamad Ali, aliwataka wakulima wa zao la muhogo kuwa tayari kutumia mbegu zinazofanyiwa utafiti ili kuongeza tija kwenye kilimo.

"Mbegu hizi kufanyiwa utafiti wa miaka mitatu, lakini zipo mbegu nyingine zinazostahimili maradhi, wadudu na zenye uzazi mkubwa ambazo huwa tayari baada ya mwaka mmoja kwa ajili ya wakulima kuzipanda," alieleza mtafiti huyo.

Aidha, alitoa wito kwa wakulima wa zao hilo kuzitunza vizuri mbegu hizo ili kuwaongeza kipato kitakachowaletea tija katika maisha yao na kupunguza changamoto ya uhaba wa chakula.





# Barabara iliyomchefua Majaliwa yakamilika

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MRADI wa barabara ya Nansio-Kilimabuye na Halmashauri-Airport wenye urefu wa kilometa mbili unaotekelezwa kwa kiwango cha lami katika kisiwa cha Nansio, wilayani Ukerewe umekamilika kwa asilimia mia na kukabidhiwa kwa uongozi wa Mkoa wa Mwanza kwa matumizi.

Awali katika ziara ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa mkoani Mwanza ulionekana na madudu kutokana na mkandarasi kuchelewesha na kujenga kwa vipindi hatua iliyosababisha mkandarasi huyo kupewa siku 15 kuukamilisha.

Akipokea mradi huo wakati wa ziara yake katika visiwa vya Ukerewe mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Adam Malima aliwataka wananchi wilayani humo kutumia barabara hizo kwa shughuli za kiuchumi.

Aliwataka kuacha kuendekeza starehe wakati wote wa kazi na kuweka juhudi katika shughuli za uzalishaji ili kuujenga uchumi wao pamoja na serikali.

Akikabidhi mradi huo, Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoa wa Mwanza, Mhandisi Goodluck Mbanga, alisema mradi huo umegharimu Sh. milioni 993 ukibaki ukamilishwaji wa mitaro na taa.

Athanas Masanja, mkazi wa Kilimabuye, wilayani Ukerewe alisema kukamilika kwa barabara hiyo kutarahisisha shughuli za usafirishaji wa mizigo kutoka katika mkoa wa jirani wa Msoma kuelekea Nansio na safari zao za kila siku ambazo awali zilishindikana kutokana na barabara hizo kuwa na mashimo mengi.

Katika ziara yake Mkuu wa Mkoa wa Mwanza wilayani Ukerewe, alishuhudia ujenzi wa mradi wa usambazaji wa maji katika kisiwa cha Gana ambao unatarajiwa kukamilika Desemba 14 na kukabidhiwa Januari Mosi, 2023.

Vilevile, alikagua ujenzi wa msingi wa zahanati ya Gana na kuwasilisha Sh. milioni 20 zilizotolewa na Waziri Mkuu na Rais Samia Suluhu Hassan kama mchango wa kuendeleza ujenzi wa zahanati hiyo.

Malima aliwataka wasimamizi wa ujenzi huo kufanya matumizi mazuri ya fedha pamoja na rasilimali za taifa kukamilisha zahanati hiyo.

Pia aliwataka wananchi kutoa ushirikiano katika ujenzi huo ikiwa ni pamoja na kushiriki katika upatikanaji wa kokoto, mchanga na maji ili kufanikisha ujenzi huo kwa haraka.




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza katika mahafali ya kidato cha nne, Shule ya Sekondari ya Kiislamu Ilala jijini Dar es Salaam jana, alihimiza wazazi kusimamia malezi bora na maadili mema kwa watoto. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Madiwani wahoji utekelezaji mradi TACTIC

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamehoji utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu katika Miji Tanzania (TACTIC) ambao ulitakiwa kuanza utekelezaji Septemba, mwaka huu ili kuondoa tatizo la miundombinu ya barabara katika baadhi ya kata.

Mradi huo ulizinduliwa mwaka jana katika kikao kilichohusu mpango wa uboreshaji wa miundombinu katika miji Tanzania kupitia mpango wa Benki ya Dunia na Manispaa ya Kahama ikiwa ni moja ya eneo la utekelezaji wa kuwa na na taa katika kila barabara.

Awali, mradi huo ulitakiwa kuanza utekelezaji Julai mwaka huu, lakini ilishindikana kutokana na sababu mbalimbali na baadaye madiwani wakajulishwa kuanza utekelezaji Septemba.

Benki ya Dunia imetenga Dola za Kimarekani milioni 500 (Sh. trilioni 1.5) kwa ajili ya mradi huo ambao utahusisha ujenzi wa barabara, mitaro na vituo vya mabasi huku manispaa ikitarajiwa kujenga barabara za urefu wa kilometa saba maeneo ya mjini, kilometa 12.6 eneo la viwanda Zongomela.

Diwani wa Nyasubi, Abel Shija alihoji kuhusu mradi huo katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/ 2023, akitaka kujua utekelezaji wa mradi huo umefikia katika hatua gani ili kutatua tatizo la ukosefu wa miundombinu ya barabara.

Alisema, wamekuwa wakiambiwa muda wa utekelezaji lakini unapofika hawaoni hatua zozote zinazoendelea hali inayozidi kuzalisha maswali kwa wananchi wao na kutaka kujua umefikia katika hatua gani.

Akijibu malalamiko hayo, Mratibu wa mradi huo Manispaa ya Kahama, Enne Moses alisema, bado michoro inaandaliwa na kuna hatua tofauti zinachukuliwa kabla ya kutekeleza na kuahidi muda utakapofika watawajulisha.

Alidai kuwa, mradi huo una hatua nane kabla ya kuanza na sasa wapo katika hatua ya sita, zitakapokamilika watatangaza zabuni ili kuanza utekelezaji.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Thomas Muyonga alisema, chama kimekua katika wakati mgumu wa mradi huo kutokana na wananchi kuahidiwa kuanza utekelezaji.

Aidha alisema, katika kipindi hiki cha mwezi Novemba wangetegemea kupata taarifa ya mkandarasi kuwapo eneo la mradi, lakini majibu yamekuwa tofauti ya upembuzi yakinifu unaendelea na wananchi kukosa matumaini.

## Wanawake watakiwa kubuni mbinu kujikwamua kiuchumi

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WANAWAKE katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, wametakiwa kubuni shughuli za uzalishaji mali zitakazowasaidia kupata mikopo kwenye taasisi za fedha ili kujikwamua kiuchumi na kupunguza utegemezi kwa wanaume.

Hayo yamebainishwa mwishoni mwa wiki na ofisa ushirika wa Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, Goodluck Temba wakati wa mkutano mkuu wa Chama cha Kuweka na Kukopa cha MUVUMA Saccos wilayani humo.

Temba alisema baadhi ya kinamama na vijana wanashindwa kupata mikopo kutokana na kukosa vigezo ikiwa ni pamoja na kutokuwa na shughuli na miradi yenye sifa za kukopeshwa.

"Ukiwa na mradi wa maana utaweza kupata wa kiasi chochote ili kuboresha shughuli zako za uzalishaji mali na itakufanya upate mzunguko wa fedha na kurejesha kwa wakati," alisema Goodlucky Temba.

Aidha, aliwataka kuanzisha miradi ya ufugaji, kilimo na biashara pamoja na ujasiriamali ili fedha wanazochukua kwenye mikopo ziwe zinazunguka na wawe na uwezo wa kuzitumia na kuzirudisha.

Mwenyekiti wa chama hicho, Petronella Julius, alisema chama hicho sio sehemu ya watu waliovuruga kwingine kwa kukopa na kushidwa kurejesha, wanahitaji watu wenye uwezo wa kurejesha fedha endapo watakopeshwa.

Awali, Julius alisema chama cha kuweka na kukopa cha MUVUMA Saccos, kilianzishwa mwaka 2007 kwa kusajiliwa na kupewa namba ya usajili ya SHR1364 na kilianza na wanachama 20 kwa kiingilio cha Sh. 20,000, na mtaji wa kuanzia ulikuwa Sh. 1,130,000, na sasa mtaji ni Sh. 51,684,938.

Kwa upande wake Bernadetha Mlagwa, mwanachama alishauri kuwekeza na kununua hisa kwenye benki ili kuimarisha uchumi wa chama hicho.

## Iran yakiri kuipatia Urusi ndege zisizo na rubani

**TEHRAN,** Iran

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Iran, Hossein Amir Abdollahian, amekiri kwamba nchi hiyo ilitoa ndege zisizo na rubani kwa Urusi.

Inaelezwa kuwa nchi hiyo ilithibitisha rasmi hatua hiyo kwa mara ya kwanza katika mkutano na waandishi, mwishoni mwa wiki iliyopita, huku Abdollahian akibainisha kwamba, utoaji huo ulifanywa kabla ya kuanza kwa uvamizi wa Urusi wa Ukraine.

"Tulikabidhi Urusi idadi ndogo ya ndege zisizo na rubani miezi michache kabla ya vita vya Ukraine," alisema.

Abdollahian alipinga madai kwamba Tehran inasambaza makombora na ndege zisizo na rubani kwa Urusi kwa ajili ya operesheni za kijeshi nchini Ukraine na kuongeza kuwa Iran inaunga mkono kukomeshwa kwa vita nchini Ukraine.

Kauli hiyo ya Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran ilikuja baada ya majadiliano kuhusu Urusi kutumia ndege zisizo na rubani za Iran nchini Ukraine, ikiwa ni pamoja na mashambulizi dhidi ya miundombinu ya nishati na makazi ya kiraia.

Katika wiki za hivi karibuni, Ukraine iliripoti ongezeko la mashambulizi ya ndege zisizo na rubani kwenye miundombinu ya kiraia, hususan matumizi ya ndege aina ya Shahed-136 zilizotengenezwa na Iran.

Aidha, Urusi inakanusha matumizi ya ndege zisizo na rubani za Iran nchini Ukraine.

**WAKAZI KHERSON WAHAMISHWA**

Wakati hilo likiendelea, Rais wa Urusi, Vladimir Putin, aliidhinisha kuhamishwa kwa raia kutoka sehemu za Kherson zinazokaliwa na Urusi kusini mwa Ukraine.

Pia taarifa zilieleza kuwa vikosi vya Kyiv vimekuwa vikisonga mbele kwa kasi katika mji huo wa kimkakati wa bandari.

Putin alisema kuwa watu wanaoishi katika maeneo hatari wanapaswa kuondoka kwani raia hawapaswi kuteseka, huku ikielezwa kuwa takribani watu 70,000 wamehamishwa tayari katika jiji hilo ambalo liliwekwa kizuizini na Urusi tangu Februari.

"Raia walio katika hatari ya kushambuliwa kwa makombora wanapaswa kuondolewa," alisema Putin.

Kyiv inaishutumu Urusi kwa kuwaondoa kwa nguvu raia wa Ukraine hatua ambayo inachukuliwa kuwa uhalifu wa kivita, ingawa Moscow inakanusha hilo.

Mashambulizi makali ya kombora na ndege zisizo na rubani za Urusi kwenye miundombinu ya raia kote Ukraine yamesababisha hasara kubwa na kufanya Kyiv kukatikiwa na umeme mara kwa mara. **BBC**

# Uganda yakanusha kuwaunga mkono M23

**KAMPALA,** Uganda

SERIKALI ya Uganda imefutilia mbali ripoti ya madai kwamba inaunga mkono kundi la waasi la M23 ambao wanashikilia sehemu za mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) huku ikisisitiza kuwa uhusiano wake na nchi hiyo ni mzuri.

Katika taarifa iliyotolewa juzi na msemaji wa serikali ya Uganda Ofwono Opondo, alisema uhusiano wao na Jeshi la Congo (FARDC) na Rais wa DRC pamoja na baraza lake la mawaziri ni mzuri.

Taarifa ya Uganda imetolewa baada ya maseneta wa DRC, makundi ya kutetea haki za kijamii na waandamanaji kudai kwamba Uganda ilikuwa inashirikiana na Rwanda kutatiza usalama wa DRC yenye utajiri mkubwa wa madini.

Wabunge nchini DRC walitoa taarifa kwa vyombo vya habari mwisho wa juma, wakitaka Kinshasa kumfukuza balozi wa Uganda nchini DRC na kufunga mpaka kati ya nchi hizo mbili kutokana na kile wanachoamini Uganda inaunga mkono waasi wa M23.

**WATAKA MPAKA UFUNGWE**

Hayo yanajiri siku chache baada ya DRC kumfukuza Balozi wa Rwanda, Vincent Karega, kutokana na nchi hiyo kusemekana kutuma maelfu ya wanajeshi wake nchini DRC kusaidia waasi wa M23 kupigana na wanajeshi wa serikali ya Kinshasa.

Inadaiwa kuwa taarifa ya wabunge wa DRC haina ushahidi wowote wala kunukuu chanzo cha madai yao kwamba Uganda inaunga mkono waasi wa M23.

Msemaji wa Serikali ya DRC, Patrick Muyaya, aliwaambia waandishi wa habari wiki iliyopita kwamba serikali nchini kwake inachunguza madai ya Uganda kuunga mkono waasi wa M23.

Mapema wiki hii, waandamanaji wenye mabango ya kudai kwamba Uganda na Rwanda zinaunga mkono waasi wa M23, waliandamana hadi kwenye mpaka wa DRC na Rwanda kabla ya kutawanywa na maofisa wa usalama wa DRC.

**MKATABA USINGE SAINIWA**

Msemaji wa Uganda Opondo alisema taifa hilo lisingesaini makubaliano ya ushirikiano juu ya ujenzi wa barabara na kuimarisha usalama kupambana na waasi wa Allied Democratic Forces (ADF), iwapo Uganda inaunga mkono waasi wa M23.

"Hata tulikuwa mstari wa mbele katika mazungumzo ya kundi la M23 kuwa sehemu ya jeshi la DRC," alisema.

Pia inaelezwa kuwa ujenzi wa barabara ya kutoka Bunagana hadi Goma umesitishwa tangu kundi la M23 lilipodhibiti mji wa Bunagana mapema mwaka huu.

Msemaji wa Jeshi la Uganda Brigedia Jenerali Felix Kulayigye, alisema waasi wa M23 walijaribu kuchoma moto magari na vifaa vya ujenzi wa barabara hiyo mjini Bunagana.

"Wamejaribu kuchoma moto vifaa vya ujenzi, ninaposikia madai kwamba tunaunga mkono waasi wa M23, nakasirika sana," alisema Kulaigye.

Ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 89, uliokuwa unatekelezwa na Kampuni ya Dott Services, ulitarajiwa kuharakisha usafirishaji wa bidhaa kutoka Uganda hadi mji wa Goma na kuimarisha biashara kati ya Goma na Kampala.

Maseneta wa DRC walidai kwamba wanajeshi wa Uganda waliwasaidia waasi wa M23 hivi karibuni, kuwashinda nguvu wanajeshi wa DRC katika mapigano ya kuidhibiti Bunagana, madai ambayo msemaji wa jeshi la Uganda Kulayigye anasema kuwa ni 'ndoto ya mchana'. **VOA**



Msongamano wa abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta Kenya (JKIA) jijini Nairobi, baada ya mgomo wa marubani wa Shirika la Ndege la Kenya Airways juzi. **PICHA: BBC**

# Kenya Airways kusitisha safari 40

**NAIROBI,** Kenya

ZAIDI ya abiria 9,000 wamekwama katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta Kenya (JKIA) jijini Nairobi na katika viwanja vingine vya ndege vya kimataifa duniani kutokana na mgomo wa marubani wa Shirika la Ndege la Kenya Airways.

Shirika la Ndege la Kenya Airways limesema jana kuwa safari 40 za ndege zimesitishwa katika siku ya kwanza ya mgomo wa marubani.

Mamia ya abiria wamehamishiwa katika mashirika mengine ya ndege, na wengine kupewa malazi katika hoteli jijini Nairobi wakisubiri mipango mipya ya usafiri.

Shirika hilo la ndege, lilisema linaendesha safari za ndege chache za kimataifa kwa kutumia marubani ambao sio wanachama wa chama cha marubani na ambao hawashiriki mgomo huo.

Foleni ndefu zilishuhudiwa Jumamosi huku wasafiri wenye wasiwasi wakisubiri kwa saa kadhaa kujua hali ya safari zao. **BBC**

# DC abana watendaji usimamizi wa miradi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

MKUU wa Wilaya ya Masasi amewataka watendaji wa serikali wilayani Masasi mkoani Mtwara kusimamia kikamilifu fedha za miradi ya maendeleo ili lengo la kuboresha maisha ya Watanzania lifikiwe.

Claudia Kitta alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza la Madiwani.

Alisema kumekuwa na malalamiko ya mara kwa mara kuhusu ubadhirifu wa fedha za serikali kwenye miradi, ambayo ikifuatiliwa kwa kina inakosa ufuatiliaji.

Kitta alisema, usimamizi wa fedha za serikali zinazoletwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo unapaswa tangu mradi unaanza kutekelezwa katika hatua ya awali badala ya kusubiri tatizo lijitokeze.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi za utekelezaji wa miradi ili ikamilike na kuonesha mafanikio chanya kwa wananchi na kunapokuwa na ubadhirifu ni kukwamisha maendeleo ya wengi.

Kadhalika, alisema watendaji wa serikali na wadau wengine wilayani humo wanapaswa kushirikana kusimamia kikamilifu fedha za serikali na yeyote atakayebainika kufanya kufuja fedha hizo achukuliwe hatua kali kuepusha vitendo hivyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Ibrahim Chaula, alisema wamepokea wazo hilo na kuhakikisha kila mradi unaotekelezwa unasimamiwa kwa ufanisi zaidi.

Aliwataka watendaji wa serikali washirikiane na madiwani kusimamia miradi ya maendeleo kwa kuwa itarahisisha kubaini ubadhirifu na wahusika wanaohujumu miradi ya maendeleo ambayo inatumia fedha nyingi za serikali.



Mbunge wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Santiel Kirumba, akimlisha keki mmoja wa wahitimu katika mahafali ya Shule ya Awali ya St Anne Marie Academy ya Mbezi Kimara kwa Msuguri jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Anayeshuhudia ni Mkurugenzi wa shule hiyo, Dk. Jasson Rweikiza **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wananchi wa Mufindi wafurahia utekelezaji miradi ruzuku ya TASAF

**Na Mwandishi Wetu,** MUFINDI

WATU 21 wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Kijiji cha Isimikinyi, wilayani Mufindi, wamenufaika na mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha vijiji vitatu kupitia ajira za muda.

Mradi huo ulitekelezwa na wananchi baada ya kuibuliwa na Kijiji cha Isimikinyi na walengwa wa Mpango wa TASAF kufanya kazi kwa ujira wa Sh. 3,000 kila siku kwa mwezi.

Ushiriki wa walengwa wa Mpango wa TASAF katika barabara hiyo kwa kushirikiana na jamii kumetajwa kumaliza changamoto ya mawasiliano iliyokuwapo awali katika vijiji vya Isimikinyi, Itengule na Kingege.

Akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki, msimamizi wa mradi huo upande wa TASAF, Janeth Mario alisema ulianza kutekelezwa Septemba mwaka jana na kukamilika Aprili mwaka huu.

Alisema kuna mwitikio mkubwa kwenye utekelezaji wa mradi huo kutokana na wananchi wengi kujua umuhimu wa kushiriki miradi inayoibuliwa.

Alifafanua kuwa fedha walizolipwa zimesaidia kuanzisha miradi midogo midogo ya ufugaji ndani ya familia zao na kuwajengea utamaduni wa kufanyakazi.

Alisema walengwa baada ya kuelimishwa maana ya mradi na faida za kushiriki kwenye kazi za ajira za muda, kaya za walengwa wa TASAF zenye watu wenye nguvu za kufanyakazi zilionesha mwitikio mzuri, hali inayoonesha mwanzo mzuri wa mwelekeo huo.

Mlengwa wa TASAF aliyeshiriki mradi huo, James Mpatule (66), mkazi wa Kijiji Isimikinyi, alisema walengwa wenzake wameelimika na wameanzisha miradi ya ufugaji ng'ombe, kuku na nguruwe kupitia ruzuku.

Alisema kupitia elimu hiyo, panapojitokeza miradi ya ajira za muda ndani ya jamii walengwa wa TASAF wanajitokeza kufanyakazi, ili waweze kupata fedha kwa ajili ya kuimarisha miradi yao na kupata ziada kwa ajili ya kutunza familia.

Mpatule alisema elimu wanayoipata kutoka kwa wataalamu wa TASAF imewaondoa kwenye matumizi mabaya ya fedha za ruzuku, kidogo wanachopata wanakikimbiza kwenye maendeleo.

## Wapewa mbinu kukabili malaria

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU wa Elimu, Malezi na Mazingira wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Buyuni, Faridu Sadick, amewahimiza Watanzania kutumia dawa za kibaiolojia zinazozalishwa katika kiwanda cha viuatilifu mjini Kibaha mkoani Pwani, kuangamiza mbu waenezao malaria na wadudu wengine.

Alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati viongozi wa chama hicho kutoka kata nne za Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam walipotembelea kiwanda hicho.

Sadick alisema wamejiridhisha kuwa dawa hizo hazina madhara kwa binadamu na viumbe wengine na kuiomba jamii isiogope kutumia.

Kwa upande wake, Ofisa Biashara Mkuu wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Doris Rutina na Meneja Uzalishaji wa kiwanda hicho, Gasper Philip, walisema licha ya juhudi kubwa zinazofanywa kuhamasisha jamii kuhusu matumizi ya dawa hizo, jamii haijahamasika vya kutosha.

Walisema kutokana na hali hiyo wanaendelea kutoa elimu na kutafuta mawakala wa usambazaji ziwafikie wananchi kwa urahisi.

## Wanaorudia sekondari wabainika kukata tamaa

**Na Mary Geofrey**

BAADHI ya wanafunzi wanaorudia masomo ya sekondari, wanasumbuliwa na tabia za utoro na kujikatia tamaa ya maisha, hali inayofanya washindwe kufikia ndoto zao.

Mkuu wa Shule Huria ya Ukonga Skillfull, Allen Tibaigana, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa mahafali ya wanafunzi wa kidato cha nne na kusema wanalazimika kutumia wanasaikolojia ili kuwaweka sawa.

Alisema mwasisi wa shule hiyo amejitahidi kuwarudisha kwenye njia sahihi za kupenda masomo na kuachana na makundi ili kufanya vizuri katika masomo yao.

"Kazi ya kuwafundisha vijana waliofeli mtihani siyo rahisi, wapo waliokuwa na tabia za kutoroka darasani lakini sisi tunajivunia kuwabadilisha na sasa wamekuwa watoto wazuri wanaofanya vizuri darasani," alisema Tibaigana.

Mwasisi wa Shule hiyo, Diodorus Tabaro alisema shule yake imefanikiwa kuwabadilisha vijana wengi waliokuwa wamekata tamaa kwa kufeli katika mitihani ya kidato cha nne na wengine darasa la saba hadi kufanya vizuri kwenye mitihani ya kidato cha sita.

Tabaro alisema watoto hao wasingepata elimu wanayoitoa, wangekuwa ni kundi kubwa la watoto hatarishi mtaani.

BURUDANI

# Dimpoz atoa ushauri wasanii wachanga

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Omary Nyembo, maarufu Ommy Dimpoz, ametoa mtazamo wake kuhusu suala zima la wasanii wakubwa kuwasaini wasanii wadogo.

Amesema wasanii wakubwa kuwasainisha wanamuziki wadogo ni jambo la muhimu katika kukuza muziki huo, lakini ni biashara.

Dimpoz alitoa maoni hayo juzi wakati alipokuwa akitambulisha albamu yake mpya ya kwanza aliyoipa jina la Dedication.

"Unatakiwa kumsaini msanii kama vile kurejesha kwa jamii, lakini ni biashara," alisema Dimpoz.

"Hivyo, unatakiwa kama wewe unafanya video ya milioni 10 basi msanii wako walau umfanyie video ya milioni nane.

"Lakini si wewe unafanya video ya milioni 10 halafu msanii wako unamfanyia video ya laki saba, hiyo si sawa," alisema.



# WAWILI BADO WASHIKILIWA KIFO MTOTO WA DAVIDO



**LAGOS,** Nigeria

WAFANYAKAZI wawili wa nyumbani ambao ni washukiwa wa kifo cha Ifeanyi, mtoto wa mwanamuziki wa Nigeria, David Adeleke na mpenzi wake Chioma Rowland, wanaweza kukabiliwa na mashtaka ya uzembe.

Watu nane waliokuwapo wakati mtoto huyo akifariki kwa kuzama kwenye bwawa la kuogolea walishikiliwa na polisi kwa mahojiano.

Sita waliachiwa, lakini mpishi na mlezi maalum wa mtoto huyo bado wanashikiliwa na polisi.

Kwa mujibu wa vyombo vya habari vya Nigeria, washukiwa hao wawili wanaweza kubaki chini ya ulinzi wa polisi hadi watakapoidhinishwa na ripoti ya uchunguzi wa maiti.

Wanaweza pia kushtakiwa kwa uzembe kwa sababu walikuwa wanamsimamia moja kwa moja Ifeanyi wakati wazazi wake hawapo.

Chanzo kimoja kilinukuliwa kikisema: "Mpishi na Yaya wake ndio walikuwa na mtoto moja kwa moja, kwa hiyo wana hatia ya uzembe hadi uchunguzi wa maiti ufanyike."

"Wakati wa uchunguzi, tuna washukiwa, na kulingana na kesi, washukiwa wanaweza kuachiwa au wasiweze kuachiwa," ilisema taarifa ya polisi.

Hadi sasa familia haijapinga uchunguzi wa maiti, lakini jinsi itafanywa haraka inategemea hospitali. Lakini hatua inayofuata ni kukagua kamera za nyumbani.

Msemaji wa Kamanda wa Polisi wa Jimbo la Lagos, Benjamin Hundeyin, ambaye alithibitisha kuzuiliwa kwa mpishi huyo na yaya, alikataa kutoa maelezo zaidi kuhusu uchunguzi unaoendelea.

# *Ali Kiba amtambulisha Vanillah*

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva na Mkurugenzi wa Lebo ya Kings Music, Ali Kiba, amemtambulisha rasmi msanii wake mpya, Vanillah.

Akizungumza kupitia ukurasa wa Instagram wa Kings Music, ameeleza sifa kadhaa za Vanillah akisema kuwa anajua sana muziki na pia ana mwonekano wa usanii.

Kiba ameeleza namna alivyowasaidia wasanii mbalimbali kupitia kolabo zao, lakini pia pale wanapomwomba ushauri wa kusikiliza nyimbo zao.

Amewataja pia Cheed na Killy kama zao lake ambao hivi karibuni walitemwa na Lebo ya Konde Music inayomilikiwa na Harmonize.



# MGUNDA AWAONYA NYOTA SIMBA VS SINGIDA BIG STARS

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, amewataka wachezaji kusahau matokeo yote ya mechi zilizopita na badala yake watazame kazi zilizoko mbele yao hususan kuelekea mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara Jumatano wiki hii dhidi ya Singida Big Stars.

**Simba wanatarajia kuivaa Singida Big Stars keshokutwa katika Uwanja wa Liti mkoani humo.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema, hakuna kitakachowasaidia ikiwa watakuwa wanakumbuka matokeo na mabao yaliyopita hivyo wanapaswa kufikiria kuanza upya.

Alisema wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kusahau matokeo ya mechi zilizopita, nguvu kubwa kuelekeza kwenye mechi zijazo ikiwamo kufanyia kazi madhaifu yaliyojitokeza mechi za awali na kuboresha ubora wao kuwa imara zaidi.

"Tumeshinda mchezo wetu dhidi ya Mtibwa Sugar na kupata pointi tatu, hilo limeisha ilikuwa hivyo hata tulipofungwa na Azam FC baada ya mchezo nilikaa na wachezaji na kuwaeleza matokeo yaliyopita ni lazima tuyafute kichwani tuanze upya," alisema Mgunda.

Alisema kila mechi inapomalizika ni mwanzo mpya wa maandalizi ya mchezo unaofuata na kwamba wanayachukuwa mazuri kuendelea kufanyia kazi ili kuwa bora wanapokwenda kwenye mechi zinazofuata.

Kocha huyo alisema maandalizi ya mchezo huo yanaendelea vizuri na wapo tayari kupambania alama tatu.

Simba ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na alama 17, tatu nyuma ya vinara wa ligi hiyo, Yanga, huku Singida Big Stars ikishika nafasi ya saba baada ya kuambulia pointi 14 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara nane hadi sasa.

**MITINDO...**



Wahitimu wa Shule ya Awali ya St Anne Marie Academy ya Mbezi Kimara kwa Msuguri, Dar es Salaam, wakionyesha mitindo ya mavazi wakati wa mahafali ya 20 ya Shule ya Awali yaliyofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# *Mbuni yanyonyolewa, yashushwa kileleni*

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza baada ya mechi saba, timu ya Mbuni FC imeshushwa kileleni mwa msimamo wa Ligi ya Championship baada ya juzi kupokea kipigo kizito cha mabao 4-0 kutoka kwa KenGold, mechi ikichezwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Kipigo hicho kilihitimisha mfululizo wa timu hiyo kuongoza ligi hiyo, kabla ya kushushwa kileleni kwenye raundi ya nane na nafasi yake kuchukuliwa na Fountaine Gate ambayo iliidungua Transit Camp bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Gairo, Morogoro.

Bao hilo lilifungwa na straika wa zamani wa Simba, Danny Mrwanda dakika ya 61.

Timu hiyo yenye maskani yake jijini Arusha, imeshushwa mpaka nafasi ya tatu ikibaki na pointi zake 18 na huenda hali ikawa mbaya zaidi, kwani inaweza kushuka tena kutegemea na matokeo ya mechi ya JKT Tanzania dhidi ya Pan African iliyotarajiwa kuchezwa jana jioni kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Wakati Fontaine Gate ya Dodoma ikikamata usukani, Kitayosce ya Tabora imekwea hadi nafasi ya pili baada ya kuichapa Copco bao 1-0 kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza, likifungwa na Mkongomani Fabrice Wangoy.

Matokeo mengine ya mechi za juzi kwenye ligi hiyo kwa ajili ya kusaka timu zitakazopanda daraja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao, Biashara United ililazimishwa suluhu dhidi ya Mashujaa, mechi ikipigwa Uwanja wa Karume, huku Green Warriors ikiitafuna Gwambina mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam.

Msimamo sasa unaonyesha Fountaine Gate ina pointi 21. Kitayosce ikiwa kwenye nafasi ya pili kwa pointi 20, Mbuni nafasi tatu ikiwa na pointi 18, Mashujaa ikikaa nafasi ya nne kwa pointi 18 pia, huku JKT Tanzania kabla ya mechi ya jana ikiwa kwenye nafasi ya tano kwa pointi zake 16.

# Ndalichako ahimiza mazoezi kazini

**Na Frank Monyo**

WAAJIRI nchini wametakiwa kuwa na programu endelevu za mazoezi kwenye maeneo yao ya kazi kwa lengo la kuwalinda wafanyakazi dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza ambayo kwa mujibu wa takwimu za hivi karibuni, yamekuwa chanzo kikubwa cha vifo.

Wito huo umetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (pichani chini), alipokuwa akizungumza mwishoni mwa wiki na mamia ya waajiri na wafanyakazi walioshiriki katika bonanza la michezo lililoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).

Bonanza hilo lililowashirikisha waajiri zaidi ya 100, lilifanyika katika viwanja vya Leadres Club vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam ambapo timu za waajiri zilishindana katika michezo mbalimbali ikiwamo mpira wa miguu, mpira wa pete, mbio fupi, kuvuta kamba, kufukuza kuku na kukimbia kwenye magunia.

Aidha, Waziri Ndalichako aliwakumbusha waajiri kuweka mifumo madhubuti ya usalama na afya mahali pa kazi ili kuwakinga wafanyakazi na vihatarishi vya magonjwa na ajali ambazo zimekuwa zikighirimu maisha ya watu au kuwasababishia ulemavu.

"Ninawapongeza sana waajiri wote ambao wameitikia wito wa ATE na kujitokeza kwenye bonanza hili kwa wingi kwani mwitikio umekuwa mkubwa sana, hivyo nawasisitiza kwamba programu kama hizi kuwa endelevu," alisema Prof. Ndalichako, nakuongeza kuwa:

"Kwa upande wa OSHA, ninawashukuru kwa kuona umuhimu wa kuwahamasisha masuala ya mazoezi kwa sababu natambua kwamba wameshiriki kwa kufadhili bonanza hili ambalo limefanikiwa kwa kiwango kikubwa na ningependa kuona kwamba linakuwa endelevu."

Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndomba, alisema lengo la kuandaa bonanza hilo ni kuwahamasisha waajiri kuona umuhimu wa kuwekeza katika afya za wafanyakazi kwa ajili ya maendeleo ya biashara na uwekezaji nchini.

"Tunashukuru waajiri kwa kuitikia wito wetu wa kushiriki kwenye bonanza hili kwani mwitikio umekuwa mzuri. Jumla ya waajiri 129 wameshiriki pamoja na kwamba bonanza hili tumelifanya kwa mara ya kwanza. Hivyo, tunawakumbusha waajiri kuwekeza katika afya za wafanyakazi kupitia programu za mazoezi kwenye maeneo yao ya kazi," alisema Ndomba.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEAO AGOMBEWA EPL

KLABU ya Chelsea na Manchester City, zitachuana kuwania saini ya mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, 23, huku ofa zikitarajiwa kuwa kati ya pauni milioni 105. ***(Tutto Mercato via Mail)***

### MADRID YAIHOFIA LIVERPOOL

REAL Madrid wana wasiwasi kwamba mbinu ya Liverpool kwa kiungo wa kati wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19, "imetatiza" jitihada zao za kumfanya kuwa mchezaji wao mkuu wa usajili msimu wa majira ya joto. ***(Marca)***

### UTD YAZIDIWA KWA ENDRICK

KLABU za Paris St-Germain, Chelsea na Real Madrid zimesonga mbeleya Manchester United katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Palmeiras, Endrick. Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 16, anayeitwa "Neymar mpya", anaweza kuondoka katika klabu hiyo kwa pauni milioni 52 atakapofikisha umri wa miaka 18. ***(Fabrizio Romano via Sun)***

### MILAN KUANZISHA MAZUNGUMZO

AC Milan ina hamu ya kuanzisha tena mazungumzo ya mkataba mpya na Rafael Leao, ambaye mkataba wake wa sasa utaendelea hadi msimu wa majira ya joto mwaka 2024. ***(Calciomercato)***

### SESKO AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko, 19, lakini mchezaji huyo wa RB Salzburg ana makubaliano ya awali ya mkataba na klabu dada ya RB Leipzig. ***(Telegraph)***

### BAMBA BADO LULU ARSENAL

ARSENAL wanaendelea kumfuatilia kiungo wa kati wa Vitoria Guimaraes aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 26, Ibrahima Bamba, 20, lakini wanakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa Atalanta na Villareal. ***(Mirror)***

### TEN HAG NA VLAHOVIC

KOCHA Erik ten Hag pia ana nia ya kumshawishi mshambuliaji wa Juventus na Serbia, Dusan Vlahovic, 22, kutua Old Trafford. ***(Sun)***

### JORGINHO MSHAHARA MKUBWA

KIUNGO wa kati wa Italia, Jorginho, anataka pauni milioni 12 kwa mwaka - mara mbili ya mshahara wake wa sasa ili kubakia Chelsea. Mkataba wake wa sasa unamalizika majira ya joto. ***(Sport)***

### TORRES AONGOZA KWA EMERY

MLINZI wa kati wa Villareal na Hispania, Pau Torres, 25, anaongoza kwenye orodha ya wachezaji wanaotakiwa na Kocha mpya wa Aston Villa, Unai Emery. ***(La Razon)***

### ARSENAL BADO NA TIELEMANS

ARSENAL bado inamnyatia Youri Tielemans, 25, wa Leicester City raia wa Ubelgiji. ***(Express)***

### ALBA ANUKIA NAPOLI

MLINZI wa kushoto wa Barcelona na Hispania, Jordi Alba, 33, hayumo katika mipango ya kocha Xavi na anaweza kuhamia Napoli. ***(El Nacional)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PIQUE ASTAAFU RASMI BARCA KWA MACHOZI

**BARCELONA,** Hispania

GERARD Pique amesisitiza kuwa "sio kwaheri" baada ya kucheza mchezo wake wa mwisho akiwa na Barcelona kwenye Uwanja wa Camp Nou kabla ya kustaafu rasmi soka, Jumamosi.

**Pique alitolewa kwa shangwe katika dakika ya 84 ya ushindi wa 2-0 wa Barca dhidi ya Almeria baada ya mabao ya kipindi cha pili kutoka kwa Ousmane Dembele na Frenkie de Jong kuwaweka 'Blaugrana' hao kwenye ushindi wa 11 katika mechi 12 zilizopita za LaLiga.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, alitangaza Ijumaa kuwa atastaafu soka Jumamosi, na klabu hiyo ilikubali kusitisha mkataba wake kabla ya kuanza kwa Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwezi huu.

**Ni wakati wa kuondoka, lakini nina hakika siku zijazo nitakuwa hapa tena, hii si...**

Pique aliondoka uwanjani kwa hisia dhidi ya Almeria ambapo alimkumbatia kila mmoja wa wachezaji wenzake.

Akiwahutubia mashabiki baada ya mchezo huo akiwa na kipaza sauti mkononi, Pique akiwa analia machozi alisema: "Kutaka ni kuachia. Kuna upendo na shauku kubwa kati yangu na Barca.

"Ulikuwa wakati wa kuondoka... lakini nina hakika kwamba katika siku zijazo nitakuwa hapa tena. Tayari niliondoka na kurudi.

"Hii si kuaga. Nimekuwa mwanachama tangu kuzaliwa hapa, na nitafia hapa."

Wachezaji wa Barca walipamba jezi maalum kabla ya mchezo ilioyoandikwa mbele 'Sempr3" na jina na namba ya Pique nyuma, na neno 'sempre' likimaanisha 'daima' kwa Kihispania, na namba tatu ya Pique aliyokuwa akiitumia.

Sergio Busquets pia alitoa pongezi kwa mchezaji mwenzake ambaye amecheza naye Barca tangu mwaka 2008 baada ya mchezo huo, akisema: "Anaondoka na urithi wa ajabu.

"Kuichezea Barcelona kunamaanisha zaidi kwake kuliko ilivyo kwa mtu yeyote."

SportPesa LIVE IN PLA

MECHI KALI
RAYO VALLECANO
VERSUS
REAL MADRID
1 | 4.91
X | 4.01
2 | 1.62

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GIROUD AKASIRIKA KUJIPA KADI NYEKUNDU




**MILAN,** Italia

OLIVIER Giroud "alikasirishwa" na yeye mwenyewe kwa kusahau kuwa tayari alikuwa amepewa kadi ya njano alipovua jezi yake kushangilia bao la ushindi la AC Milan dakika za lala salama dhidi ya Spezia.

Giroud alitoka kwenye benchi na kuipa Milan ushindi wa 2-1 dakika ya 89 baada ya kuunganisha pasi ya Sandro Tonali, Jumamosi.

Mshambuliaji huyo wa Ufaransa alionyeshwa kadi ya njano ya kwanza dakika sita kabla ya kufunga bao lake hilo.

Giroud amekuwa kwenye kiwango bora wiki hii, akifunga mabao mawili na kutoa pasi nyingi zaidi katika ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Salzburg kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kukiweka kikosi hicho cha kocha Stefano Pioli katika hatua ya mtoano wa timu 16-bora Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 36, alisahau kwamba awali alikuwa ameshapewa kadi ya njano.

"Hakika lilikuwa bao zuri sana, ambalo lilikuja kutokana na pasi ya Tonali," alisema akiiambia Sky Sport.

"Tulitaka kushinda mechi hii, cha muhimu ni kuwa na pointi tatu zaidi kwenye msimamo, lakini nina hasira kwa sababu nilisahau kama nilikuwa na kadi ya njano ya kwanza."



## 'Penalti ilinipa wasiwasi sana'

**MANCHESTER,** England

ERLING Haaland alielezea penalti yake ya dakika za lala salama dhidi ya Fulham kama "mojawapo ya nyakati nilizokuwa na wasiwasi sana maishani mwangu", alipofunga bao na kuipeleka Manchester City kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England.

Mkwaju huo wa penalti uliipa City ushindi wa mabao 2-1 nyumbani Jumamosi baada ya kucheza kwa zaidi ya dakika 64 wakiwa na wachezaji 10 kutokana na kadi nyekundu ya Joao Cancelo.

Haaland, ambaye alianzia benchi baada ya kukosa michezo miwili kutokana na jeraha la mguu, alichukua nafasi ya Julian Alvarez dakika ya 64 na alifunga bao lililokataliwa kwa kuotea kabla ya kuzamisha nyavuni penalti hiyo.

Alvarez alikuwa ameipa City uongozi, lakini Cancelo alipomwangusha Harry Wilson kwenye dakika ya 26 aliipa Fulham penalti na kujipatia kadi nyekundu, hivyo mchezo kubadilika.

Andreas Pereira alisawazisha na City hawakuwa huru katika ushambuliaji wao baada ya hapo.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Haaland alisema: "Ajabu, nilikuwa na wasiwasi. Ulikuwa mojawapo ya wakati wa wasiwasi sana katika maisha yangu.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

# DUBE AELEZA MAGUMU ALIYOPITIA MABAO AZAM

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Azam FC, Drince Dube, amekiri kupitia kipindi kigumu kwenye maisha yake ya soka mpaka alipofanikiwa kupata bao kwenye mechi dhidi ya Simba na mechi iliyofuata dhidi ya Ihefu.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Dube raia wa Zimbabwe ambaye misimu miwili iliyopita alikuwa moto wa kuotea mbali, lakini msimu uliopita akaandamwa na majeraha, alisema ilikuwa ni furaha sana kwake na kupatwa na hisia kali alipofunga bao dhidi ya Simba Oktoba 27, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Unajua, nachoweza kusema nimepitia kipindi kigumu sana kwenye mpira, unapokuwa hufungi, wengi watakuhukumu kwa hilo, kutofunga muda mrefu, halafu unafunga kwenye mechi dhidi ya Simba na nyingine inayofuata, nilijihisi nimeutua mzigo. Machozi ya furaha yalinitoka, ni hisia kubwa kufunga bao kwenye timu kama Simba, lakini natakiwa kuendelea kufunga hata kwenye timu zingine," alisema mchezaji huyo.

**Alisema angalau msimu huu anaona ameanza kurejea kwenye kiwango chake cha kawaida taratibu, lakini msimu uliopita hakuwa vizuri kutokana na kukumbwa na majereha.**

"Washambuliaji tunapitia kipindi kigumu hasa unapokuwa hufungi, wengi wanaanza kukusema na kukuhukumu, lakini nashukuru nimefanikiwa kufunga mabao mawili kwenye mechi mbili mfululizo.

Mbali na kufunga kwenye mechi dhidi ya Simba, bao pekee lililoipa ushindi wa 1-0, Dube alifunga lingine kwenye mechi iliyofuata dhidi ya Ihefu Oktoba 31, nalo liliiwezesha Azam kupata ushindi kama huo.

Dube anatarajiwa tena kukiongoza kikosi cha Azam keshokutwa, Jumatano kwenye Uwanja wa Azam Complex, timu yake itakapocheza dhidi ya Dodoma Jiji katika mechi ya 10 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

**TAIKONDO...**



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Ilala Islamic, wakionyesha mchezo wa Taikondo katika mahafali ya kidato cha nne shuleni hapo yaliyofanyika viwanja vya Masjid Tagwa, Ilala Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Simba Queens yabeba mil. 540/-

INATOKA UKURASA 32

wake waongeze juhudi kwenye kushambulia ili wafunge magoli na hatimaye kupata ushindi.

Mganda huyo alisema mabadiliko aliyofanya ya kumwingiza Asha Djafari na Vivian Corazone Odhiambo yalisaidia kuongeza nguvu katika kikosi chake na hatimaye kupata mabao mawili yaliyowafanya wasonge mbele kwenye michuano hiyo.

"Napenda kumshukuru Mungu, wachezaji, viongozi wote wa Simba na mashabiki, tumekuja kuchukua kikombe, tutaendelea kupambana kuhakikisha tunafikia malengo, uwezo na nia ya kuleta heshima tunayo, " alisema kocha huyo.

Aliongeza kuwa anafurahi pia kuona amekuwa Mganda wa kwanza kuipeleka timu katika hatua hiyo na anawashukuru Simba kwa kumpa nafasi ya kuiongoza timu kufika hatua hiyo kwenye fainali hizo.

Oppa Clement, nahodha wa Simba Queens, alianza kwa kuwashukuru mashabiki wa klabu hiyo kutokana na sapoti ambayo wamewapa kuanzia mwanzo wa mashindano hayo yanayofanyika kwa mara ya pili barani hapa.

## *Nabi aipa ulinzi, mbinu Yanga SC*

INATOKA UKURASA 32

kufunguka na tunafanyia kazi kwa ajili ya kuwa imara zaidi," alisema Nabi.

Alisema mechi haitakuwa rahisi na hawatacheza kwa sababu ya historia bali amewataka wachezaji kila mmoja kupambana kwa ajili ya kwenda kutafuta matokeo mazuri katika mchezo huo.

Kikosi cha Yanga kinaendelea kujifua katika mji wa Sousse ambako wameweka kambi Yanga na kesho, Jumanne asubuhi kitaanza safari kuelekea Tunis kwa mchezo huo utakaopigwa Jumatano.

Timu itakayofuzu itasubiri kujua wapinzani wake watatu kwenye hatua ya makundi wakati droo itakapochezeshwa Novemba 16, mwaka huu jijini Cairo, Misri yalipo makao makuu ya CAF.


## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 07/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:00 | 3030 | Surkhon Termez vs Dinamo Samarqand | 1.41 | 4.09 | 6.81 |
| 12:30 | 2385 | Shandong Luneng vs Shanghai Shenhua | 1.52 | 3.79 | 5.64 |
| 14:00 | 1371 | Tianjin Teda vs Hebei Zhongji | 1.03 | 11.67 | 22.38 |
| 14:15 | 1858 | Kokand 1912 vs Bunyodkor | 2.44 | 2.78 | 3.03 |
| 14:15 | 5286 | Otmk Olmaliq vs FC Olimpik | 1.75 | 3.11 | 4.86 |
| 14:15 | 5553 | Sogdiyona Jizzax vs Lokomotiv Tashkent | 1.64 | 3.51 | 4.88 |
| 14:30 | 3594 | Chengdu Qianbao vs Changchun Yatai | 2.04 | 3.10 | 3.49 |
| 16:00 | 1312 | Sidama Bunna SC vs Adama City FC | 2.28 | 2.82 | 3.26 |
| 16:00 | 2758 | Ruvu Shooting vs Tanzania Prisons | 2.36 | 2.73 | 3.22 |
| 16:00 | 3009 | Buqaa Amman vs AL Karmel | 1.94 | 3.50 | 3.75 |
| 16:00 | 3807 | Wigan U23 vs Barnsley U23 | 1.62 | 4.40 | 3.91 |
| 16:00 | 5731 | AL Tora vs Al-Arabi | 2.86 | 3.01 | 2.39 |
| 16:30 | 1231 | Nasaf Qarshi vs Neftchi Fargona | 1.32 | 4.66 | 7.77 |
| 16:30 | 2118 | Metallurg Bekabad vs Navbahor Namangan | 4.78 | 3.02 | 1.79 |
| 16:30 | 4180 | Pakhtakor vs Qizilqum | 1.32 | 4.37 | 8.74 |
| 18:00 | 1090 | Al Jabalain vs AL Riyadh | 1.61 | 3.49 | 5.23 |
| 18:00 | 3672 | Benfica U23 vs Portimonense U23 | 1.34 | 4.85 | 6.79 |
| 18:00 | 3836 | FK Panevezys B vs Be1 NFa | 4.58 | 3.90 | 1.60 |
| 19:00 | 1403 | CSA Steaua Bucuresti vs Unirea Dej | 1.75 | 3.52 | 4.10 |
| 19:00 | 4361 | Hadiya Hosahina FC vs Legetafo Legedadi | 1.96 | 3.06 | 3.79 |
| 19:30 | 4733 | Aris Limassol vs Omonia Nicosia | 2.15 | 3.31 | 3.31 |
| 19:35 | 3840 | AL Sahel SC vs Al Qadisiyah | 2.71 | 2.81 | 2.66 |
| 20:00 | 3049 | Fenerbahce vs Sivasspor | 1.37 | 4.89 | 7.19 |
| 20:00 | 3084 | FA Siauliai B vs Riteriai B | 2.75 | 3.50 | 2.38 |
| 20:00 | 3628 | Maccabi Petach Tikva vs Bnei Yehuda | 1.62 | 3.66 | 5.62 |
| 20:00 | 3724 | Akritas Chlorakas vs AEK Larnaca | 5.79 | 3.99 | 1.55 |
| 20:00 | 4285 | Hapoel Rishon Lezion vs Hapoel Afula | 2.25 | 3.05 | 3.35 |
| 20:00 | 5351 | Hatayspor vs Basaksehir | 4.09 | 3.39 | 1.87 |
| 20:00 | 5558 | Ironi Hasharon vs El Fahem | 3.41 | 3.06 | 2.22 |
| 20:15 | 2927 | Stomil Olsztyn vs Kotwica Kolobrzeg | 2.58 | 3.41 | 2.39 |
| 21:00 | 1488 | Midtjylland vs Nordsjalland | 2.06 | 3.49 | 3.29 |
| 21:00 | 2192 | Karmiotissa vs Apollon Limassol | 4.20 | 3.55 | 1.82 |
| 21:00 | 2797 | Villefranche Sur Saone vs Nancy | 2.05 | 3.35 | 3.35 |
| 21:00 | 3221 | CD Trofense vs Benfica Lisbon B | 3.96 | 3.61 | 1.80 |
| 21:00 | 4787 | Paris 13 Atletico vs Orleans | 2.77 | 3.06 | 2.52 |
| 22:00 | 1679 | Jong PSV vs Almere City | 2.21 | 3.54 | 2.85 |
| 22:00 | 2886 | CFR Cluj vs U Craiova SA | 1.68 | 3.53 | 4.97 |
| 22:00 | 4446 | Jong AZ Alkmaar vs Roda Kerkrade | 2.91 | 3.40 | 2.24 |
| 22:00 | 5308 | Jong Utrecht vs FC Eindhoven | 3.16 | 3.55 | 2.05 |
| 22:30 | 1757 | Reggina vs Genoa | 3.03 | 3.18 | 2.30 |
| 22:30 | 2204 | Foggia vs Avellino | 1.99 | 3.34 | 3.74 |
| 22:30 | 5841 | Juventus Youth vs Inter Youth | 1.44 | 4.59 | 5.27 |
| 22:45 | 1088 | Bracknell Town vs Ipswich | 12.87 | 7.33 | 1.15 |
| 22:45 | 1520 | Metz vs St Etienne | 2.18 | 3.27 | 3.17 |
| 22:45 | 3734 | Chelmsford vs Dover | 1.88 | 3.40 | 3.64 |
| 23:00 | 1024 | Marsa FC vs Swieqi United FC | 2.55 | 3.04 | 2.65 |
| 23:00 | 2879 | Red Star vs Dunkerque | 2.06 | 3.21 | 3.46 |
| 23:00 | 3242 | Lugo vs FC Cartagena | 2.68 | 2.93 | 2.73 |
| 23:00 | 4835 | Rayo Vallecano vs Real Madrid | 4.91 | 4.01 | 1.62 |
| 23:15 | 3154 | GD Chaves vs Santa Clara | 2.32 | 3.08 | 3.13 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe

Jumatatu Novemba 7, 2022




Pique astaafu rasmi Barca

UKURASA 29

FETTY DENSA...



Fatma Issa maarufu Fetty Densa, akimiliki mpira dhidi ya Ireen Lungu katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake dhidi ya Green Buffaloes ya Zambia iliyopigwa Uwanja wa Grande de Stade Marrakech juzi usiku. Simba Queens ilishinda mabao 2-0 na kufuzu hatua ya nusu fainali. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# NABI AIPA ULINZI, MBINU YANGA SC

**Na Saada Akida**

## ●●● Aificha nyumbani kwao, sasa kuipeleka Uwanja wa Club Africain kesho, asema...

BAADA ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, kuhakikisha Yanga inakuwa salama katika kambi yake ya siku tatu iliyoweka mjini Sousse ambapo ndipo nyumbani kwake, mwalimu huyo sasa atakiongoza kikosi hicho kesho, Jumanne kuelekea jijini Tunis itakapopigwa mechi ya mkondo wa pili ya mchujo dhidi ya Club Africain kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

**Sousse ambako ndio nyumbani kwa Nabi, Yanga ilitua hapo tangu Jumamosi kujiandaa na mechi hiyo itakayopigwa Uwanja wa Olympique Hamadi Agrebi jijini Tunis, ambapo ni umbali wa takriban Km. 140 kutoka walipo.**

Katika mechi hiyo, Yanga inahitaji sare yoyote ya mabao ama ushindi ili kufuzu na kama matokeo yatakuwa suluhu, basi changamoto ya mikwaju ya penalti itachukua nafasi yake, hiyo ikitokana na sare tasa timu hizo zilipokutana Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumatano iliyopita.

Kikosi hicho kimejichimba katika mji wa Sousse chini ya Nabi kikijifua vikali mara mbili kwa siku, asubuhi na jioni lengo likiwa ni kuhakikisha kinapata matokeo mazuri na kusonga mbele hatua ya makundi baada ya kupoteza nafasi kama hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kutolewa na Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anaifahamu timu ya Club Africain inapokuwa nyumbani tofauti na walivyocheza ugenini katika mechi yao ya kwanza.

Alisema kila mchezaji anatakiwa kuwa makini na kufanya majukumu yake kwa kuzingatia vitu muhimu anavyowapa mazoezini hasa kuongeza umakini kwenye mipira ya faulo kutokana na ubora wa Club Africain katika idara hiyo.

"Hatutaki kuruhusu wapate bao katika mipira hiyo ya adhabu, lakini mabeki kuwa makini zaidi na washambuliaji wa Club Africain kwa sababu mechi yao ya mwisho nyumbani walishinda mabao 7-0 dhidi ya Kipanga.

"Katika mechi hiyo walifunguka kwa sababu wako nyumbani, ugenini hawakucheza hivyo, kwa kuwa tumeona ubora wao hatutakiwi kuwapa nafasi ya

INAENDELEA UK. 31

# Simba Queens rasmi yabeba mil. 540/- CAF

**Na Somoe Ng'itu,** MARRAKECH

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, kikosi cha Simba Queens, kinatarajia kupokea zawadi ya zaidi ya Sh. milioni 540, imefahamika.

Fedha hizo wanazotarajia kupata Simba Queens ni Dola za Marekani 200,000 (sawa na Sh. milioni 465.4 zinazotolewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) kwa kufika hatua hiyo huku klabu ya Simba ikiahidi kuwazawadia Sh. milioni 100.

Simba Queens itacheza mechi ya hatua ya nusu fainali keshokutwa dhidi ya mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Queens kutoka Afrika Kusini ambayo jana usiku ilitarajia kukutana na TP Mazembe Queens kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Akizungumza na wachezaji wa Simba Queens kabla ya kuikabili Green Buffaloes juzi usiku, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema klabu inakiamini kikosi hicho na wanachotakiwa ni kuendelea kupeperusha vema bendera ya Tanzania.

Barbara alisema wachezaji wanatakiwa kucheza kwa bidii katika mechi zote na waamini wao ni moja ya timu bora na ndio maana wamefika katika hatua hiyo.

"Napenda kuwaambia klabu imepanga kuwapa Sh. milioni 100 kama bonasi endapo leo (juzi) mtashinda, ninajua klabu ina mambo mengi, lakini kwa sasa tumeweka nguvu na akili katika upande wenu ili kuhakikisha tunashinda kila mechi iliyoko mbele yetu," alisema Barbara.

Naye Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, alianza kwa kumshukuru Mungu kwa matokeo mazuri aliyopata na kusisitiza wamekuja Morocco kuchukua kikombe cha mashindano haya ya kimataifa na makubwa kwa ngazi ya klabu kwa wanawake barani Afrika.

Lukula alisema baada ya kumaliza dakika 45 za kwanza bila kupata bao, alitumia muda wa mapumziko kuwaambia wachezaji

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >